# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Arobaini na Nne – Tarehe 14 Agosti, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA HAIDI MKULO):** Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Benki ya Posta, Tanzania *(TPB)* kwa Mwaka 2006 *(The Annual Report and Accounts of the Tanzania Postal Bank for the year 2006)*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 405

**Utafiti wa Uchimbaji wa Madini**

**MHE. SAID AMOUR ARFI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwepo harakati za utatifi na uchimbaji wa Madini (*drilling*) kwa zaidi ya miaka sita huko Lukoma kati ya Mwese na Mwambao wa Ziwa Tanganyika:-

(a) Je, ni nini matokeo ya utafiti huo na kwa sababu gani umechukua muda mrefu?

(b) Kwa kuwa, Makampuni ya *Geo-Search, Drill Corp, Stanley* na *Tan Drill* kwa nyakati mbalimbali yamekuwa yakifanya kazi Lukoma, nini mahusiano ya kampuni hizo na matokeo ya utafiti wa kampuni?

(c) Je, utafiti huo wa muda mrefu umelinufaisha Taifa kwa kiasi gani, au hasara ambayo Taifa limepata kutokana na kuchukuliwa mawe yaliyochimbwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba niungane na wenzangu kukupa pole wewe kwa msiba mkubwa uliokupata, msiba wa Taifa kwa kumpoteza Mzee wetu Marehemu Chifu Abdallah Said Fundikira.

Lakini pia nitoe pole kwa Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa kufiwa na Baba mzazi wake. Mwenyezi Mungu Aziweke Roho za Marehemu wote Mahali Pema Peponi, Amin!

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naomba sasa kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini na kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, utafutaji wa Madini hutumia mbinu za kijiofizikia, kijiokemia na kijiolojia katika kujua aina na ukumbwa wa mashapo ya Madini katika eneo husika kabla ya hatua za uendelezaji mgodi kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, chini ya Sheria ya Madini ya mwaka 1998, leseni ya utafutaji wa Madini (*Prospecting Licence*) huweza kuendelea kuwa hai kwa muda wa miaka saba. Hata hivyo, kazi ya utafutaji Madini inaweza kuchukuliwa muda mrefu zaidi kutegemea upatikanaji wa Madini ya kutosha kufungua mgodi na mwenendo wa soko la Madini yanayotafutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kampuni ya *Nyati Mining* (*Tanzania Limited*) ya Australia tangu mwaka 2000 imekuwa ikifanya utafutaji wa Madini katika eneo la Lukoma ambalo lina miamba inayoambatana na Madini ya kundi la Platinamu yaani (*Platinum Group of Elements*), ambayo ni Platinamu, Nikeli na *Cobalt*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo ya utangulizi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, lenye sehemu a, b, na c na ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, matokeo ya kazi ya utafutaji Madini iliyofanyika katika eneo la Lukoma ni kugunduliwa kwa Madini ya kundi la Platinamu *(Platinum Group of Elements*) ambapo kampuni ya *Nyati Mining (Tanzania) Limited* ilitangaza ugunduzi huo Agosti 2001. Shughuli za utafutaji Madini zinaendelea kwa mujibu wa Sheria ya Madini ili kugundua Madini ya kutosha yatakayowezesha mgodi kufunguliwa katika eneo hilo.

(b) Mheshimiwa Spika, kampuni za *Geo-Research, Drill Corp, Stanley* na *Tan Drill* zilikodiwa na kampuni ya *Nyati Mining (Tanzania) Limited* kufanya shughuli za uchorongaji wa miamba katika eneo la Lukoma ili kupata sampuni za miamba iliyo chini ya ardhi kwa ajili ya uchunguzi wa kitaalamu ukiwemo wa kimaabara.

(c) Mheshimiwa Spika, manufaa ya utafutaji unaoendelea katika eneo la Lukoma ni upatikanaji wa taarifa za kuwepo Madini ya kundi la Platinamu na kufahamu mifumo ya kijiolojia katika eneo hilo. Taarifa hizi huvutia uwekezaji. Aidha, kazi za utafutaji Madini zinapofanyika katika eneo lolote nchini likiwemo eneo la Lukoma huchangia kutoa ajira na kuongeza biashara za bidhaa za wananchi wa eneo husika. Miundombinu kama Barabara imeboreshwa na uwanja wa ndege umejengwa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba hakuna hasara inayopatikana kutokana na mawe yanayochukuliw akama sampuli wakati wa utafutaji wa Madini kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Said Amour Arfi swali la nyongeza.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, utafutaji wa Madini wa aina kama uliokuwa ukifanyika kule Lukoma umefanyika pia kule Karema katika eneo la Kaparamsenga na kampuni ya Anglo America mpaka saa matokeo ya uchunguzi huo hayakufahamika lakini inasadikiwa kwamba sampuni zilizokuwa zikitoka pale zikipakiwa ndani ya Meli na kupelekwa Kigoma kwa ajili ya kupelekwa Dar es Salaam na kusafirishwa nje zilikuwa zikibadilishwa zikiwa ndani ya Meli na kupelekwa Zambia na baadaye Afrika ya Kusini.

Je, Serikali itakuwa tayari kuchunguza kama hilo lilikuwa limefanyika? Kama ni kweli au si kweli na kama si kweli ni kiasi gani cha mawe ambacho Serikali inafahamu yamesafirishwa kutoka huko Karema?

Pili, kwa kuwa, mwambao wa Ziwa Tanganyika na Wilaya ya Mpanda inaelekea kwamba ina Madini ya kutosha. Je Serikali itawasaidia vipi wachimbaji wadogowadogo ili waweze kupata zana za kweza kufanya utafiti wa kutosha katika miamba migumu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu mawali mwili ya nyongeza ya kutoka kwa Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda, kati kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza niseme tu kwamba Serikali haina taarifa kwamba kumekuwa na sampuli ambazo zimekuwa zikisafirishwa na baadaye zinabadilishwa na kwa usimamizi ambao tunao tuna imani kwamba pamoja na kuheshimu sana kauli ya Mheshimiwa Mbunge lakini kwa udhibiti ambao Serikali imekuwa ikifanya kupitia Wizara zetu za Serikali tunajua kwamba ambacho Mheshimiwa Mbunge amekisema bado hakijathibitishwa lakini tunaheshimu kauli yake na tutaendelea kuifanyia kazi kuona kama hizi tuhuma ama hisia ambazo amezisema zinaweza kuwa za kweli.

Lakini mpaka sasa hivi Serikali imekuwa ikifuatilia jambo hili kwa karibu na hatuna taarifa zozote zilizowasilishwa na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu ni kiasi gani cha mawe ni kama nilivyosema kwamba hizi ni takwimu ambazo zinahitaji kuwa makini zaidi kuzitoa katika Bunge lako Tukufu. Kwa hiyo, niseme tu kwamba Ofisi yetu tutajiridhisha kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge ni kiasi gani cha sampuni ambacho mpaka sasa hivi kimeshachukuliwa kwa sababu takwimu zipo ofisini, hili halina tatizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili kwamba mwambao wa ziwa Tanganyika na maeneo ya Mpanda na Serikali itawasaidia vipi wachimbaji wadogo wadogo ni kwamba tumekuwa tukiliarifu Bunge lako Tukufu na tutaendelea kuliarifu tena kwa mara nyingine kwamba Serikali inandaa utaratibu mzuri lakini mojawapo ambacho tunakifanya ni kuwahamasisha wachimbaji wadogo wajiandae na wajiunge katika vikundi ambavyo itakuwa rahisi kwa Serikali kuweza kushirikiana na wadau wengine kuwawezesha kwa namna mbalimbali ikiwemo mitaji kwa sababu vinginevyo kwa mmoja mmoja itakuwa ni kazi ngumu kidogo.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine tutaendelea kutenga maeneo ya wachimbaji wadogowadogo mahususi kwa ajili yao tu na kama ambavyo tumeliarifu Bunge lako Tukufu mara kadhaa ni maeneo kadhaa yameshatengwa mpaka sasa hivi na tutaendelea na zoezi hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ponsiano Damiano Nyami, nilikuona kwa swali la nyongeza.

**MHE. PONSIANO DAMIANO NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, huu utafiti uliofanyika kwenye maeneo ya Lukoma na maeneo ya Karema pamoja na maeneo ya Mwese ulionekana kuwa una matunda kidogo.

Lakini vilevile maeneo ya Kabwe, Kipili, Kirando pamoja na Chala na kipande eneo la Nkasi ni maeneo ambayo yana Madini mengi na wachimbaji wadogo wadogo wanachimba sana hasa dhahabu, rubi na kunaonekana kama vile kuna almasi.

Je, ni lini ambapo Serikali inafikiria kufanya utafiti katika eneo la Nkasi pamoja na eneo la kuelekea Zambia kule maeneo ya Kasanga, Serikali itafanya utafiti lini kwa sababu ninaamini kwamba kuna Madini mengi ukitilia maanani kwamba upande wa Zambia eneo hilo hilo la Ziwa Tanganyika na upande wa Kongo wanachimba Madini mengi. Kwa nini utafiti usifanyike eneo la Nkasi pamoja na Kasanga?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ponsiano Damiano Nyami kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kimsingi ni karibu nchi nzima imeshafanyiwa utafiti na Wizara yetu ina taarifa kwa maeneo mbalimbali kuhusu viwango vya Madini yanayopatikana ama raslimali ya Madini yanayopatikana katika nchi hii.

Kwa hiyo, nimkaribishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba endapo kuna watu wanahitaji kujua takwimu sahihi zilizopo na Madini gani yapo maeneo gani na kwa kiwango gani na *licence* zake zikoje nimkaribishe tu Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa wengine ofisini. Lakini pia tuwakaribishe wawekezaji ambao wana dhamira ya kuwekeza katika nchi hii wawe wa ndani ama nje ya nchi waje tu kwani zoezi hili limekuwa likiendelea siku zote. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge leo maswali ya nyongeza nitaruhusu mengi zaidi kwa sababu maswali ya msingi ni machache. Kwa hiyo tunaendelea bado na Wizara hii na nitamkaribisha Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba kwa swali la nyongeza.

**MHE. KABUZI FAUSTINE RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza.

Watafuta Madini wakubwa au wachimbaji wakubwa huchukua muda mrefu sana kutafuta Madini na kwa bahati mbaya sana huchukua maeneo makubwa sana ambayo husababisha wachimbaji wadogo kukosa maeneo na hii inatokana kwamba sheria hairuhusu wachimbaji wadogo kuingia kwenye maeneo ya wachimbaji wakubwa. Je, Serikali inasemaje kuhusu wachimbaji wadogo?

Kwa kuwa wachimbaji wakubwa huwa wanalenga kwenda chini kwa nini wachimbaji wadogo wasiruhusiwe kuendelea wakati utafiti unaendelea wao wawe wanachimba kidogokidogo ikishaonekana kuwa na mgodi basi wakawaachia wale wachimbaji wakubwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba Mbunge wa Busanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utafutaji ama uchimbaji wa Madini kwa nchi nyingine unaongozwa na Sheria pamoja na Kanuni ambazo tumejiwekea kama nchi na ninaomba kukumbusha kwamba kiwango cha mwisho cha utautaji wa Madini kwa licence mbalimbali licence ya kwanza ambayo ni ya utafiti awali ni miaka miwili na huwa haihuishwi na tulishalieleza Bunge hili tukufu na tutaendelea kufanya hivyo.

Lakini pia, leseni nyingine huwa haizidi miaka saba kama ambavyo tumekuwa tukisema. Sasa kwa jambo hili ufafanuzi ni wazi kwamba utafutaji wa Madini unaendelea kwa Sheria na kipindi cha mwisho kabisa cha juu ni miaka saba.

Mheshimiwa Spika, Lakini kusema kwamba wachimbaji wadogo waruhusiwe mahali ambapo kuna wachimbaji wakubwa kwa sababu wenyewe wanchimba kwa kwenda chini zaidi. Maelezo sahihi ni kwamba kimsingi tunaogopa sana kugonganisha vibali vya shughuli za Madini katika maeneo husika kama ilivyo shughuli nyingine, tunaogopa sana *double allocation* kwa sababu ukiruhusu kila mtafutaji ama mchimbaji anafanya kwa mujibu wa Sheria na ana kibali chake. Ukiruhusu wafanye hivyo itakuwa ni usumbufu na itakuwa ndiyo mwanzo wa migogoro.

Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwamba tuendelee kukubaliana kwamba tukubaliane na Taratibu na Kanuni na pia Sheria ambazo tumeziweka kama nchi na tuziheshimu lakini tuwahamasishe wachimbaji wadogo kwamba mara wanapobaini kwamba kuna mahali kuna Madini basi wafuate taratibu za kawaida kupitia Ofisi zetu za Madini ili wapate vibali vya kumiliki kwa sababu kama mchimbaji mdogo yupo basi mchimbaji mkubwa hawezi kuruhusiwa kupewa eneo hilo ambalo mchimbaji mdogo analo. Kwa hiyo, wote wanapata fursa sawa kwa kiwango cha shughuli ambazo wanazifanya. (*Makofi*)

**SPIKA:** Swali la mwisho la nyongeza kwa wizara hii, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, swali la msingi linahusu mchanga wa dhahabu unaochimbwa na ndani ya mchanga huo kunakuwa na Madini mengine ya platinamu na nikeli.

Je, Serikali ina utaratibu gani hivi sasa wa kuweka kiwanda cha kuchambua Madini yaliyobaki kwa maana ya kigezo kuwa na mchanga mwingi ndiyo iweze kuendeshwa kibiashara. Je, migodi iliyokuwepo haiwezi kukidhi wingi wa mchanga huo na *process* hiyo ikafanyika hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, zinavyoelezea Sera za Chama cha Mapinduzi ni kwamba shughuli za kibiashara ni kwamba zinaendeshwa na soko huru na ziko huru kwa wote lakini tunafahamu kwamba pia ni muhimu Serikali ikashiriki kwa namna moja ama nyingine kwenye maeneo ambayo inaona kwamba ni vema kulinda maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa hivi sasa tunaona tumshauri na tumkumbushe na tuendelee kushauriana kama ambavyo tulishawahi kusema katika Bunge hili Tukufu tuwahamasishe wawekezaji wa ndani na nje ya nchi wawekeze. Tumeshasema mara kadhaa kwamba shughuli za uwekezaji katika shughuli hizi mitaji yake ni mikubwa lakini tunaamini kwamba wawekezaji wenye dhamira kweli wakipatikana jambo hili linaweza kuendelea.

Mheshimiwa Spika, tunachofanya sasa hivi kama Serikali ni kwamba tunaendelea kuwahamasisha wawekezaji mbalimbali ili waweze kujenga kiwanda cha kuchambua Madini mbalimbali hapa nchini na zoezi hili linaendelea. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kwa mujibu wa desturi za kuendesha shughuli za Mabunge katika Jumuiya ya Madola anaposimama Kiongozi wa Upinzani huwezi kumpuuza, kwa hiyo Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante na ninakushukuru sana, lakini nina swali dogo la nyongeza.

Katika swali la msingi na majibu ya msingi aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza kwamba Serikali inafuatilia kwa makini sana hawa wachimbaji wa migodi mikubwa na midogo.

Katika taarifa ya Hesabu za Serikali iliyotolewa katika Bunge lako Tukufu mwaka 2003 ilibaini kwamba almasi zinazosafirishwa Tanzania Wizara yetu ya Madini ilikuwa na taarifa chache kuliko taarifa ambazo tumezipata kutoka *TANSORT* iliyopo London na pamoja na dhahabu ambayo ilikamatwa kwenye makontena mbalimbali.

Je, haoni bado udhibiti wa hii raslimali yetu kutoka Serikalini bado haujakuwa sawasawa na kwamba kuna haja sasa ya kutafuta utaratibu madhubuti zaidi wa kuimarisha udhibiti wa raslimali zetu?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama ulivyozungumza ukisema kwamba Kiongozi wa Upinzania anapouliza swali ni hadhi vilevile akajibiwa na Waziri yule yule mwenye dhamana. (*Kicheko /Makofi*)

Baada ya hapo napenda kijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kama kuna Madini yoyote ambayo yanafuatiliwa kwa karibu sana basi ni almasi, waheshimiwa Wabunge kama kuna yeyote ambaye ameweza kutembelea mgozi wa Almasi wa Williamson Diamond kuona jinsi unavyoingia kule milango unayopitia na mahali ambapo almasi yenyewe imehifadhiwa na wale wanaoichambua wala hawaigusi.

Mheshimiwa Spika, wanapitisha mkono wao kwenye tundu angeweza kujua kwamba kweli pale pana udhibiti mkali sana na ni kweli tunaweza kutambua kwamba kuna wachimbaji wadogo wadogo ambao labda wanaweza kuwa wanapenyesha ile almasi kupitia njia za panya.

Lakini kwa wachimbaji wakubwa ambao ni Williamson Diamond pamoja na sasa hivi kuna mwingine ni Elhilary wana udhibiti wa kutosha na hizo taarifa tunajua kwamba hata Mkaguzi wa Serikali mwaka jana alikuwa amesema kwamba almasi iliyokuwa imekuwa *sorted* pale haionekani lakini baada ya kuangalia vitabu ilikuwa ni vitabu tu almasi yenyewe ikapatikana.

Lakini pili, kwa upande wa dhahabu migodi yote ambayo inachimbwa dhahabu tulikuwa tunatumia wakaguzi *Alex Stuart* ambao katika taarifa yao imeonyesha kwamba hakuna upotevu wa dhahabu katika migodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo nataka kuwahakikishia wananchi kwamba kwa wachimbaji wakubwa kuna udhibiti wa kutosha na kwa wachimbaji wadogo jinsi tutakavyoweka hii Sekta ya wachimbaji wadogo kuwa katika mfumo rasmi na yenyewe udhibiti utaongezeka na mwaka huu sisi kama Serikali tutachukua kile kitengo cha usimamizi wa ukaguzi na tutaendeleza kuwa na juhudi lakini angalizo alilotoa Mheshimiwa Mbunge hatutalipuuza. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri na sasa swali linalofuata linaelekezwa Wizara hiyo hiyo na lingeulizwa na Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, ambaye simwoni humu ndani kwa hiyo naona amemkabidhi Dr. Harrison George Mwakyembe.

Na. 406

**Makaa ya Mawe – Kiwira na Mchuchuma**

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE (K.n.y. MHE. VICTOR KILASILE MWAMBALASWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imedhamiria kutatua tatizo sugu la upatikanaji wa umeme nchini kwa kutotegemea maji peke yake kwa kuzalisha umeme na hivyo kutegemea pia gesi na makaa ya mawe, na kwa kuwa, makaa ya mawe ya Kiwira na Mchuchuma yana majivu (*ash-content*) ambayo yana *impact* kubwa kwenye mazingira:-

(a) Je, makaa ya mawe ya Kiwira na Mchuchuma yana kiasi gani cha majivu *(ash-content)?*

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kwa uharibifu wa mazingira kwenye mgodi wa Kiwira ambao umeanza kufanya kazi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu a na b kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, makaa ya mawe ya Mchuchuma yanapatikana katika miamba ya tabaka la shale na *sandstone*. Makaa ya mawe yanapatikana kwenye mwamba wa tabala ya shale yana majivu kati ya 25% na 50% na yale ya kwenye tabaka la *sandstone* yana majivu kati ya 10% na 20%.

Mheshimiwa Spika, makaa ya mawe ya Kiwira yanapatikana katika miamba ya tabaka la shale pekee na yana kiwango cha majivu kati ya asilimia 25% na 50% kama ilivyo kwa mwamba wa tabaka la shale wa makaa ya Mchuchuma.

Mheshimiwa Spika, makaa ya kwenye miamba ya tabaka ya shale yanaweza kuoshwa ili kupunguza taka na hivyo kupata majivu kiasi cha asilimia chini ya 25%.

(b) Mheshimiwa Spika, Mwekezaji hulazimika kukamilisha taratibu zote zinazotakiwa Kisheria zikiwemo kuandaa na kuwaslisha tathmini (*Environmental Impact Assessment* (*EIA*) na mpango wa kudhibiti na kupunguza athari kwa jamii na MAZINGIRA (*Environmental and Social Management Plan* (*ESMP*) kwa athari ambazo zimekwishaainishwa kwenye *EIA*. Lengo ni kuweka bayana faida na athari za mradi kwa jamii na mazingira na mbinu zitakazotumika katika kumaliza kabisa au kupunguza athari. Taarifa hizo hukubalika na kuanza kutumika baada ya kupitiwa na wadau wote, wakiwemo wananchi wa eneo ambalo mradi utakuwepo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kampuni ya *Tanpower Resources Limited* kumiliki mgodi wa makaa ya mawe Kiwira kupitia kampuni yake tanzu ya *Kiwira Coal and Power Limited* ilifanya tathmini ya athari kwa mazingira na jamii na kuainisha mpango wa udhibiti wa athari kwa mazingira na jamii.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango wa hifadhi ya mazingira uliokubalika, mgodi wa Kiwira pia huboresha maji yatokayo kwenye mgodi na mtambo wa kuzalisha umeme kwa kutumia kemikali. Vilevile, mawe yanayotoka mgodini (*waste rock*) husagwa na kutumika katika uzalishaji wa umeme. Majivu yatokayo kwenye mtambo wa kuzalisha umeme hutumika kutengenezea Barabara na matofali.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu ili kuhakikisha kwamba mgodi wa Kiwira unatekeleza hifadhi ya mazingira kama ilivyobainisha katika mpango wake wa hifadhi ya mazingira ikiwemo kutumia mawe na majivu kwa matumizi mbadala endelevu.

**MHE. PROF. RAPHAEL BENEDICT MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninaomba niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, swali la msingi linahusu mbadala wa vyanzo vya umeme unaotegemea maji ambayo ni makaa ya mawe na gesi. Je, nini kinaendelea kuhusiana na mradi wa Mchuchuma kwa kuzingatia kwamba tafiti zote zinazohusu mradi huo zimekamilika na vilevile ilani ya Chama cha Mapinduzi inataka kwamba mradi huo uwe umeanza kutekelezwa ifikapo mwaka 2010? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Prof. Raphael Benedict Mwalyosi, kama ifuatavyo:-

Kweli tunatambua umuhimu wa Mradi wa Mchuchuma kama tulivyouahidi katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi lakini katika kuangalia mradi wa Mchuchuma una sehemu mbili, Mchuchuma una sehemu ya Makaa na Liganga na una sehemu ya Chuma.

Sehemu ya Makaa ya Mchuchuma tafiti zimekwisha kamilika lakini sehemu ya Liganga ya Chuma utafiti haujakamilika kabisa. Tungeweza sasa hivi tukaanza kuzalisha umeme kutokana na makaa ya Mchuchuma.

Lakini mkaa ule tukiumaliza tutashindwa kupata Nishati ya kuweza kufua chuma ambacho kinatokana na Liganga. Kwa kuangalia hilo hii miradi yote inabidi kuanza sambamba kwa sababu sasa hivi hatuna tatizo kubwa la umeme la kuharakisha Mchuchuma.

Afadhali tungoje tafiti za Liganga zikamilike kusudi Liganga itakapoanza isije ikakosa Nishati kwa sababu utakuta tumeshamaliza kutumia mkaa na kwa sasa hivi Mshauri Mwelekezi amekwisha tafutwa ili kuweza kusaidia Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko katika kuendeleza kwa haraka tafiti za Liganga ili mradi wa Chuma na mradi wa Mkaa wa Mchuchuma viende kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. ENG. STELLA MARTIN MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii niulize swali dogo sana la nyongeza kwa kuzingatia swali la msingi.

Kwa kuwa hivi kuna *NGOs* pamoja na Wajasiriamali ambao wameamua kuendeleza Nishati hii ya kutumia makaa kwa ajili ya kupikia. Je, Wizara imeshawasiliana na *TBS* pamoja na Wataalamu wengine kuona kwamba mkaa huo unaotumika hauna athari kwa binadamu ukizingatia kwamba *carbon monoxide* inakuwepo pia kwenye Makaa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yetu inatambua uweo wa wajasiriamali wadogo na *NGOs* ambao sasa hivi zinaendelea kutumia Nishati ya makaa ya mawe na ofisiyetu imekuwa ikiwasiliana na hawa wajasiriamali mara kadhaa.

Lakini naomba nitumie fursa hii kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba kile ambacho kinafanywa na wajasiriamali kimeshazingatia taratibu zote na Wizara inatambua hilo na Idara zote za Serikali zimeshiriki kuhakikisha kwamba kile ambacho wanakileta sokoni kwa watumiaji ni kwa maslahi ya afya na kwa maslahi ya wananchi kwa kuzingatia Kanuni na Taratibu zote ambacho zimewekwa na nchi yetu.

**SPIKA:** Nimemwona Mheshimiwa John Samwel Malecela swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninapenda kuuliza swali la nyongeza.

Wachina kule Kiwira waliweza wakatengeneza *brickets* za mkaa wa mawe wakichanganya na udongo ili ziweze kutumiwa na watu wa kawaida bila sufuria zao kuharibika na ikaonekana kwamba inawezekana.

Je, Serikali haioni umuhimu hasa kwa wakati huu ambapo tunasema kukata miti ni kuharibu mazingira. Serikali ingeingiza hata sehemu ya fedha ika-*invest* katika mradi wa namna hiyo ili *brickets* hizo zikapatikana kwa urahisi hasa mijini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli alichokisema Mheshimiwa Malecela kilishafanyika miaka ya nyuma na ofisi yetu inafahamu. Lakini nitumie fursa hii kulihakikishia Taifa kwamba ushauri wa Mheshimiwa Waziri Mkuu Mstaafu tunauchukua na tutaufanyia kazi.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa swali la msingi lilikuwa linaulizia upatikanaji wa umeme na kutumia nishati mbadala ya maji yaani makaa ya mawe na nishati zingine. Je, kwa kuwa Mkoa wa Rukwa haujaunganishwa katika gridi ya Taifa na kule Muze kuna *deposit* kubwa ya makaa ya mawe ambayo yameshaanza kuchimba. Je, Serikali itakuwa tayari kufanya utafiti kuona makaa ya mawe ya Muze kwamba yanaweza kuzalisha umeme kwa ajili ya Mkoa wa Rukwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, tunazingatia ushauri wake na Wizara yetu inafahamu lakini taratibu zinaendelea kubaini ni kiwango gani kipo pale kama kinaweza kuzalisha nishati ambayo inahitajika. Lakini ushauri wake tunauchukua na tutaendelea kuufanyia kazi na tumkaribishe ili kupata taarifa kwa kadri siku zinavyokwenda kwa sababu jambo hili linaendelea kufanyiwa kazi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea sasa na Wizara ya Maliasili na Utalii kuna Mbunge mmoja ameniandikia kwa nini naonekana kuchekacheka peke yangu, hivi leo?

Jana katika gazeti la NIPASHE kuna takwimu muhimu sana kwa nchi yetu zimejitokeza, ukurasa wa 3 wa NIPASHE linasema:- "Asilimia 54 ya wanamume wa Tanzania hupigwa na wake zao". Halafu linaendelea: "Wanaume wengi wanaopigwa na wake zao hawajitokezi kupata msaada wa kisheria kutokana na kuona aibu kuwa kufanya hivyo ni kujidhalilisha". Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa Kituo cha Elimu na Mahusiano ya Kifamilia Bi Mwadawa Lugongo akizungumza na NIPASHE kuhusu masuala mbalimbali ya familia. Alisema: "Utafiti uliofanywa unaonyesha kuwa asilimia 54 ya wanamume hapa Tanzania wanapigwa na wake zao lakini hawatoi taarifa sehemu

zinazohusika, kutokana na hali hiyo alisema wanaume hao huamua kukaa kimya kwa muda mrefu hali inayowasababishia msongo wa mawazo". Halafu inaendelea.

Sasa kwa nini nacheka? Unajua nikiwatazama kama Mheshimiwa Mwinchoum, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, sasa nikiwatazama najiuliza, huyu naye yumo katika kundi hilo la kupigwa na mke wake? *(Makofi/Kicheko)*

Lakini pia nikiwatazama, maana yake takwimu hizi sisi ni wawakilishi wa nchi. Kwa hiyo, kama takwimu hizi zimekaa sawa asilimia 54 ya Wabunge hupigwa na wake zao. Lakini pia kuna Wabunge wanawake humu. Kwa hiyo, nikimtazama kama Naibu Waziri TAMISEMI hivi naye huwa anapiga mumewe? (*Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge tunahamia Wizara ya Maliasili na Utalii.Swali linauliza na Mheshimiwa Mgana Msindai. Jamani, hebu mwangalieni naye sasa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakikishie huwa sipigwi na mke wangu. *(Makofi)*

Na. 407

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa, inaonekana kwamba, katika kipindi kifupi kijacho, Maaskari wa Wanyamapori, Maafisa Wanyamapori Wasaidizi na kwa upande wa Misitu, Maafisa Misitu Wasaidizi na Walinzi wa Hifadhi zetu wengi wamefikia/wamekaribia muda wao wa kustaafu, jambo linaloashiria kuwepo kwa upungufu mkubwa wa watumishi katika siku za usoni na hivyo kuwa na dalili za kuongezeka kwa wimbi la ujangili katika maeneo hayo kama hatua za makusudi hazitachukuliwa:_

Je, Serikali inasema nini juu ya hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Wizara yangu imekuwa ikiwasiliana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kila mwaka kuomba nafasi za ajira mpya (Ikama) na ajira mbadala ili kupata watumishi wa kuziba nafasi zilizoachwa wazi kutokana na baadhi ya watumishi kustaafu, kufariki, kufukuzwa au kuacha kazi. Hatua hii inalenga katika kuiwezesha Wizara kuwa na idadi ya Watumishi inayokidhi mahitaji ya sekta husika.

Idara ya Wanyamapori kwa sasa ina jumla ya watumishi 1,171. Ili iweze kusimamia majukumu ya uhifadhi wa wanyamapori ipasavyo, inahitaji kuwa na watumishi 3,943. Hivyo kuna upungufu wa watumishi 2,772, katika mwaka 2007/2008 Wizara inatarajia kuajiri jumla ya watumishi 60.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeweka mikakati katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa wafanyakazi na kuongeza ufanisi katika Uhifadhi Wanyamapori kama ifuatavyo:-

Wizara yangu itapanua uwezo wa vyuo vya mafunzo ya taaluma ya wanyamapori (Mweka na Pasiansi) kwa kukarabati miundombinu iliyopo na kuongeza majengo mapya (mabweni na madarasa) ili kuviongezea vyuo vyetu uwezo wa kupokea wanafunzi wengi zaidi kuliko ilivyo sasa. Utekelezaji utafanyika kwa awamu kwa kutegemea upatikanaji wa fedha za Maendeleo.

Aidha, Wizara itatekeleza kazi zake kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola kama Jeshi la Polisi na Mahakama ili kuongeza uwezo wetu wa kupambana na kudhibiti vitendo vya ujangili nchini.

Kuendeleza ushirikiano na wadau mbalimbali katika uhifadhi wa wanyamapori. Mfano ni ushirikishaji wa wananchi katika uhifadhi kwa kuanzisha maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori *(WMA)* na kushirikiana na Kampuni za uwindaji wa kitalii.

Kununua vifaa vya doria:- Wizara imeweza kununua vifaa kwa ajili ya doria. Vifaa hivyo ni mahema, silaha za kisasa, risasi na magari. Vile vile Wizara ina mpango wa kununua ndege mpya aina ya *Caravan* 208 yenye uwezo wa kubeba watu 13 na imekarabati ndege zote 4 zilizopo. Ndege zote hizi ni kwa ajili ya kuwezesha doria na uokoaji. Aidha, rubani mmoja amepatiwa mafunzo, hivyo Idara ina jumla ya marubani watatu.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Misitu na Nyuki ina jumla ya watumishi 1,784 na ili iweze kufanya kazi vizuri inahitaji jumla ya watumishi 2,037 ikiwa na upungufu wa watumishi 253. Kutokana na upungufu huu katika mwaka wa fedha 2007/2008 Wizara inatarajia kuajiri jumla ya watumishi 77. Aidha, kuanzia mwaka wa fedha 2007/2008 hadi 2010/2011 idadi ya watumishi wanaotarajia kustaafu katika Idara ya Misitu na Nyuki katika kada mbalimbali za misitu ni 165.

Wizara baada ya kuona tatizo la upungufu wa watumishi ilichukua hatua za makusudi ikiwa ni pamoja na kusajili na kutoa mafunzo katika ngazi ya stashahada na stashahada kwa wanafunzi watarajali, mpango ambao ulianza mwaka 2003/2004 katika Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi na Chuo cha Misitu Olmotonyi, Arusha. Kutokana na idadi ndogo ya wanachuo wanaosajiliwa katika Chuo cha Misitu Olmotonyi na Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi, Wizara imeweka mkakati wa muda mfupi na mrefu ili kukabiliana na tatizo hili kama ifuatavyo:-

Mkakati wa muda mfupi kwa kutumia miundo mbinu iliyopo Mkakati huu unalenga kukarabati mabweni na madarasa ambayo hayatumiki na kununua vifaa vya kufundishia. Baada ya ukarabati Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi kinaweza kudahili wanafunzi wapya 47 tofauti na ilivyokuwa ikichukua wanafunzi 15 kwa mwaka. Aidha, Chuo cha Misitu Olmotonyi, baada ya marekebisho kitaweza kudahili wanafunzi wapya 121 badala ya wanafunzi 46 kwa mwaka.

Mkakati wa muda mrefu katika Chuo cha Misitu Olmotonyi utalenga kuongeza idadi ya madarasa, mabweni, vifaa vya kufundishia na wakufunzi ili hatimaye Chuo kiwe na uwezo wa kudahili wanafunzi 160 kila mwaka. Aidha, Chuo cha Viwanda vya Misitu, mkakati utalenga kufanya yafuatayo: Ujenzi wa vyumba vya madarasa, maabara, maktaba, ofisi, kuongeza idadi ya mabweni, kupanua jiko, kuongeza idadi ya wakufunzi na kununua vifaa vya kufundishia. Mkakati huu utakiwezesha chuo kuwa na uwezo wa kudahili wanafunzi 80 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Wizara itakuwa inajaza nafasi wazi kwa kadri zitakavyojitokeza kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza kwa kuwa Serikali imekiri kwamba kuna upungufu mkubwa sana wa askari wa wanyamapori na kwa kuwa upungufu huu ndio unaosababisha kwenye baadhi ya vitalu, wenye vitalu kujiwindia kadri wanavyopenda kwa sababu hakuna askari wa kuwadhibiti. Akiwinda mnyama mkubwa, akipata mwingine huyu anamtupa anachukua yule mkubwa zaidi, Serikali haioni kwamba tunapoteza heshima na mapato makubwa ya Serikali na vile vile kumaliza wanyama wetu?

Pili, kwa kuwa upungufu huu utachukua muda mrefu kuziba. Je, Serikali iko tayari kuajiri *Village Scouts* kusaidia kulinda maliasili zetu?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli katika jibu langu la msingi nimeeleza kwamba kwa kweli tuna upungufu mkubwa sana wa askari wanyamapori. Lakini vile vile nimeeleza mikakati ambayo Serikali inachukua ili kuongeza idadi hiyo.

Lakini kuhusu wenye vitalu kuwinda watakavyo, kwa utaratibu uliopo wakati ambapo kuna uwindaji wa kitalii huwa kuna askari wanyamapori kutoka katika Halmashauri husika ambaye anakuwa na mwindaji wa kitalii ili kuhakikisha kwamba anawinda kwa jinsi ambavyo ameelekezwa.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile katika Chuo chetu cha Mweka mwaka huu tutaanza kufundisha wawindaji bingwa ambao nao pia baadaye tutakuwa tukiwatumia katika uwindaji wa kitalii badala ya wawindaji wa kitalii kuja na wawindaji bingwa wao wenyewe.

Kuhusu upungufu ambao inaelekea na ni dhahiri kwamba itachukua muda mrefu suala la kuajiri *Village Scouts* ni suala ambalo linazungumzika na nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tumelipokea na tutalifanyia kazi.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Swali la msingi la Mheshimiwa Msindai linazungumzia upungufu mkubwa sana wa watumishi hasa kwa Idara ya Wanyamapori kwa ajili ya kusimamia mapori ya akiba yanayoitwa *Game Reserves*.

Imekuwa ni mapendekezo ya muda mrefu ya Kamati ya Maliasili na Mazingira, kwa Wizara ya Maliasili na Serikali kwamba ili kumaliza tatizo hili la ufumbuzi halisi ni kuipunguzia Idara ya Wanyamapori majukumu ili iendelee kushughulikia sera, sheria na mambo mengine kwa kuunda Shirika jipya litakalosimamia mapori yote ya akiba *Game Reserves* zote. Shirika kama *TANAPA* lakini litasimamia *Game Reserves* zote. Je, sasa Serikali iko tayari katika marekebisho ya sheria itakayokuja mwezi Novemba au Januari kuingiza jambo hili la kuunda Shirika jipya?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kutokana na upungufu wa wanyamapori ni kwamba kuna pendekezo ambalo linasema kwamba kuundwe Shirika ambalo litasimamia *Game Reserves* zote.

Mheshimiwa Spika, ombi hili tulikwishalieleza katika Kamati kwamba tumelichukua na tunalifanyia kazi na tutaona jinsi ambavyo tunaweza tukalichukulia. Ahsante.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ajira ya askari wanyamapori katika Mashirika yaliyoko chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Na kwa kuwa ajira ya askari hawa ni ya mwaka mmoja lakini wanaweza waka-*renew* mkataba kila baada ya mwaka mmoja.

Je, isingekuwa busara kuajiri askari hawa wapate ajira ya kudumu baada ya miaka mitatu ili kuziba nafasi ya hawa askari wanyamapori ambao wamekaribia kustaafu?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira ya hawa askari wanyamapori wa Mashirika kwamba waajiriwe badala ya kuwa wanafanya kazi kwa mkataba kwa kweli itategemea na ajira ambazo tutazipata kutoka Idara Kuu ya Utumishi na kutokana na sifa za hao askari wanyamapori.

Na. 408

**Kilimo cha Muhogo Nchini**

**MHE. RAYNALD A. MROPE (K.n.y. CAPT. GEORGE MKUCHIKA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, zao la Muhogo hustawi sana Mikoa ya Mwambao mwa Tanzania ikiwa ni pamoja na Mkoa wa Mtwara; na kwa kuwa, Mihogo toka Mtwara ilisaidia kupunguza tatizo la njaa mwaka 1983 kwa kupelekwa Mikoa ya Lindi, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Tabora, Tanga, Mwanza na Mara chini ya usimamizi wa aliyekuwa Waziri Mkuu wakati huo Hayati Edward Sokoine; na kwa kuwa, hivi sasa mihogo hainunuliwi na Vyama vya Ushirika wala wafanyabiashara binafsi, hivyo wakulima wa zao hilo kukosa soko:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuliendeleza zao hilo ili lisaidie katika mapambano ya njaa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Capt. George Mkuchika, Mbunge wa Newala, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Uhimizaji wa uzalishaji wa zao la muhogo umekuwa ukifanywa na Mkoa wa Mtwara mara kwa mara na ulijiwekea lengo la chini la kila kaya kulima ekari mbili. Uhimizaji huu ni pamoja na kampeni zilizofanyika za Ondoa Njaa Masasi (ONJAMA) katika Wilaya ya Masasi kati ya mwaka wa 1987 na 1988; Tulime Tuongeze Mazao Newala (TUTUMANE) katika Wilaya ya Newala kati ya mwaka 1988 na 1989; kujitosheleza kwa Chakula na Kukuza Uchumi Mtwara (KUCHAKUMI) katika Wilaya ya Mtwara kati ya mwaka wa 1988 na 1989; Kilimo cha Wakazi wa Mtwara – Mikindani (KIWAMI) na Tulime Tuongeze Mazao Tandahimba (TUTUMATA) katika mwaka wa 1996. Pamoja na Kampeni hizo, Mkoa ulifanya mikutano ya kuhimiza kilimo mmojawapo ukiwa Mkutano Mkuu wa Kilimo uliofanyika Agosti, 2003.Aidha, sehemu kubwa ya muhogo ambao umekuwa ukizalishwa Mikoa ya Mwambao mwa Tanzania umekuwa ukiuzwa nje ya nchi, kwa mfano kati ya mwaka wa 1984 na 1994 wastani wa tani 15,309.864 ziliuzwa nje ya nchi kila mwaka kati ya tani 345,805 zilizozalishwa katika kipindi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Mkuchika, kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inayo mipango ya kuliendeleza zao la muhogo ikiwa ni pamoja na kuanzisha mashamba ya vipando bora vya mihogo vyenye ukinzani dhidi ya magonjwa na tija kubwa ili kupata vipando vya kuwapatia wakulima. Vipando hivyo vinazalishwa katika Magereza ya Lilungu liliko katika Manispaa ya Mtwara Mikindani na Namajani liliko katika Wilaya ya Masasi. Vipando vipatavyo 3,000,000 vitakavyozalishwa kwenye mashamba hayo vitatosha kupanda hekta 300 na kusambazwa kwa wakulima. Magereza

inategemewa kuwa chimbuko la kudumu la vipando bora vya mihogo kwa ajili ya Mkoa wa Mtwara na hasa Wilaya ya Newala ambayo ni mzalishaji mkubwa wa muhogo.

(b) Serikali kupitia Mradi wa Ushirikishwaji na Uwezeshaji wa Jamii *(PADEP)*, inaendesha mafunzo ya usindikaji wa zao la muhogo ambapo vikundi vya wakulima wanapatiwa mashine za kusindika muhogo. Lengo ni kuwafundisha wakulima mbinu ya kuongeza thamani ya muhogo na kumpunguzia harubu ya kubeba na kusafirisha malighafi. Aidha, wakulima watapata bei nzuri kwa kuuza muhogo uliosindikwa na pia unaweza kuhifadhiwa kwa muda mrefu zaidi hivyo kuwawezesha wakulima kuwa na uhakika wa usalama wa chakula.

Pamoja na juhudi za kusambaza vipando, Serikali inaendelea kufanya utafiti ili kupata vipando vya mihogo inayoweza kutoa wanga mwingi.Hadi sasa vipando vya Naliendele 90/034, Kitumbua, Kigoma Red, Kalulu na Kiroba, ambavyo vina uwezo wa kuvumilia magonjwa na tija yake ni kubwa, vimesambazwa katika Mkoa wa Mtwara.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri ningependa kuuliza. Kwa kuwa itakuwa ni busara kubwa kuongelea thamani ya zao hili la muhogo na hasa katika masoko ya hapa nchini na nchi za nje. Je, Wizara haioni umuhimu wa kuanzisha Kiwanda Maalum cha Kusindika muhogo ili kupata wanga, gundi na kadhalika katika maeneo haya ya Mkoa wa Mtwara na hasa katika kijiji cha Chiwanga ambacho wananchi wa Newala walikwishatoa ardhi.

Pili, hivi karibuni kumekuwa na magonjwa mengi ya zao hili la muhogo hasa virusi vinavyoishambulia majani na mizizi. Je, Serikali inasema nini na hasa ina mpango gani wa kuweza kuondoa magonjwa haya ili tuweze kuongeza zao hili la muhogo katika mikoa hii ya Pwani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. DAVID M. DAVID):** Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali haianzishi Viwanda, Serikali haijengi viwanda lakini Serikali inatengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kujenga viwanda. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tunahamasisha wafanyabiashara na wawekezaji kutoka nje na ndani ya nchi kuanzisha viwanda vya kutengeneza, kusindika muhogo ikiwa ni pamoja na kutengeneza wanga kwa ajili nguo na kutengeneza nishati mbadala, vyakula vya mifugo kutengeneza biskuti pamoja na kutengeneza vifungashio. Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Spika, Serikali sasa hivi inaendelea na teknolojia ile ya kuzalisha mihogo ambayo iko *resistance* na magonjwa. Kwa mfano tuna *research* inayoitwa *molecular breeding* ambayo inazalisha mihogo yenye ukinzani wa magonjwa pamoja na vidudu vinavyoshambulia mihogo lakini pia mihogo hii inayozalishwa kutokana na njia hii inatoa mavuno mengi. Pili, tuna *tissue culture* inatuhakikishia kuzalisha mazao mengi ya mihogo lakini pia mihogo inatokana na *tissue culture* ina vimelea vichache ama hakuna kabisa vile vinavyo *affect* mihogo.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa kichocheo kikubwa cha uzalishaji ni kuwa na soko la uhakika. Kwa kuwa mwaka juzi Serikali iliarifiwa rasmi kupata mnunuzi wa muhogo wa tani laki moja kupeleka India na Serikali ikamshauri mnunuzi huyo kwamba ajenge kiwanda badala ya kununua muhogo. Hivi sasa wakulima wa Kusini wamepata soko la tani milioni moja kwenda China kupeleka mihogo na tani laki mbili kupeleka Finland lakini hatuna hatua yoyote iliyochukuliwa.

Je, Serikali itawasaidiaje wakulima wa mikoa ya Kusini ili kuweza kuyatumia masoko haya kama kichocheo cha wakulima kuweza kuongeza uzalishaji.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. DR. M. DAVID):** Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali kuwasaidia wananchi wanaolima mihogo kwa kanda hii ya Pwani lakini pia maeneo mengine Tanzania nzima. Ushauri wake huo nimeuchukua na tutaufanyia kazi na pengine tukitoka hapa ningependa tuonane naye kusudi tuweze kupata *details* zaidi za kuweza kuona uwezekano wa kutumia hayo masoko ya nje.

Na. 409

**Uhaba wa Walimu Shule za Sekondari Geita**

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA (K.n.y. MHE. ERNEST G. MABINA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika kutumiza malengo ya Serikali ya muda mrefu katika ujenzi wa Shule za Sekondari, Wilaya ya Geita imefanikiwa kujenga shule katika kila Kata hivyo kutimiza Ilani ya Uchaguzi wa CCM kabla ya muda uliopangwa; na kwa kuwa, katika shule hizo hakuna walimu, vitabu, moja na vitu muhimu vinavyohitajika:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzipatia shule hizo walimu wenye ujuzi;

(b) Je, kwa nini Serikali isichimbie katika kila shule kisima kirefu cha maji ili kunusuru maisha ya walimu na wanafunzi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina, Mbunge wa Geita lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuwapongeza wananchi wa Geita kwa kufanikiwa kujenga Shule ya Sekondari katika kila Kata. Katika utekelezaji wa Mipango

ya MMEM na MMES, suala la kuandaa walimu bora na wenye ujuzi linazingatiwa. Wizara imeandaa Mkakati wa kupata walimu wa kuweza kukidhi mahitaji shuleni.

Kwa mfano katika mwaka wa 2007/2008 jumla ya walimu 6,733 wa Shahada na Stashahada wanatarajiwa kuhitimu kutoka katika Vyuo vya Ualimu na Vyuo Vikuu. Walimu hao wataajiriwa na kupangwa katika Shule za Sekondari zikiwemo za Wilaya ya Geita. Hivyo Wizara itaendelea na kuwapanga katika Mikoa.

Aidha Mkoa wa Mwanza utawapanga walimu hao katika shule za Geita kadri watakavyopatikana. Muhimu ni kwa wananchi kuendelea kuandaa mazingira mazuri kwa walimu hasa ujenzi wa nyumba za walimu na kuwapokea vizuri walimu wapya wanapopelekwa huko.

(b) Mheshimiwa Spika, wazo la kuwa na kisima kirefu cha maji kwa kila shule ili kunusuru maisha ya walimu na wanafunzi na wazo zuri. Serikali imekuwa ikitoa fedha kupitia MMES kwa ajili ya kuchangia nguvu za wananchi katika ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Kwa mpango huu wa kushirikiana, tunawaomba wananchi kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Geita kuendelea na kushirikiana ili kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa kile shule inakuwa na chanzo cha maji safi na salama vikiwemo visima vya maji.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniruhusu kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na jitihada za wananchi wa Geita kuna tatizo kubwa la walimu na si tatizo kubwa la walimu tu kuna shule nyingi mpaka sasa hivi hazina Walimu Wakuu. Kwa mfano shule ya Nyakagomba, shule ya Nyamigota na shule ya Msalala. Shule ya Msalala wanafunzi wamefikia hatua ya kuchagua walimu ambaye ni Mkuu wa Shule, mwalimu wa kujitolea na wiki mbili zilizopita walikwenda wakaguzi pale kwa sababu hajui utaratibu wakamfukuza akasema wapitie kwa Diwani wakarudi bila kufanya kazi.

Je, Serikali sasa inaweza ikachukua hatua za maksudi kwenda katika Wilaya ya Geita kupeleka Walimu Wakuu kwa shule zote badala ya kuachia matatizo?

La pili, shule za sekondari za Geita ziko 43, ni tatu tu ambazo zina umeme zingine hazina umeme.

Je, Wizara ina mpango gani kuweza kuwasaidia angalau jenereta kila shule katika fedha hizo za MMES waweze kuwa na jenereta au solar angalau vijana wetu waweze kufanya kazi kama vijana wengine ambao wanapambana katika mashindano ya elimu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu inatambua tatizo hili la walimu nchi nzima hasa linatokana na ongezeko kubwa la shule za sekondari zilizoweza kujengwa na wananchi katika kipindi hiki cha miaka hii miwili.

Lakini kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi nimeeleza wazi kwamba Wizara inampango thabiti ya kuweza kupata walimu wa kutosha katika kipindi kifupi ili tuweza kuhakikisha kwamba kila shule inapata walimu wa kutosha; na hivyo kwa shule zile ambazo hazina Walimu Wakuu mchakato wa kuendelea kuwateua Walimu Wakuu wa shule hasa shule hizi mpya bado unaendelea na kama ilitokea mwalimu muda wa muda akateuliwa kuwa Mkuu wa Shule ni bahati mbaya kwa sababu Maafisa wetu wanaelekezwa ni nini la kufanywa pale shule mpya inapoanzishwa na hakuna Mwalimu Mkuu.

Hivyo Wizara yangu itatoa maelekezo kwa Maafisa Elimu wa Mkoa wa Mwanza ili wahakikishe kwamba wanateua watu wenye sifa na wenye uzoefu ili waweze kufanya kazi hiyo ya kukaimu nafasi ya Ualimu Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, tunawapongeza wananchi wa Geita kwa kuwa na shule za sekondari 43 lakini kwa sababu tatizo hili la umeme ni la nchi nzima ukiangalia asilimia ya wananchi wanaopata umeme ni kiasi kidogo sana hasa vijijini ni kweli hata shule zetu za sekondari karibu nyingi sana hazina umeme.

Lakini tunashauri Walimu Wakuu waangalie jinsi ya kuweza kuwapatia wanafunzi umeme wa jenereta kwa kuangalia fedha zile wanazopewa zile za *capitation*. Pia fedha wanazozalisha katika shule ambazo ni za miradi yao wanaweze kutumia jenereta na shule nyingine wanatumia *solar*.

Tunawashauri wajaribu kuangalia ni umeme upi utakaowafaa wakati huu ambapo Serikali inajipanga kuangalia ni jinsi gani umeme utasambazwa vijijini kwa ajili ya kuwasaidia wananchi pamoja na shule zetu za sekondari ambazo zimetawanyika nchi yote ya Tanzania.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niongezee kwa majibu mazuri aliyoyatoa Naibu Waziri kuhusu swali la nyongeza hasa la kwanza kuhusu upatikanaji wa walimu na nimeona ni vizuri niongezee taarifa tu kwamba baada ya mwaka jana na mwaka huu kupeleka jumla ya Walimu 7,872 tumeona ni vizuri tufanye tathimini kwanza kuona hali ilivyo mashuleni.

Sasa hivi taarifa zinaendelea kupatikana kutoka kwa waratibu wa elimu ya sekondari nchi nzima ili kuona hali ilivyo mashuleni ili tuweze kujua angalau shule zina walimu wangapi hasa hizi mpya. Kwa hiyo ni zoezi ambalo ni muhimu lifanyike nchi nzima kuona hali halisi baada ya kupeleka idadi kubwa ya walimu ili tuone.

Je, katika hawa walimu tunaotarajia kuwapata 6,733 mwaka huu kutoka vyuoni watatosheleza au tuchukue hatua nyingine ya dharura kama ambavyo tumeshafanya kwa siku zilizopita. Niliona ni vizuri kutoa taarifa hii ili wananchi waelewe kwamba Wizara inafuatilia kwa karibu sana hali ya walimu ilivyo mashuleni.

Na. 410

**Ubovu wa Barabara ya Sengerema Kahunda – Lushamba**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA** aliuliza:-

Kwa kuwa msitu wa Buhindi ulioko Tarafa ya Kahunda Wilayani Sengerema unaipatia Serikali fedha nyingi sana kutokana na uvunaji wa miti.

Je, Serikali haioni haja ya kuitengeneza barabara ya kutoka Sengerema, Kahunda hai Lushamba kwa kutumia fedha zinazotokana na uvunaji miti ambayo ni mbaya sana kiasi cha kusababisha malori yanayobeba miti hiyo kukwama?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Sengerema – Nyamazugo – Nyehunge –Kahunda ni barabara ya Mkoa na inahudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Mkoa wa Mwanza. Hali ya barabara hii kati ya Sengerema – Nyamazugo hadi Nyehunge ni ya wastani na inapatikana vizuri kufuatia matengenezo ya dharura yaliyofanyika hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Nyehunge –Kahunda yenye urefu wa Km. 34 ni mbaya kutokana na mvua na mafuriko yaliyotokea kati ya mwezi wa Desemba 2006 na Machi 2007. Barabara hii itafanyiwa matengenezo katika mradi wa *PMMR (Perfomance Based Management and Maintenance of Roads)* ambapo barabara hii baada ya kufanyiwa matengenezo itakuwa chini ya uangalizi wa mkandarasi kwa muda wa miaka mitano. Mradi huu unaotegemewa kuondoa adha kwa watumiaji wa barabara hii, unafadhiliwa na Benki ya Dunia pamoja na Serikali yetu, Mkataba unategemewa kusainiwa mwezi huu na kazi zitaanza mwezi Septemba mwaka huu.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa tarehe 6 mwezi wa nane nililalamikia usafiri wa maji kwa watu wa Tarafa hii ya Kahunda wa kwenda Maisome nikaambiwa nirudi kwenye Halmshauri yangu. Leo tena barabara hii ya hawa wakazi wa Kahunda ni mbaya sana na Mheshimiwa Waziri amekiri. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri anieleze leo kwamba sasa huo mkataba ambao atasaini ni wa lami au wa changarawe?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, itakuwa ya changarawe imara. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha sasa matangazo.

Wageni na wale ambao ni mara yao ya kwanza wafahamu kwamba ninapowatamka wanaombwa wasimame ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuwatambua. Wageni wa Mheshimiwa Yusuf Rajabu Makamba, kwanza ni Mheshimiwa Jaka Mwambi, Naibu Katibu Mkuu wa CCM Tanzania Bara, karibu sana Ndugu Mwambi. Ndugu Mwambi amefuatana na wafuatao Bi. Maria Sarungi *Director* wa *Miss Universe,* Karibu sana.

Lakini amepambwa na Bi. Flaviana Matata ambaye ni Mshindi wa *Miss Universe* toka Afrika karibu sana sana. Yupo pia Easther Baruti ambaye ni Afisa Mratibu wa *fund raising* kwa masuala ya watoto *SOS Children Villeges in Tanzania* pamoja nao yupo Afisa wa Makao Makuu ya CCM, Dodoma anaitwa Ndugu Agnes Hokororo, yule pale.

Waheshimiwa Wabunge, Bi. Flaviana Matata atakuwepo nasi kwa siku nzima na baadaye atahitaji kukutana na Waheshimiwa Wabunge nadhani tutamwomba Mheshimiwa Jenista Mhagama Kamati ya Maendeleo ya Jamii, ili ufanyike utaratibu wa kuelezea matatizo haya ya *SOS* ambayo Bi. Flaviana anayasimamia wanahitaji msaada kwa watoto yatima na sisi kama Wawakilishi wa Wananchi daima tuko mstari wa mbele kusaidia wale ambao ni wanyonge zaidi. Kwa hiyo, kutakuwa na utaratibu utatangazwa kukutana na timu nzima hii ili kuona namna gani sisi tunaweza kuchangia katika kupunguza matatizo ya watoto yatima kupitia Asasi hii ya *SOS*.

Wageni wengine ni kama ifuatavyo, mgeni wa Mheshimiwa Waziri Sofia Simba na Mheshimiwa Juma Kapuya na Mbunge Ponsiano Nyami, huyu ni mgeni wa wote hawa watatu huyu si mwingine ni Bi Asha Baraka Mmiliki wa Bendi ya Twanga Pepeta yule pale. Ahsante sana Bi Asha Baraka, kazi nzuri sana unaifanya katika jamii ni bahati mbaya katika burudani za Waheshimiwa Wabunge haikuwezekana kuwaona vijana wa Twanga Pepeta lakini nadhani katika Mkutano wa Tisa utaratibu utaweza kufanywa ili tuburudike. Si rahisi kwetu kwenda kumbi kama zile za Magomeni Kondoa na kwingine. Kwa hiyo, huwa tunafurahi kama tunawapata Twanga Pepeta hapa hapa. Tunaomba uwasalimie vijana na wafanye mazoezi ya nguvu. *(Makofi)*

Kuna Mgeni mwingine wa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa Nazir Karamagi ambaye ni Bwana Athar Mwakapugi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini yule pale. Karibu sana.

Mgeni wa Mheshimiwa Naibu Waziri Dr. Luka Siyame ni Lucky Siyame ambaye ni mtoto wake yule pale. Mgeni wa Mheshimiwa Emmanuel Luhahula ambaye ni Martha Luhahula, yule pale karibu sana mama. Wageni wa Wabunge wa Mkoa wa Rukwa ni kama ifuatavyo Ndugu Andrew Ngindo, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Rukwa, Williad Njenje Katibu wa Jumuiya ya Wazazi, Suleiman Namanga Mjumbe wa Baraza Kuu Wazazi Taifa CCM.

Wageni wa Mheshimiwa Beatrice Shellukindo ni Steven Ngonyani Mjumbe Baraza la Wazazi Tanga, Bi. Mery Chatanda, Katibu wa CCM Mkoa wa Morogoro, yule pale na Mashaka Mhando Mwandishi wa Majira Tanga.

Viongozi wa Serikali ya Chuo cha *St. Augustine University of Tanzania* waliopo hapa, ni Ndugu Revocatus Kasimba Rais wa Chuo yule pale. Deodatus Kazinja Waziri Mkuu na Edson Kamkala Waziri ambaye hakutajwa Waziri wa kitu gani, lakini zamani walikuwa wanaitwa *Without portfolio.* Karibuni sana tunawakaribisha hapa. Wapo pia wanafunzi 50 kutoka Shule ya Sekondari ya Msalato Dodoma baadhi yao tulikuwa nao jana nadhani wanakuja kwa makundi. Karibu sana vijana na walimu wa Msalato na tunawapongeza sana kwa matokeo mazuri ya mitihani mwaka hadi mwaka. *(Makofi)*

Wanafunzi 40 wa awali na msingi Ignisius Dodoma nadhani wamekosa nafasi. Wanafunzi 26 kutoka chuo cha walimu Selesian Seminari Dodoma wale pale karibuni sana Walimu na Walimu watarajiwa. Wanafunzi 40 wa awali na msingi wa Shule ya Chemchem Dodoma wale pale karibuni sana walimu na wanafunzi.

Wanafunzi 50 kutoka shule ya Msingi Makole Dodoma hao hapo pamoja na Walimu wao. Shule hii kwa kiasi kikubwa ina walimu wanawake tu. Lakini nadhani ni mambo mazuri tu. Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji ameomba kwamba nitangaze mgeni wake ambaye ni Bwana Ali Tamim Hali Katibu wa Wazazi Katibu wa Wazazi Mkoa wa Kusini Unguja yule pale karibu sana na mwanae Mheshimiwa Mbunge ambaye anaitwa Makame Haji Mwita.

Mikutano:- Lediana Mafuru Mng'ong'o Katibu wa Wanawake Wabunge wa CCM anaomba kwamba wanachama au Wajumbe wakutane leo saa saba mchana kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa Gedion Cheyo ameniomba nitangaze kuwa kutakuwa na kikao saa saba mchana cha wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, ukumbi namba 432 hivi leo.

Ninaomba wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi, Tume ya Huduma za Bunge Kamati ya Kanuni za Bunge tukutane katika ukumbi wangu, saa saba na robo leo mchana pamoja na Kamati wale wa Kamati ndogo iliyopitia Kanuni za Bunge ili tuhitimishe kazi tuliyoianza hapo jana.

Kuna tangaza limekuja sasa hivi. Jana wakati ninatangaza ushindi wa timu ya soka mpira wa miguu kwa bahati mbaya kwa sababu tangazo lililetwa papo kwa papo na lilikuwa refu sikuweza kuona kumbe timu yetu ya Netiboli imefanya vizuri sana na haielezwi hapa kama ilishinda lakini, *ok* ilishinda basi maana yake imesema tu nitambue ushajaa ni pamoja na kushindwa.

Lakini nawapongeza sana sana timu yetu ya Netiboli na nimeombwa niwataje kwa makhususi ni Mheshimiwa Mwaka, na Mheshimiwa Grace Kiwelu walichomoza hawa kwa uchezaji bora zaidi kulikoi wengine. Nashukuru sana ahsante sana.

## HOJA BINAFSI ZA WABUNGE

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita mtoa hoja ambaye ni Mheshimiwi Kabwe Zuberi Zitto nilikuwa na taarifa tu kwamba ilikuwapo pia Hoja Binafsi ya Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa inayohusu anayodai yeye ni matumizi mabaya ya fedha katika Benki Kuu ya Tanzania.

Lakini hoja za namna hiyo na hasa inapogusa Taasisi nzito kama Benki Kuu ya Nchi ilikuwa inabidi nijiridhishe mimi mwenyewe kwamba yanayosemwa humo katika hoja angalau yana ushahidi wa awali. Kwa sababu tabu ya Waheshimiwa Wabunge jina la mtu au la Taasisi huwa linachafuliwa mara hoja ikifika mezani.

Sasa itakapogundulika kwamba yaliyosemwa si sahihi bado haisadii kwa sababu taasisi au mtu anakuwa amekwisha chafuliwa. Kwa hiyo, katika hali hiyo Maspika huwa waangalifu sana. Maspika huwa waangalifu sana wanataka ushahidi zaidi uendane na hizo hoja.

Kwa hiyo, nilimwomba Mheshimiwa Dr. Slaa na sasa hivi naambiwa imeandaliwa ni *book* kubwa sana. Sasa mpaka nitakapolitathmini na kuona kama linalingana na hoja anayoitoa ndipo nitaweza kupanga hoja yake katika orodha ya shughuli. Kwa leo tutakuwa na hoja hii ya Mheshimiwa kabwe Zuberi Zitto. Kwa hiyo, namwita ili aweze kuwasilisha hoja yake.

Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto tunafuata taratibu zile zile za hoja za kawaida kwamba mtoa hoja anapata dakika zisizozidi 60. Hii siyo ya Bajeti, hii ni hoja ya kawaida tu.

Kwa hiyo, inakwenda na utaratibu wake dakika zisizozidi 60 halafu nitaita upande wa Serikali, Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi, Waziri wa Nishati na Madini, kwa muda ambao hauwezi ukakadiriwa kwa sababu atakuwa anajibu hoja zote za ile hoja kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo nitaita wachangiaji kadiri ambavyo mtakuwa mnaleta majina. Kwa hiyo, sasa ni Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto.

### Uchunguzi wa Mapitio ya Mikataba ya Madini

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, Maelezo yangu kuhusu Hoja ya kuundwa Kamati Teule ya Bunge kuchunguza mapitio ya Mikataba ya Madini na mazingira ya kusainiwa kwa Mkataba (*MDA*) mpya wa madini wa Buzwagi kulikofanywa na Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa Nazir Karamagi, huko Uingereza Mwezi Februari 2007. Nawasilisha maelezo haya kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni 104(2) Toleo la mwaka 2004

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunipatia fursa ya kuleta hoja hii hapa kwenye Bunge lako Tukufu kwa mujibu wa kanuni zetu za Bunge. Kuletwa kwa hoja hii, bila kujali maamuzi ya kuhusu hoja yenyewe, ni ishara

tosha ya ukomavu wa demokrasia yetu ambayo inakuzwa na mijadala ya Bunge lako Tukufu. Nakupongeza kwa dhati kabisa kwa juhudi zako za kuliimarisha Bunge letu na kujenga muhimili imara wa ulinzi wa demokrasia ya vyama vingi nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 16/7/2007 mara baada ya hoja ya Waziri wa Nishati na Madini kuamuliwa na Bunge lako Tukufu nilisimama mahala pangu na kutoa taarifa ya kukusudia kuleta hoja ya kuunda Kamati teule ya Bunge.

Mheshimiwa Slpika, nilisema kama ifuatavyo (kwa mujibu wa kumbukumbu sahihi za Mijadala ya Bunge), ninanukuu '…… naomba kutoa Taarifa Rasmi za Bunge…… kwamba nakusudia kuleta hoja ya kuunda Kamati Teule kuchunguza mkataba mpya wa Madini ambao Waziri wa Nishati na Madini ameusaini bila kuzingatia maagizo ya Rais (wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) ya kupitia mikataba aliyoyatoa mbele ya Bunge lako tukufu tarehe 30 Desemba, 2005. Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, nimeshawasilisha hoja yangu hii kwa maandishi kwa Katibu wa Bunge na sasa nawasilisha rasmi katika kikao hiki cha Bunge kwa uamuzi. Nimezingatia kanuni 104 (2) katika kuwasilisha hoja yangu.

Mheshimiwa Spika, katika maelezo yangu niliyowasilisha Bungeni wakati wa mjadala wa Hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini siku ya tarehe 16/7/2007 nilihitaji maelezo kutoka serikalini katika masuala makuu mawili yafuatayo:-

(i) Kusainiwa kwa Mkataba mpya wa wa Madini wa mgodi (mradi) wa Buzwagi kati ya Serikali na Kampuni ya Barrick na sababu za mkataba huo kusainiwa nje ya nchi, London Uingereza.

Mheshimiwa Spika, vile vile kwa nini mkataba huo umesainiwa wakati bado serikali inafanya durusu (*review*) ya mikataba kufuatana na maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. *(Makofi)*

(ii) Kuondolewa kwa kipengele katika Sheria ya Kodi ya mapato ya mwaka 1973 kuhusiana na asilimia 15% ya *Capital allowance on unredeemed qualifying capital expenditure* bila ya kibali cha Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, wakati akijibu hoja zangu Waziri wa Nishati na Madini alijenga hoja zake kama ifuatavyo:-

Kusainiwa kwa Mkataba wa Mgodi (Mradi) wa Buzwagi.

Mheshimiwa Spika, Wakati akijibu hoja yangu kuhusiana na suala la Mkataba mpya wa mgodi wa Buzwagi, Waziri wa Nishati na Madini amenukuliwa na kumbukumbu za majadiliano ya Bunge akisema kama ifuatavyo, nanukuu:-

"Mheshimiwa Spika, katika tathmini ya Migodi, Mgodi wa Buzwagi ni *Marginal Mine* ambao uhai wake si wa muda mrefu. Bila ya kutumia fursa ya bei ya Dhahabu uwekezaji wake usingeweza kuwa wa faida. Hata hivyo, Mkataba wa Buzwagi hauna mapungufu yaliyokuwamo kwenye mikataba ya zamani". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Waziri alikiri mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba amesaini Mkataba huo jijini London Uingereza.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Mikataba ya Madini ni mchakato ambao mwisho wake ni kuletwa kwa sheria ya madini hapa Bungeni na kuifanyia marekebisho ili kuiboresha na kuondoa mapungufu.

Hivyo, mpaka hapo sheria itakaporekebishwa ndipo tutasema tumemaliza zoezi la kupitia mikataba ya madini na hivyo kusaini mikataba mipya na makampuni yote ya madini yaliyopo nchini na yatakayokuja kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, suala ambalo linanipelekea kuomba kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge kuchunguza mkataba huu mpya ni kuhusu uharaka uliopelekea Waziri wa Nishati na Madini kusaini Mkataba huu. Sheria ya Madini bado haijarekebishwa.

Je, Waziri anatumia vigezo gani kusema mkataba mpya wa Buzwagi aliousaini London hauna mapungufu?

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Nishati na Madini aliliambia Bunge lako Tukufu kuwa Buzwagi ni *Marginal Mine*. Vile vile Waziri anasema kuwa Kampuni ya Barrick inamiliki migodi mitatu tu kupitia kampuni zake tanzu ambazo ni Bulyanhulu *Gold Mine, North Mara Gold Mine* na *Pangea Minerals Limited* Tulawaka. Kwa maelezo haya ya Waziri Karamagi, Buzwagi sio Mgodi.

Mheshimiwa Spika, hoja hii ya kuwa Buzwagi sio mgodi inashabihiana kabisa na hoja ya Kampuni ya *Barrick* kwamba Buzwagi ni *Project.* Taarifa ya kampuni hii ya *Barrick Gold Corporation-Global Operations - Africa* - Buzwagi, inaonesha kuwa Buzwagi ni mradi. Taarifa hii nimeiambatanisha katika hoja hii.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya *Barrick, Annual Review* 2006 inasema ifuatavyo katika ukurasa wa 23, naomba kunukuu: "*A major milestone was reached in February, 2007 when we signed a mineral Development Agreement (MDA) with the Tanzanian Government. In 2007, we expect to complete a detailed construction design and receive Environmental Impact Assessment Approval approval"*.

Mheshimiwa Spika, suala ambalo vilevile linanisukuma kuomba Bunge lako Tukufu kuunda Kamati Teule ni kwamba, iwapo Buzwagi sio mgodi bali ni mradi, ni kwa nini tumesaini *Mineral Development Agreement (MDA)* mpya? Kwa kuwa *Pangea Minerals* Tulawaka ndio inaonekana kumiliki mradi huu, je, Serikali imefanya

marekebisho tu ya *MDA* na Kampuni ya *Barrick?* Naomba Kamati Teule ichunguze ni nini kilichosainiwa, marekebisho ya mkataba wa Tulawaka au *MDA* mpya ya Buzwagi?

Mheshimiwa Spika, Buzwagi inashika nafasi ya pili kwa uwekezaji wa *Barrick* katika migodi hapa nchini. Wakati Kampuni hii inawekeza dola za kimarekani milioni 400 katika Buzwagi, imewekeza dola za kimarekani milioni 600 katika Bulyanhulu. Je, ni kwa vipi Buzwagi iwe *marginal mine* wakati uwekezaji wake unashinda uwekezaji wa Migodi ya Tulawaka na *North Mara?*

Mheshimiwa Spika, chini ya kifungu cha 47 cha Sheria ya Madini ya Mwaka 1998 (Na.5/98), pamoja na mambo mengine kinataka leseni yoyote isitolewe mpaka taarifa ya mazingira iwe imetolewa na kuruhusu mgodi kuendelea na kazi.

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri wa Nishati na Madini ameweka saini Mkataba wa Buzwagi juma la mwisho la mwezi Februari, 2007, Baraza la Mazingira nchini limetoa kibali *(Environmental Impact Assessment- EIA approval)* tarehe 11 Mei, 2007. Kwa nini Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Nazir Karamagi alisaini *MDA* ya Buzwagi na Kampuni ya *Barrick* kabla ya Baraza la Mazingira la Taifa *(NEMC)* halijatoa ruhusa?*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini niliyoitaja hapo awali imeunda Kamati ya Ushauri ya Madini *(Mining Advisory Committee).* Kabla ya Waziri kusaini mkataba wowote ni lazima apate ushauri kutoka kwenye Kamati hii. Kwa taratibu za Kiserikali, kama Kamati ikimshauri Waziri na akakataa ushauri huo, inampasa Waziri atoe sababu kwa nini anakataa ushauri. Je, Waziri alifuata ushauri wa Kamati ya Ushauri ya Madini kuhusiana na wakati mwafaka? Narudia, kuhusiana na wakati muafaka wa kusaini Mkataba huu?

Mheshimiwa Spika, inawezekana kabisa *MDA* ya Buzwagi kusainiwa Uingereza sio tatizo. Kwa mfano, mwaka 2006 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilisaini mikataba kadhaa. Ni mingapi kati ya Mikataba hii imesainiwa nje ya nchi? Nini madhara ya kisheria kwa Mkataba kusaniwa Uingereza? Je, mkataba ambao umesainiwa wa Buzwagi umeandikwa "*signed in London"* au "*signed in Dar es Salaam"*, yaani umesainiwa *London* au umesainiwa Dar es salaam? Kamati Teule ya Bunge ndio chombo pekee kitakachoweza kutoa majibu ya maswali haya. Kuhusiana na asilimia 15% ya *capital allowance on unredeemed qualifying capital expenditure.*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini amenukuliwa na kumbukumbu za majadiliano ya Bunge akisema, naomba kunukuu: "…kwa hiyo pamoja na kwamba namheshimu sana Mheshimiwa Kabwe Zitto na sote tunamheshimu, ni msomaji mzuri, lakini wakati mwingine lazima kuangalia vitu gani unasoma. Ni kwamba kipengele hiki cha sheria kililetwa hapa Bungeni mwaka 2001 kwenye Bajeti kikabadilishwa." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, katika kuandaa hoja yangu hii, ilinibidi kupitia upya kumbukumbu za majadiliano ya Bunge ili kujiridhisha na maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, maelezo ambayo nililiarifu Bunge lako Tukufu tarehe 16/7/2007 kuwa sio sahihi.

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu hizo zinaonesha kwamba, Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 *(Finance Act. No.14, 2001)* ilifanyiwa marekebisho kadhaa yakiwemo marekebisho ya sheria ya madini kifungu cha 87 ambapo kifungu kidogo cha (3) cha kifungu cha 87 kiliongezwa. Kifungu kidogo hicho kinasema; naomba kununukuu kwa Kiingereza: (3) *"The provisions of subsections (1) and (2) shall not apply to any person who, immediately before the first day of July, 2001 was not the holder of a mineral right granted under this Act."*

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 87 cha Sheria ya Madini ya Mwaka 1998 (Na.5/1998) kinazungumzia mrabaha wa madini *(remission and deferment of royalties).* Hivyo, kama Sheria ya Fedha ya Mwaka 2001 haikubadili kipenge hiki, Mheshimiwa Waziri ametoa wapi jibu aliloliambia Bunge? Suala hili linahusu haki, kinga na madaraka ya Bunge kwa mujibu wa Sheria Na. 3 ya 1988.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika hotuba ya Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, akiwasilisha Hotuba ya Bajeti mwaka 2002, tarehe13 Juni, alizungumzia kipengele hiki. Naomba kunukuu sehemu ya hotuba ya Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basili Mramba katika hotuba ya bajeti ya Kiingereza: "*Amendment to the Income Tax structure, (44) Mr. Speaker, in this area I propose to take the following measures:* (v) *I propose to reinstate*...! Naomba kurudia, *"the additional 15 percent capital allowance on unredeemed qualifying capital expenditure as set out in the Mining Act. No. 5 of 1998."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, nilipopitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2002 nimekuta sehemu ya 8 inazungumzia mabadiliko katika kodi ya mapato ya 1973 ambayo imefanyiwa marekebisho mwaka 2004. Na hata katika ukurasa wa kwanza wa sheria hii *(Arrangement of Contents),* sheria ya Madini haitajwi. Maelezo haya ya Waziri wa Fedha ya mwaka 2002 yanaonesha dhahiri utata wa kipengele hiki. Ni kwa vipi kifungu cha sheria ambacho hakijafutwa kirejeshwe? Tuchukulie kuwa maneno ya Waziri ni ya kweli? Je, kwa nini makampuni ya Madini ambayo yameingia Mkataba na Serikali kuanzia tarehe 1 Julai, 2001 hayajaanza kulipa kodi ya mapato kama Waziri alivyosema?

Mheshimiwa Spika, utata huu ambao umegubika sekta hii ya madini unaweza kufafanuliwa na Bunge lako Tukufu kupitia Kamati Teule. Kamati Teule ya Bunge ichunguze upitiaji wa mikataba hii na kuona kama kuna vitendo vyovyote vya uvunjaji wa sheria za nchi na kupotea kwa mapato ya Serikali na ufisadi.

Mheshimiwa Spika, suala hili ni suala la kitaifa. Halina hata chembe ya itikadi za kivyama. Naamini Wabunge wataamua kwa maslahi ya Taifa letu. Uundwaji wa Kamati Teule ya Bunge kuchunguza mapitio ya mikataba ya madini na mazingira ya kusainiwa

kwa mkataba mpya wa Buzwagi utatoa msaada mkubwa kwa azma ya Rais wetu, Ndugu Jakaya Mrisho Kikwete ya kuona rasilimali za madini zinafaidisha nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA**: Asante sana Mheshimiwa! Hoja hiyo imetolewa na imeungwa mkono. Lakini kwa sababu inahitaji majibu, sasa tutaendelea na utaratibu wa kuijadili ili tuweze kufikia uamuzi sahihi. Baada ya kumwita Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, ninao wachangiaji 13; labda nitaje watatu wa mwanzo…..! Acha niwataje wote ili wajiandae. Wa kwanza ni Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Maulida Komu, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Adam Malima, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir na atakayehitimisha ni Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir...! Kuna mwingine? Mheshimiwa Phares Kabuye naye ameomba. Basi kwa mpangilio nitamchomeka labda kati kati ya Mheshimiwa Manju Msambya na Mheshimiwa Mudhihir, watakuwa 14. Ni dhahiri mjadala huu utaendelea hadi jioni, kwa hiyo, tujiandae hivyo. Sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI**: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuchangia kwa niaba ya Serikali hoja ya Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto kuhusu kuundwa kwa Kamati Teule ya kuchunguza Mapitio ya Mikataba ya Madini na Mazingira ya Kusainiwa kwa Mkataba Mpya wa Madini wa Buzwagi.

Mheshimiwa Spika, mtoa hoja amejielekeza katika masuala makuu mawili ambayo anadai wakati nayaelezea, aidha sikuwa sahihi au nilidanganya. Kwanza, licha ya maelezo ambayo nilikwishayatoa kwa niaba ya Serikali juu ya kuondolewa kwa kipengele katika Sheria ya Mapato ya mwaka 1973 kuhusiana na Nyongeza ya asilimia 15 kwenye mtaji wa uwekezaji ambao haurejeshwi kwa kila mwaka *(Additional capital allowance of 15% per annum applied to the balance of unredeemed qualifying capital expenditure),* Mheshimiwa Kabwe Zitto anaendelea kusisitiza kuwa kuondolewa kwa kipengele hicho kulifanyika bila ya kupata kibali cha Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika kujaribu kuthibitisha hoja yake Mheshimiwa Kabwe Zitto amenukuu kumbukumbu za Bunge ambazo zinaonyesha marekebisho yaliyofanyika kwenye Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 *(Finance Act. No. 14 of 2001),* kwa kutaja marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 1998 kifungu cha 87 ambapo kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hicho kiliongezwa.

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako Tukufu litambue kuwa hapa Mheshimiwa Kabwe Zitto anachanganya Sheria mbili tofauti: Sheria ya Madini ya Mwaka 1998 na Sheria ya Kodi ya Mwaka 1973. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipengele kinachozungumziwa hakiko chini ya Sheria ya Madini ya mwaka 1998, bali kipo chini ya Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 1973. Ukweli kuhusu suala hili ni kwamba kipengele hiki cha Nyongeza ya asilimia 15 kwenye Mtaji wa Uwekezaji ambao haujarejeshwa kiliondolewa na Bunge kupitia Sheria ya Fedha ya 2001. Kama Mheshimiwa Zitto angesoma kwa uangalifu..! Narudia, kama Mheshimiwa Zitto angesoma kwa uangalifu *Finance Act No.14 of 2001* aliyoinukuu angebaini kuwa marekebisho ya kipengele hiki yalifanyika katika kifungu cha 16B cha Jedwali la Pili la Sheria ya Mapato ya Mwaka 1973 na siyo kifungu cha 87 cha Sheria ya Madini ya mwaka 1998 kama anavyodai Mheshimiwa Kabwe Zitto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kunukuu marekebisho kama yalivyoletwa Bungeni kwa manufaa ya Bunge lako Tukufu:

16B. *Paragraph 16 of the Second Schedule to the Principal Act is amended*:

(i) *by deleting the definitions of the words "additional capital allowance" and qualifying capital expenditure" which appear in sub-paragraph (1) of paragraph 16.*

*(ii) by deleting the definitions of word "expenditure" and substituting for it the following definition:"expenditure" means the sum of prospecting capital expenditure and development capital expenditure incurred in the United Republic of Tanzania by any person carrying on mining operations. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana ya mabadiliko haya ni kwamba kifungu cha 18 (1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 1973 kinachoweka masharti ya kipengele cha nyongeza ya asilimia 15% kwenye mtaji wa uwekezaji ambao haujarejeshwa kiliondolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya Bunge kupitisha marekebisho hayo, matokeo yake yalikuwa kwamba Bunge liliafiki kuondolewa kwa 15% ya *additional capital allowance on unredeemed qualifying capital expenditure* bila ya kujali mikataba ambayo baadhi ya makampuni ya madini yalikuwa yameingia na Serikali kwa mujibu wa kifungu cha 10 cha Sheria ya Madini ya mwaka 1998 kabla ya mabadiliko haya.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kwamba mikataba ambayo Serikali iliingia na kampuni za madini kabla ya mabadiliko ya sheria hiyo ilikuwa inaifunga *(binding)* Serikali kutofanya mabadiliko ya sheria ambayo yataondoa vivutio vya kodi vilivyokuwepo wakati mkataba unatiwa saini, Serikali ilileta mapendekezo kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2002 *(The Finance Act, 2002)* ambayo yalipitishwa na Bunge ili kurekebisha kasoro hiyo.

Mheshimiwa Spika, maana ya mabadiliko hayo ni kwamba *15% additional capital allowance on unredeemed qualifying capital expenditure* ilirudishwa kwa makampuni ya madini yaliyoingia mkataba na Serikali kabla ya tarehe 1 Julai, 2001. Ndio sababu migodi iliyokuwa na mkataba na Serikali kabla ya tarehe 1 Julai, 2001

ilieendelea kuwa na kivutio *15% additional capital allowance on unredeemed qualifying capital expenditure* hata baada ya kuondolewa kwa fungu hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuthibitisha kauli yangu, nimewasilisha kwako nakala ya *Hansard* ya tarehe 14 Juni, 2001 na nakala ya Ibara ya 16 ya *Finance Act No.14 of 2001* ilivyowasilishwa Bungeni ili igawiwe kwa Mtoa hoja na Waheshimiwa Wabunge wengine wanaotaka kujiridhisha na ukweli huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali makini kama ilivyo Serikali yetu, haidanganyi. Uthibitisho huu ni kielelezo tosha kuwa mtoa hoja ndiye aliyedanganya Bunge na Watanzania waliomsikiliza kwa….! Nitarudia, Uthibitisho huu ni kielelezo tosha kuwa mtoa hoja ndiye aliyedanganya Bunge na Watanzania waliomsikiliza kwa kutokuwa makini na kauli yake Bungeni. Nataka kuchukua nafsi hii kuwasilisha kwako ile *Hansard* niliyoizungumzia ambayo mwaka 2002 iliondoa kipengele hicho. *(Makofi)*

*(Hapa Hansard husika na viambatisho vyake vilikabidhiwa kwa Spika)*

Mheshimiwa Spika, pili , Mheshimiwa Zitto anahoji kusainiwa kwa mkataba mpya wa Madini wa mgodi wa Buzwagi kati ya Serikali na kampuni ya *Barrick* na uhalali wa Mkataba huo kusainiwa mjini *London,* Uingereza. Vilevile, Mheshimiwa Zitto anahoji kwa nini Mkataba huo umesainiwa wakati Serikali bado inafanya durusu *(review)* ya mikataba ya Madini kufuatia maagizo ya Rais. Kuhusu suala la Mkataba kusainiwa Uingereza, kama nilivyolielezea Bunge lako Tukufu wakati nahitimisha hoja ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2007/08, mkataba huo uliandaliwa Tanzania na wataalamu wetu na ukapitia taratibu zote zinazopaswa kufuatwa ikiwa ni pamoja na kuidhinishwa na Kamati ya Ushauri ya Madini *(Mining Advisory Committee)* na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.Katika viambatisho nilivyokupatia sasa hivi, vilevile nimeambatisha na kauli yangu hii. Uamuzi wa kuingiza mradi wa Buzwagi kwenye miradi ya *Barrick Gold Corporation* ambayo ni kampuni mama, ulihitajika kufanyika kabla ya Machi, 2007, vinginevyo fursa ya uwekezaji katika mradi huu ingepotea. Kwa kuwa maandalizi yote ya kusaini mkataba yalikamilika nikiwa ziara ndefu nchi za nje, niliona si busara kuhatarisha uwekezaji wa mradi huu jambo ambalo lingeathiri maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kutoa faida inayotarajiwa kutokana na Mgodi wa Buzwagi katika kipindi cha uhai wake ambayo kama usingesainiwa na *Barrick* wasiwekeze kwenye mradi huu ingepotea:-

(i) Mrabaha na kodi nyingine zinatarajiwa kufikia kiasi cha *USD*198.9 milioni.

(ii) *Pay As You Earn* kwa wafanyakazi inatarajiwa kufikia *USD*50.3 milioni.

(iii) Ujenzi wa laini ya umeme na matumizi ya umeme ya mgodi na maeneo yanayozunguka mgodi yanategemea kutumia *USD*30 milioni.

(iv) Kununua huduma mbalimbali za wakati wa kujenga miundombinu mingine kwenda mgodini, ujenzi wa mitambo na wakati wa uzalishaji ambao unatarajiwa kugharimu takriban *USD*568.4 milioni.

(v) Jumla ya mapato yote yatakayoingia kwenye uchumi wa Taifa katika kipindi cha uhai wa mgodi yanatarajiwa kufikia takriban *USD*818.3 milioni.

(vi) Mgodi unatarajia kutoa ajira katika fani mbalimbali kwa jumla ya watu 696 watakaopata ajira ya kudumu. Kati yao, 630 au asimilia 91 watakuwa Watanzania ikiwa ni pamoja na maafisa waandamizi.

(vii) Mgodi utaongeza mapato ya taifa ya fedha za kigeni kutokana na mauzo ya madini nje.

(viii) Mgodi utaendeleza miundombinu ya kiuchumi na kijamii, hasa huduma za jamii kama vile shule na zahanati katika maeneo yanayozunguka mgodi.

(ix) Kufunguliwa kwa mgodi huo kutafungua fursa nyingine za kiuchumi katika maeneo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kabwe Zitto anauliza kwenye mkataba huo, je, kipengele kimekuwa *signed in London* ama *signed* in Dar es Salaam? Hali ya maendeleo tuliyoyafikia dunia ya kileo, si muhuimu tena kwenye mikataba kuweka kipengele cha kubainisha mkataba kuweka kipengele cha kubainisha mkataba umewekwa saini eneo gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *Format* ya mkataba wa madini wa Buzwagi hauna kipengele anachokiuliza Mheshimiwa Kabwe Zitto. Hiki si kitu cha ajabu kwa mikataba ya siku hizi ambapo mkataba unaweza kusainiwa na pande zaidi ya mbili zikiwa nchi tofauti. Mkataba unaweza ukasainiwa upande mmoja na ukatumwa kusainiwa na upande mwingine, nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu muhimu katika mkataba ni kuonyesha k ni sheria ya nchi gani itaongoza kwenye mkataba. Mkataba wa Mgodi wa Buzwagi unataja kuwa sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo itaongoza mkataba huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kabwe Zitto anahoji kama kabla ya kusaini Mkataba wa Buzwagi nilifuata Sheria inayonitaka kwanza kupata ushauri wa Kamati ya Ushauri ya Madini.

Kama nilivyokwishasema mkataba ulipitia taratibu zote zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kupata baraka za Kamati ya Ushauri ya Madini. Kivuli cha idhini ya Kamati hiyo nimekwishawasilisha kwako kama kielelezo cha kuthibitisha kauli yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kabwe Zitto anazungumza kwamba maagizo ya Rais yalikiukwa, kauli anayoitoa bila ya kutafakari maagizo hayo yalikuwa ya aina gani. Mheshimiwa Rais aliagiza mikataba yote ya madini kufanyiwa mapitio ili kubaini maeneo yanayoweza kurekebishwa kwa faida ya pande zote mbili – faida ya nchi na faida kwa Mwekezaji *(win-win situation).*

Kamati iliundwa kwa sababu hiyo na baada ya kukamilisha kazi iliyopewa, iliwasilisha mapendekezo yake Serikalini tarehe 14 Septemba, 2006. Baadhi ya mapendekezo ya Kamati hiyo yalitumika katika majadiliano na makampuni ya madini yenye mikataba ya zamani. Mafanikio ya majadiliano hayo niliyataja kwenye hotuba yangu wakati nawasilisha bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini ya mwaka 2007/08 kuwa ni:-

(i) Kuondoa nyongeza ya asilimia 15 kwenye mtaji wa uwekezaji ambao haujarejeshwa *(15% additional capital allowance on unredeemed qualifying capital expenditure)*. Hatua hii itawezesha kampuni hizi kukomboa gharama zao za uwekezaji mapema na hivyo kuweza kulipa kodi ya mapato *(corporation tax).*

Kwa hili, ningependa kumsahihisha Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto kwamba kuondolewa kipengele hicho siyo *automatic* kwamba kampuni inaanza kulipa kodi, isipokuwa inaharakisha muda wa kampuni kulipa kodi.

(ii) Kulipa kiasi cha Dola za Marekani 200,000 kwa mwaka kwa Halmashauri zinazohusika na migodi hiyo. Kampuni ya *Barrick Gold Corporation* imekubali na imeanza kulipa Dola za Marekani milioni 7 kila mwaka kama malipo ya awali ya kodi ya mapato ya kampuni hadi migodi yake itakapoanza kulipa kodi stahili.

(iii) Kampuni ya *Resolute (Tanzania) Limited* imeondoa kipengele kwenye mkataba wake kilichokuwa kinairuhusu kutokulipa kodi ya mapato kwa wafanyakazi wake wa kigeni. Kuondolewa kwa kipengele hiki kutailazimu kampuni hii kulipa takriban Dola za Marekani milioni 2.2 kila mwaka kama malipo ya kodi ya mapato. Katika mwaka 2006/07 kampuni hiyo imelipa Dola za Marekani milioni 2.3.

(iv) Kampuni ya *Anglo Gold Ashanti* inayomiliki mgodi wa Geita imekubali kulipa kiasi cha Dola za Marekani 200,000 kwa mwaka kwa Halmashauri ya Wilaya ya Geita. Aidha, majadiliano katika maeneo mengine ya mkataba wake yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, hivyo, si kweli kuwa zoezi la kudurusu mikataba ya madini bado linaendelea. Nilisema kuwa mkataba mpya kuhusu Buzwagi hauna upungufu uliokuwemo kwenye mikataba ya zamani – ikiwa na maana kuwa kwa kutumia ushauri wa Kamati niliyoitaja hapo juu, mkataba wa Buzwagi umeboreshwa kwa maslahi ya Taifa ukilinganisha na mikataba ya zamani. Naomba ninukuu baadhi ya vipengele vilivyoboreshwa:-

(a) *Depreciation* ya gharama ya uwekezaji ni asilimia 80 mwaka wa kwanza, na baadaye asilimia 50 miaka inayofuata. Katika Mikataba ya awali *depreciation allowance* ni asilimia 100 mwaka wa kwanza.

(b) *Withholding taxes* zimeongezwa kiwango kama ifuatavyo:-

(i) Technical services kodi ya zuio itakuwa asilimia 5 badala ya asilimia 3 zilizoko kwenye Mikataba *(MDAs)* ya zamani na hii ni kwa kila malipo yanayozidi asilimia 2 ya gharama za uzalishaji.

(ii) *Service fees* kwa ajili ya gharama za utawala itakuwa asilimia 15 ikilinganishwa na asilimia 3 za Mikataba *(MDAs)* ya awali na hii ni kwa gharama ya uzalishaji. *(Makofi)*

(iii) Kuna masharti ambayo hayakuwemo kuhusu kununua bidhaa na huduma mbalimbali hapa nchini.

(iv) Kuna masharti kuhusu kuchangia mfuko wa uwezeshaji *(empowerment fund)* ambao haukuwepo katika mikataba ya zamani, kupitia Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, *USD* 125,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, utaona kuwa kuna vipengele vilivyowekwa kwenye mkataba huu ambavyo utekelezaji wake utafanyika baada ya kuleta Bungeni mapendekezo ya kurebisha vifungu husika kwenye sheria inayohusu mfumo wa kodi katika sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kabwe Zitto, anasisitiza kuwa zoezi la kudurusu mikataba bado linaendelea. Mtoa hoja labda anachanganya tena zoezi la kudurusu mikataba na zoezi linaloendelea na kudurusu Sheria ya Madini ya Mwaka 1998 na Sheria zinahusu mfumo wa kodi katika sekta ya madini kitu ambacho ni kipana zaidi na kinawahusu wadau wote yaani, wawekezaji wakubwa, wawekezaji wadogo na wote wanaojihusisha na utafiti katika sekta ya madini. Akielewa hili mtoa hoja atabaini kuwa maagizo ya Rais yalitekelezwa kikamilifu na matokeo yake yamekwishaanza kujitokeza kama faida nilizozieleza hapo juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kabwe Zitto anahoji kama Buzwagi ni mradi *(project)* au ni mgodi *(mine)*. Nafikiri hili ni suala dogo ambalo naamini ni la uelewa tu. Hadi sasa mradi wa Buzwagi haujafikia hadhi ya kuitwa mgodi.

Kama ilivyo miradi yote, Buzwagi utapata hadhi ya kuitwa mgodi baada ya Waziri wa Nishati na Madini kutoa leseni ya uchimbaji, ujenzi wa mgodi kukamilika na shughuli za uchimbaji kuanza. Kwa hiyo, nazidi kusisitiza kwamba Buzwagi ni mradi. Kama tulivyo hapa kwenye Bunge Tukufu, wakati ujenzi ulipokuwa ukiendelea tusingeliweza kuliita Bunge kama jengo, lilikuwa linaitwa mradi mpaka lilipokamilika tukaingia ndiyo likaitwa jengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mgodi wa Buzwadi kuwa ni *marginal mine.* Nilisema kwamba katika tathmini ya migodi, Mgodi wa Buzwagi ni *marginal mine* ambao uhai wake si wa muda mrefu na kwamba bila ya kutumia fedha fursa iliyokuwepo hususan bei kubwa ya dhahabu uwekezaji wake usingekuwa wa faida.

Wizara ya Nishati na Madini ilifanya uchambuzi wa taarifa ya uwekezaji katika Mgodi wa Buzwagi na kuonekana kuwa mgodi huo ni *marginal project* na ukianza kuendelezwa wakati huu ambapo bei ya dhahabu ni kubwa wastani wa zaidi ya dola za Marekani 600 kwa wakia, ndiyo utatoa *marginal profit* na kuwezesha mwekezaji kuendeleza mradi wa Buzwagi hadi kufikia hadhi ya kuwa mgodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kabwe anasema kuwa mgodi wa Buzwagi hauwezi kuitwa *marginal mine* kwa kigezo kuwa utashika nafasi ya pili kwa migodi inayomilikiwa na kampuni ya *Barrick* kwa kulinganisha moja kwa moja na gharama za uwekezaji kati ya Mgodi wa Bulyanhulu uliofanyika miaka ya tisini na mgodi wa Buzwagi unaotarajiwa kujengwa mwaka ujao 2008.

Mheshimiwa Spika, mtoa hoja inaelekea anazungumzia suala la utaalamu wa fedha ambalo inaonyesha wazi hana ujuzi nalo. Hata hivyo, mtu hahitaji kuwa mtaalamu ili kuelewa kuwa kama mwekezaji alitumia thamani ya dola za Kimarekani milioni 600 kujenga mgodi wa Bulyanhulu miaka kumi iliyopita, akitaka kujenga mgodi kama huo kwa sasa thamani yake itakuwa kubwa maradufu. Labda kwa manufaa ya Bunge lako Tukufu, naomba nitoe ufafanuzi wa ziada ili kuonyesha kuwa gharama za uwekezaji siyo kigezo pekee cha kupima ubora wa mgodi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, vigezo vingine vinavyotumika kujua ubora wa mgodi ni pamoja na mashapo yaliyopo na kiwango cha upatikanaji wa dhahabu kwa tani ya miamba (*ore grade per tonne)*. Kiwango cha upatikanaji wa dhahabu katika mgodi wa Bulyanhulu ni wastani wa gramu 11 za dhahabu kwa tani ikilinganishwa na Buzwagi ambapo ni gramu 1.8 za dhahabu kwa tani. Mashapo yaliyopo Bulyanhulu ni kiasi cha wakia milioni 12 inayoweza kuchimbwa kwa miaka karibu 25 wakati Buzwagi ni wakia milioni 2.2 inayoweza kuchimbwa kwa miaka 10. Kutathiminiwa Mgodi wa Buzwagi kama marginal mine ni suala la kitaalamu lenye takwimu za wazi ambalo halipingiki wala halipindishwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuhuma kwamba sheria imevunjwa kwa kusaini Mkataba kabla ya Baraza la Mazingira kutoa kibali. Mheshimiwa Kabwe Zitto amenukuu kifungu cha 47 cha Sheria ya madini ya mwaka 1998 kinachotaka leseni yeyote ya uchimbaji madini isitolewe mpaka taarifa ya mazingira iwe imetolewa.

Mheshimiwa Spika, Kabwe Zitto anachanganya tena vitu viwili tofauti, yaani Mkataba wa Madini na Leseni ya Madini. Mkataba wa Madini kati ya Serikali na kampuni za madini unaingiwa chini ya kifungu cha 10 cha Sheria ya Madini ya mwaka 1998 na hicho kitu cha kwanza kinachoanzishwa mchakato wa uwekezaji. Hivyo, tathimini ya mazingira *(environmental impact assessment study)* inafanywa baada ya mwekezaji kuwa na mkataba.

Mwekezaji anaweza kuomba leseni ya uchimbaji wa madini wakati wowote lakini hawezi kuipata mpaka awe na kibali cha Baraza la Mazingira la Taifa *(NEMC).*

Kwa maneno mengine kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 1998, maombi ya leseni ya uchimbaji wa madini *(mining license)* lazima yaambatane pamoja na mambo mengine na tathimini ya mazingira kuhusu mradi huo *(environment impact Assessment study).* Mpaka sasa leseni ya uchimbaji kwa mradi wa Buzwagi bado haijatolewa. Kwa kupata kibali cha Bazara la Mazingira la Taifa *(NEMC)* mwekezaji atakuwa ametimiza sharti mojawapo la kupata leseni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kumshauri Mheshimiwa Kabwe Zitto ajielimishe zaidi juu ya sheria zinazosimamia sekta ya madini hapa nchini.

Vilevile namshauri Mheshimiwa Kabwe Zitto kujiepusha na hulka ya kutoa kauli nzito ambazo hazikufanyiwa utafiti wa kutosha kama hili analodai kuwa Serikali imevunja sheria za nchi na kulidanganya Bunge wakati ni yeye mwenyewe hajajielimisha vya kutosha kuhusu sheria anayoizungumzia kwamba imevunjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtoa hoja amedai kuwa suala analolizungumzia ni la kitaifa na halina hata chembe chembe za itikadi za vyama. Pamoja na kuwa hoja alizozitoa hazina ushahidi wowote, tayari hoja hizo zimekwishadakwa na kubebewa bango na Mwenyekiti wa Chama chake cha CHADEMA na wamezigeuza kuwa propaganda ya kisiasa kupitia vyombo vya habari. Labda angalizo alilolitoa Mheshimiwa Kabwe Zitto, analilenga kwa Chama chake mwenyewe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuna msemo wa Kingereza usemao *no research no right to speak,* bila utafiti huna haki ya kuzungumza. Hivyo vilevile Chama makini kinahitaji kufanya utafiti kabla ya kujihusisha na mambo ya kuzua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya Mheshimiwa Kabwe Zitto, imeonyesha upungufu mkubwa wa tafsiri ya sheria anazozinukuu na vifungu anavyovilenga ili kuthibitisha kuwa Serikali imelidanganya Bunge.

Ni dhahiri hoja yake imejengwa katika mazingira ya uzushi yenye malengo makuu mawili. Kwanza, kuchonganisha Bunge lako Tukufu na Serikali na pili kuwapotosha wananchi juu ya sheria zinazotungwa na Bunge lako Tukufu kwa nia ya kujitafutia umaarufu.

Nataka kurudia, ni dhahiri hoja yake imejengwa kwa mazingira ya uzushi yenye malengo makuu mawili, kwanza, kuchonganisha Bunge lako Tukufu na Serikali na pili kuwapotosha wananchi juu ya sheria zinazotungwa na Bunge lako Tukufu kwa nia ya kujitafutia umaarufu usiokuwa na msingi *(cheap popularity). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtoa hoja analiomba Bunge lako Tukufu kuunda Kamati Teule ya Bunge hili, Kamati imfanyie kazi ya kuhalalisha mambo ya kuzua au kumsaidia kumfafanulia sheria ambazo yeye mwenyewe kashindwa kuzielewa. Hii si kazi ambayo Bunge hili linaweza kutumia fedha za walipa kodi kuifanya. Tabia ya namna hii ikiruhusiwa kuendelea inaweza kulipunguzia Bunge lako Tukufu heshima na hadhi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nijielekeze yaliyojitokeza tarehe 16 Julai, 2007 mara baada ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kupitishwa na Bunge. Mheshimiwa Kabwe Zitto alisimama na kutoa tuhuma nzito kwangu kama Waziri wa Nishati na Madini, kuhusiana na mkataba mpya wa Buzwagi.

Akinukuliwa na *Hansard* ya tarehe 16/07/2007, ambayo mwenyewe ameinukuu bila kuikamilisha, Mheshimiwa Kabwe Zitto alisema; nanukuu: "...kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri kuhusiana na mkataba mpya wa mgodi wa Buzwagi ambao Mheshimiwa Waziri ameeleza maelezo ambayo siyo sahihi, amedanganya na ameeleza vitu ambavyo kwa kweli sivyo ambavyo vipo katika mkataba ambao ameusaini..." Mwisho wa kunukuu".

Kutokana na tuhuma hizo, Mheshimiwa Zitto kwa kutumia Kanuni ya 104 (1) ya Kanuni za Bunge alitoa taarifa rasmi ya mdomo ya kusudio la kuleta hoja ya kuunda Kamati Teule kuchunguza mkataba mpya wa Madini wa Buzwagi. Leo ametoa hoja aliyoitolea taarifa, lakini mbali ya kujikanganya kwenye sheria alizodai zimevunjwa, hajaonyesha wazi pasipotiliwa mashaka wapi nililidanganya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuhuma alizozitoa Mheshimiwa Kabwe Zitto kwangu kama Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Nishati na Madini na kudakwa na vyombo vya habari ameniathiri mimi binafsi kwa kunichafulia jina langu bila sababu za msingi kwa kutoa taarifa za uzushi tena wa hatari.

Nina hakika wewe mwenyewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu mmeshuhudia jinsi magazeti mbalimbali yalivyokuwa yakitoa vichwa vya habari vyenye kutoa lugha za kejeli kwangu kutokana na tuhuma Mheshimiwa Kabwe Zitto alizozitoa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa vielelezo na maelezo ya Serikali niliyoyatoa, sasa naomba kupitia kwako kuliomba Bunge lako Tukufu vilevile liangalie vielelezo alivyovitoa mtoa hoja kama vipo ili liweze kupima na kuamua ni nani mwongo; ni nani aliyelidanganya Bunge, mimi au Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, ni dhahiri tuna kazi kubwa hapa ya kufanya ili tufikie haki. Sasa kwa mpangilio nitamwita mchangiaji, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa halafu atafutiwa na Mheshimiwa Ruth Msafiri na wakati huo huo Mheshimiwa Maulidah Anna Komu ajiandae.

**MHE. KHALIFA S. KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fura hii ili na mimi nichangie machache katika hoja hii ambayo ipo mbele ya Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Spika, na mimi niungane na wenzangu kwanza kwa kukupa pole sana wewe binafsi, familia ya marehemu mzee Fundikira na wananchi wote wa Tanzania kwa kuondokewa na mzee wetu ambaye sote tuliomjua tuliona busara zake na mchango wake.

Aidha, nitumie fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Gando pia kumpa pole Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa kifo cha mzee wake na nampa pole kwa sababu siku mbili tu kabla yake tulikuwa na Mheshimiwa John Pombe Magufuli, akaniambia hali ya mzee wake, kumbe alikuwa anabashiri kifo cha karibu cha mzee huyu. Mwenyezi Mungu awape malipo yanayostahili watu hawa kwa mujibu wa madi zao.

Mheshimiwa Spika, hoja iliyopo mbele yetu ninavyoitazama ni ndogo sana, udogo wake ni kuwa inazungumziwa suala la kuundwa kwa Tume teule ya Bunge. Sasa udogo wake ama kukubali au kukataa. Mwisho, katika maneno ya mwisho ya Mheshimiwa Waziri hapa ninayemheshimu sana amesema maneno kuwa vielelezo alivyovitoa Mheshimiwa mtoa hoja kama vipo na vielelezo alivyovitoa yeye ambavyo naamini vipo vinahitaji kutazamwa. Chombo cha kutazama vielelezo hivyo na kuthibitisha nani mwongo ni hiyo Kamati Teule ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imezuka shutuma kuwa Mheshimiwa Rais amesema kwa nia nzuri tu suala la kupitiwa mikataba. Ni kweli Mheshimiwa Rais amesema hivi na mimi naamini amesema kwa nia safi. Sasa sisi hatukulazimisha kama Wabunge kuwa tuione mikataba. Lakini kama kumbukumbu ni sahihi ni Bunge hili hili na Wabunge hawa hawa katika mijadala mbalimbali wamekuwa wakilizungumzia jambo hilo labda wayafute maneno yao hayo leo.

Wamezungumza sana kuhusu mikataba ya madini. Kama tutakuwa tunakwenda katika mwenendo huo hiyo ni hatari mno. Kwa sababu ni sisi Wabunge, Bunge hili hili tumesema mikataba ya madini ina matatizo tunahitaji tuione ina mambo mengi. Sasa kama leo imetolewa hoja ya kuundwa Tume ya Bunge kutazama *issue* moja tu ya mkataba mmoja tu ilishakuwa tatizo kubwa, nasikitika sana. *(Makofi)*

Tumeambiwa hapa, mfano mzuri kampuni ya *Barrick* kuwa inachingia shilingi bilioni 7 au dola milioni 7. Lakini maneno hayo tunaambiwa leo baada ya kauli ya Mheshimiwa Rais ya kupitiwa mikataba. Hivi kwa nini haikuwepo mwanzo? Kwa nini Kampuni ya *Barrick?* Hizi nyingine? Sasa yote hayo ni mambo ambayo Wabunge kama wawakilishi wa wananchi wanapaswa kuyajua.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hilo wewe mwenyewe ulisema hapa kuwa mitandao tusiitumie sana na taarifa za mitandao mingine si sahihi sana. *Ruling* yako naiheshimu

kweli kweli kwa sababu *ruling* yako ni kubwa, mara nyingine hata kuliko kanuni zetu za Bunge kwa mtu anayeelewa taratibu za hapa. Lakini *DRC* ambayo ni taifa lililotulia karibuni tu wamechukua miezi minne kupitia mikataba yao. Sasa sisi ni muda mrefu, ni miezi 18 kimya, inakuja taarifa tena ndogo tu kama hiyo *Barrick* inachangia, makampuni mengine yatakayochangia dola 250,000 sijui dola 200,000 kwa Halmashauri kwa kifupi namna hii.

Sasa nije kwenye hoja ya Mheshimiwa Mbunge, Bunge hili katika kipindi kilichopita liliwahukumu Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano, wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)* kwa kosa la kutia sahihi taarifa ya Kamati ya *PAC* kantini. Ndani ya Bunge hili baadhi ya Wabunge wakaadhibiwa na Bunge kwa kosa hilo. Sasa mimi nashtuka sana inaposemwa kuwa kumbe jambo zito unaweza ukalifanya vyovyote kwa sababu unataka hivyo. Je, tuliwaadhibu nini wale kama lile lilikuwa si kosa kwani kantini si mahali, si Tanzania hii hii? Lakini tukawaadhibu wakakosa Ubunge kwa wale wanaokumbuka. *(Makofi)*

Sasa tunapoambiwa tu ni jambo la kawaida tu kwenda kusainiwa nje ya nchi jambo zito kama hili linalohusu maslahi ya wananchi na halafu inajengwa hoja ya kuwa hapana haja ya kujua kinachofanyika ndiyo kinachosemwa katika hoja hii kuundwa Kamati maana yake ni kuwa kijulikane kilichofanyika, kwa nini iwe nje isiwe ndani?

Sasa mimi napata tabu kidogo kuona kuwa tunayajadili mambo yanayohusu Watanzania, tena mara nyingine nasikitika kidogo kwa sababu lugha ambazo zimetumika si nzuri hata kidogo! Hatuwezi kupingana na kanuni tukaelezana na nini kwa sababu si utaratibu na tunaheshimiana sana humu ndani. Hii kanuni sisi wengine tunaijua vizuri kweli kweli. Lakini si vizuri anasimama mtu mzima unampiga kanuni, kaa kitako lugha si nzuri.

Lugha iliyokuwa ikisemwa hapa kama lugha iliyozungumzwa katika hoja ya mtoa hoja hapo mwanzo tarehe 16 ilikuwa ina maneno ya kukera na hii ya leo waliosikia ni maneno ya kukera sana. Sasa katika busara ya kawaida, katika watu tulioendelea kama sisi na tena bahati nzuri tunajisifu kuwa tumesoma sana tuna sheria nyingi, tusitukanane kabisa kwa sababu wananchi wetu wanasikia na hawapendi vitu hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia kwenye hoja yangu ya msingi kwamba ipo haja ya kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge na naunga mkono kwa asilimia kubwa kabisa asilimia mia moja na zaidi kuwa Bunge hili Tukufu kwa kuangalia hali nzima ilivyokwenda na utata huu, lazima iundwe Kamati Teule ya Bunge. Kama hoja ni kutumia fedha za wananchi, fedha za wananchi zimetumiwa katika majadiliano madogo tu ya hapa. Ofisi yako imeunda Kamati Teule na zimetumika fedha, Serikali haikuwa na maneno, je, jambo hili linalohusu maslahi ya wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nipate nafasi ya kuchangia machache katika hoja iliyoko mbele yetu. Hoja

iliyowasilishwa asubuhi hii na Mheshimiwa Kabwe ni ya kuona uwezekano wa kuunda Kamati Teule ya Bunge kwa mujibu wa kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2004, Ibara ya 104 (2).

Mheshimiwa Spika, naomba nitamke moja kwa moja kwamba hakuna haja ya kuunda Kamati hii. Nasema hivyo kwa sababu mto hoja alifuata taratibu zote ambazo alitakiwa kuzifuata kwa mujibu wa kanuni. Asubuhi ya leo amepata nafasi ya ziada, ametoa maelezo yake yeye mwenyewe, alikwishawasilisha vielelezo vyake mapema tu na vilevile tumepata nafasi ya kumsikiliza mjibu hoja na pia ametoa vielelezo vyake mbele ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Bunge letu limekuwa na kawaida ya kupokea hoja na kuzijadili kwa kupima nguvu ya hoja yenyewe. Kwa mujibu wa hoja iliyotolewa na majibu tuliyokwisha kuyapata nimeridhika kabisa kwamba mjibu hoja ameweza kujibu hoja zote vizuri. Hali ambayo inaondoa madhumuni ya kuwa na Kamati Teule kama ambavyo mtoa hoja alipendekeza.

Yapo mambo mengine ambayo ni madogo madogo ambayo kimsingi wala hayakutakiwa hata kuonekana. Kwa mfano, anaposema mkataba ulisainiwa *London* au Dar es Salaam, nashindwa kujua kwamba aliyeusaini ni nani? Kwa sababu sijui Mheshimiwa Waziri akishakuwa amekula kiapo ni wakati gani anapoacha kuwa Waziri, anapokuwa yupo ndani ya nchi, ama nje ya nchi? Ni wakati gani ambapo hatumii madaraka yake ipasavyo? *(Makofi)*

Kwa hali hiyo, mimi sikuona mahali ambapo Mheshimiwa Waziri kwa kusaini mkataba huu alipokuwa nje nchi alifanya makosa. Alifanya hivyo kwa kutumia mamlaka aliyopewa na mamlaka iliyomteua. Mamlaka hiyo haijamlalamikia, imeridhika kwa kazi aliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, tumekwishafanya mikutano sisi wenyewe Wabunge, sielewi labda Mheshimiwa Kabwe lakini sisi tumekwishafanya mikutano, tunakaa Dar es Salaam tuko ndani ya ukumbi wa Mkutano kwa kutumia mtandao, tunafanya mkutano na wenzetu ambao wako katika nchi zingine, wako Afrika ya Kusini, wako Uingereza, wako *New York* tunaongea nao tukiwa katika kumbi ambazo zimeandaliwa.

**MBUNGE FULANI:** *Visual Conference.*

Wamenipa jina rasmi basi nilitamke sikuwa napenda kulisema, inaitwa *Visual Conference.* Mnaonana, mnazungumza, mnajibizana na mnaweza kuzungumza na kufikia muafaka wa jambo lolote na yale mnayoyafikia yanachukuliwa kwamba ni maazimio rasmi ambayo mmeyafikia. Hamkuonana uso kwa uso lakini kwa kutumia vyombo mmeweza kuonana. *(Makofi)*

Sasa ikiwa katika mkataba huu hili jambo linashangaza labda tu niunge mkono kwamba maneno ya Waziri kwamba mtoa hoja ajielimishe zaidi pamoja na mitandao ya kisasa kwa umri bado anaweza kufanya hivyo na akafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna maneno mengine ambapo mimi nadhani tumepata darasa kidogo kwa Mheshimiwa Waziri kwa kutuelimisha tofauti ya mkataba na tofauti ya leseni, ni wakati ambapo mkataba unasainiwa, wakati gani tathmini ya mazingira inafanywa. Hakuna tathmini ya mazingira inaweza ikafanywa wakati huyu mwenye kuingia mkataba hajaonyesha nia na hajaingia makubaliano. Sasa baraza litakwenda kutazama nini kati ya nani na nani maana mimi sijapata kusikia ndoa inaandaliwa kati ya watu wawili ambao hawajakubaliana. Kwa hiyo, haiwezekani Baraza likaenda kufanya tathmini ya mazingira wakati Serikali haijakubaliana na yule mwenye kutaka kuingia mkataba ule. Katika hili ndicho kitu kilichofanyika. Kwa hali hiyo, mimi sijaona tunaiunda Kamati teule kwenda kuchunguza nini na kitu gani ambacho hasa ni kigumu katika hili.

Lakini kinachonikera zaidi, nataka nijirejeshe kwenye *hansard,* kuna mazingira ambayo yameendelea kujengeka kwa namna ambavyo inatisha. Naomba ninukuu *hansard* wakati mtoa hoja anaposema: "Mheshimiwa Spika, kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri kuhusiana na mkataba mpya wa Mgodi wa Buzwagi ambao Mheshimiwa Waziri ameeleza maelezo ambayo siyo sahihi, amedanganya na ameeleza vitu ambavyo kwa kweli sivyo ambavyo viko katika mkataba ambao ameusaini. Naomba kutoa taarifa rasmi ya mdomo kwamba nakusudia kuleta hoja ya kuunda Kamati Teule kuchunguza mkataba mpya wa madini ambao Waziri wa Nishati na Madini ameusaini. Napenda nisisitize pale ambao ameusaini bila kuzingatia maagizo ya Rais ya kupitia mikataba ya madini aliyoitoa mbele ya Bunge lako Tukufu tarehe 30 Desemba, 2005."

Mheshimiwa Spika, mimi naona hapa jina la Rais limetumika tu labda kuvuta hisia kwamba kuna hoja hapa ya msingi. Lakini halikutumika kueleza kwamba hoja yenyewe ni hoja gani na mjibu hoja ameeleza vizuri. Kwa hali hiyo mimi nisingelipenda tabia inayojengeka ya kupenda kutumia jina la viongozi wakuu kuonyesha kwamba hili jambo ni zito wakati uzito wenyewe haupo. *(Makofi)*

Lakini vilevile inanikera kuona kwamba ndani ya chombo hiki kitukufu, ndani ya ukumbi huu mtukufu, tunaanza kujengeana mazingira ya kuwajengea wenzetu kutokuaminiwa.

Kuwajengea wenzetu hisia za kuonyesha kwamba wanadanganya. Inasikitisha kweli kweli kuona kwamba kiongozi aliyeaminiwa na wananchi akaaminiwa na kiongozi wa nchi akapewa mamlaka makubwa ya kusimama, akawa miongoni mwa watendaji wakuu wa Serikali anaweza kuelezwa kwamba amedanganya.

Hiki ni kitu ambacho hakika mtoa hoja anaposema kwamba haizui hisia za kisiasa. Mimi nakataa kwamba anayetaka atumie ukumbi huu kuonyesha kwamba sasa yeye ana hisia zake za kisiasa na anataka kuzijenga ndani ya ukumbi huu kwa kudhalilisha watendaji wazuri walioteuliwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu hiki si kitu kizuri. Wote tunamfahamu vizuri Mheshimiwa Nadhir Karamagi, ni kipindi chake cha kwanza kuwa Bungeni, amefanya

kazi zake kwa uaminifu na uadilifu na hata mabadiliko ya Mawaziri yalipokuja bado aliendelea kuwa ndani ya Serikali.

Amefanya kazi yake ambayo ni nzuri, na Wizara aliyoshika tunajua ilivyo nzito na nyeti. Inashikilia nishati na madini ambayo ni maeneo ambayo ni nyeti katika Taifa letu na sisi tunapenda kuona kazi hii inafanyika vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo, mimi naona kabisa kwamba maelezao haya ya mtoa hoja yamekusudia kumdhalilisha mjibu hoja ambaye ni Mheshimiwa Waziri na nikisoma Kanuni ya 50, Kanuni Ndogo ya 8(a) na (d) ambayo inasema ni marufuku kwa mtu yoyote kutumia lugha ya kuudhi, vilevile kujiingiza katika mambo ya kuwasema wenzake au zaidi ni kutaka kuleta malumbano ya kisiasa ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa imezoeleka kuwa ni tabia Mheshimiwa Mbunge ananyanyuka anazungumza maneno, anasema futa, anafuta. Lakini akishafuta anarudia neno la kusema kwamba *message sent and delivered.* Hii inaonyesha kwamba ni madhumuni yanayotumika kuutumia ukumbi huu vibaya ili kupeleka ujumbe usiokuwa sahihi kwa wanaosikiliza, kwa wananchi ambao wanadhani kwamba hapa ni mahali pa watu kuja kutoa hoja zao ambazo hazijibiwi. Ninapenda kulishauri Bunge lako Tukufu kwamba sasa liongeze kipengele kingine ndani ya Kanuni kwamba Mbunge yeyote anayezungumza maneno ya uongo hana ushahidi, hata kama ametakiwa kuyafuta na akayafuta, bado apewe adhabu.

Mheshimiwa Spika, kusudi kuzuia tabia ya kusema uongo na kulitumia Bunge hili kusema uongo kisha kufuta na kuongeza maneno, *message sent and delivered,* hiki ni kitu ambacho ni dharau kubwa na kwa kweli hakijengi heshima ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba niseme kwamba hakuna haja ya kuunda Kamati Teule, maelezo yaliyotolewa yanatosha. Serikali yetu ni aminifu, inatenda kazi zake kwa umakini mkubwa, na maelezo yaliyotolewa yanatosheleza.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nitoe tu taarifa Mheshimiwa Ruth Msafiri amezungumzia Kanuni. Kanuni ipo. Sio kwamba haipo, Kanuni ya 59 fasili ya 3. Nainukuu, "..iwapo hadi kufikia mwisho wa muda aliopewa Mbunge aliyeamriwa kuthibitisha ukweli wa usemi wake, atakataa au atashindwa kutoa uthibitisho huo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge basi Mbunge huyo atachukuliwa hatua na Spika, kwa mujibu wa Kanuni wa 59(2)." *(Makofi)*

Lakini bado tunaendelea. Sasa namwita Mheshimiwa Maulidah Anna Komu, ajiandae Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya na atafuatia Mheshimiwa Suleiman Kumchaya.

**MHE. ANNA M. KOMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuiona *note* yangu ya kutaka kuchangia hoja hii na kunipa nafasi hii adhimu ya kuchangia. Kabla sijaanza hata mchango naomba kusema naunga mkono hoja kama wenzangu husema mia kwa mia, mimi naunga kwa mamilioini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea kwanza nikupe pole kwa kifo cha Mzee wetu, sisi wote na pia niungane na wenzangu kumpa pole Mheshimiwa Waziri Magufuli kwa kifo cha mzee wetu kwa sababu mzee wake ni mzee wetu. Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Amina!

Mheshimiwa Spika, naomba tukumbushane kidogo japokuwa wenzangu wanasema kwamba tusitumie majina ya viongozi kwenye ukumbi huu kwa kujinufaisha, lakini mimi kamwe kwenye maisha yangu sitasahau kauli za Baba wa Taifa, Mzee wetu Julius Kambarage Nyerere, na kila nitakapokuwa natoa mchango nikikumbuka kauli yake nitamtaja. Tena ninapomtaja huwa ninamtaja kwa uchungu mkubwa sana. Ama kweli kama Mwenyezi Mungu ameleta kitu kibaya duniani au kitu ambacho kinatuchosha kuleta kifo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuondokewa kwa baba yetu, tumeondokewa sana na nina hakika kwamba majadiliano haya yaliyopo leo katika Bunge lako yasingekuwepo. Mali ya nchi hii, madini ya nchi hii, alikabidhiwa yeye kutoka kwa wakoloni. Lakini hakuna kitu alichopenda kukihifadhi na kukienzi kama madini na mali kwa ajili ya kutuwekea sisi Watanzania. Leo ninapoona kwamba tunatumia mali hizi zote kwa kusema kwamba ati tunataka kufanya haraka kwa ajili ya mustakabali wa Watanzania, sikubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya tuzitumie kwa vitu ambavyo tunaviona kwamba havitaleta mjalada kwa Watanzania pindi wakivipokea. Mimi sioni tabu kabisa kwa nini Mheshimiwa Waziri amesaini mkataba Uingereza. Asaini mkataba Uingereza, Somalia, Ethiopia, popote atakapopaona yeye kwamba ana haraka ya kusaini mkataba.

Tatizo langu ni kitu kimoja tu, kuna tatizo gani wakati madini ya dhahabu tunayotafutia wafadhili yako Tanzania? Waziri wetu ni Waziri wa Wizara ya Serikali ya Tanzania. Mwekezaji anayekuja kuwekeza anakuja kuwekeza kwa madhumuni na mintarafu ya misaada na yote yaliyozungumzwa kuhusu shule na zahanati kwa ajili ya Mtanzania. Tuna haraka gani ya kuchukua mikataba hii ikasainiwe nje ya Tanzania wakati tunajua kwamba Watanzania wenzetu walio wengi ambao wananisikiliza, naomba wanisamehe, wengi wetu hatuelewi nini maana au faida ya mikataba juu ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila siku nitakuwa nakuambia na nikiwaambia ukumbi huu, tujitahidi sana kuwa wa wazi. Tujitahidi sana kuweka hivi vitu visilete maswali kwa sababu jambo hata likiwa zuri, lakini ukayajengea maswali mengi katika jambo lenyewe linakuwa si zuri tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimesema ninaunga mkono mamilioni kwa sababu sioni hata kitu kimoja kilichokuwa tatizo katika karatasi hii au katika hoja hii. Mheshimiwa Zitto kama alivyoambiwa kwamba hana anachokijua akasome, sawa! Lakini anachotaka kusoma ndiyo masuala zaidi ya 11 aliyoyatoa katika karakatasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimejaribu kupitia hii karatasi hii, naona mengi ni maswali anauliza, na kwa sababu hajui ndiyo alitaka kujulishwa. Sasa kuna tatizo gani la yeye kutaka kujua maana yake mtatutisha hata sisi wengine ambao siyo wacharukaji humu ndani.

Mtakapoona kuna jambo huko nje nikasema ngoja niende Bungeni kwa sababu nina uwezo huo nikaulizie nitakuwa naogopa, ninakaa kwa sababu nikiuliza nitaambiwa Mama Komu kajifunze zaidi hujui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nina hakika sisi wote wote hapa hata tuliomaliza miaka 30 katika Bunge hili kila siku mwanadamu anataka kujua zaidi. Sikuambii sisi wengine ambao ndio kwanza tumekuja na pengine tusirudi. Sasa miaka yangu mitano nisiitumie kweli kwa kuuliza kitu ambacho sikijui? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri ustaarabu wa mtu siyo kunyamaza kuuliza, ustaarabu wa mtu ni kuuliza ili apate jibu. Sasa maswali yaliyomo humu ndani mwanangu Zitto anachokitafuta hapa ni kutaka kujua je, katika haya masuala aliyoyauliza nikikupa mfano swali moja, anasema je, Waziri anatumia vigezo gani kusema mkataba mpya wa Buzwage uliosainiwa *London* hauna upungufu?

Anataka kujua tu, amweleze hivyo vigezo. Lakini sasa tukianza tena na kupeana maneno ya kashfa humu ndani tutakuwa kweli hatutendeani haki na hasa nikirudi tena, hii Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii sisi tunasema ni Msahafu au Biblia na kadhalika lakini ndiyo mwongozo wetu.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 100 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inataja kuwa kutakuwa na uhuru wa mawazo, majadiliano, na utaratibu katika Bunge na uhuru huo hautavunjwa wala kuhojiwa na chombo chochote katika Jamhuri ya Muungano ama katika Mahakama, au mahali pengine popote nje ya Bunge. Kwa hiyo, swali lolote lile mtakaloliona linanikita, nakuja kuliuliza kwa sababu sitapelekwa Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema kitu kidogo tu ambacho nimekinukuu hapa. Shule, zahanati pia zimetajwa kwamba wawekezaji hawa wanakuja hapa katika kuchimba hayo madini, wakati tunazungumza kila siku hapa, tujitahidi sana mali hizi tuzishike wenyewe Watanzania. Mimi nitarudia tena na tena kwa kusema tena na tena kwamba huwezi kumpa mgeni mali kama hizi za dhahabu, almasi na kadhalika achume akuachie wewe vyote. Lazima atahakikisha atapeleka kwao. Anachochukua yeye ni kingi zaidi, atachukua anakupa wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hizi shule na hizi zahanati basi mimi ningetaka zisiwe shule tu na zahanati na *shopping centre* kama wenzetu wanavyoendelea. Tusidanganye kwa sababu kama ni shule basi hata Watanzania tunachangishana tunajenga shule, kama zahanati ilizungumzwa hapa kwamba tumemaliza shule sasa tutaingia kwenye zahanati. Mimi nakwenda Mererani kila siku. Hali ya Mererani si nzuri na nina hakika kwamba na wewe pengine ulishapitia njia ni mbovu, maisha ya watu wa pale ukiwaona unawaona kwamba maisha haya si mazuri. Tumeanza lini kuchimba *Tanzanite,* miaka mingapi sasa *Tanzanite* inachimbwa. Kipo wapi hicho mwekezaji ambacho atatutishia kwamba ametuletea baada ya yeye kunufaika? Hii ni mifano midogo tu. Sasa tunapokuja pahala kama hapa tukawa tunataka kujua zaidi, lakini tukaleteana kashfa, tukaambiana maneno yasiyokuwa na maana, nasisitiza tena kwamba itakuwa siyo vizuri. Mimi ni Mbunge na wenzangu wote hapa ni Wabunge wa Majimbo, wameletwa na wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa, itapendeza na itausaidia mjadala kama na wewe utatathmini majibu ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu na wewe unaanza kusema vitu na kupuuza bila kuzitaja hoja zenyewe. Mheshimiwa Zitto katoa hoja. Mheshimiwa Waziri kazijibu hoja na kwa taarifa Waheshimiwa Wabunge kwa sababu mimi ni *fair* kabisa nimeagiza zimechukuliwa fotokopi. Dr. Slaa kama Kiongozi pale na mtoa hoja wanayo majibu ya Mheshimiwa Waziri. Sasa tukielekeza kujibu tusiseme tu kwamba kuna kashfa, inakuwa ni malumbano tu hayana maana. *(Makofi)*

**MHE. ANNA M. KOMU:** Ahsante Mheshimiwa Spika, nakusikiliza. Narudia tena samahani, kwamba alichokijibu Mheshimiwa Waziri sijapingana nacho na wala alichouliza Mheshimiwa Zitto sijapingana nacho. Isipokuwa narudia tena kusema kinachotakiwa hapa ni kuundwa kwa Tume tu kwamba Mheshimiwa Zitto aweze kujiridhisha na maswali yake 11 na zaidi ambayo aliyouliza kwenye hoja yake na Mheshimiwa Waziri kama alivyomjibu inawezekana kwamba Mheshimiwa alivyojibu yeye mimi nimeona nimeridhika kwa sababu amejibu vizuri. Je, mtoa hoja ameridhika?

Sasa ninarudia pale pale kusema kwa hizo hoja zilizoletwa katika Ukumbi huu isiishie hapa tu kwa vyovyote vile naunga mkono tena kusema kwamba Tume Teule iundwe na ichunguze jambo hili mpaka upatikane ukweli ili na wananchi wa Tanzania na wao waridhike kuona kwamba kweli Tume imeundwa na jibu limekuja zuri.

Sio kwamba kwa jinsi alivyouliza Mheshimiwa Zitto na jinsi alivyojibu Waziri tumeridhika sisi. Je, wananchi wote wameridhika? Iundwe Tume huru kabisa ije ichunguze jambo hili jibu lije hadharani na wananchi waridhie kwamba kweli Zitto kasema uongo, Waziri kasema kweli au Waziri kasema uongo Zitto kasema kweli.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja mamilioni. *(Makofi)*

**MHE. ANNA M. ABDALLAH**: Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anna Abdallah mwongozo wa Spika.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. Hivi hii sasa ni hoja ya Bunge ama bado ni hoja ya mtu binafsi. Yeye ameitoa mbele ya Bunge, Bunge tunajadili. Sasa hii hoja ni ya nani? Sio ya ndani ya Bunge? Inatakiwa sisi ndiyo tujiridhishe wote? Lazima aridhike mtoa hoja? Ndiyo nilitaka kujua tu hilo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hilo nilitaka kulisema. Lakini nadhani Mheshimiwa Anna Abdallah ameniwahi tu. Hoja ikishawasilishwa hapa, uamuzi wa usahihi wa yote yatakayosemwa ni uamuzi wa Bunge. Hatumfurahishi mtu, hatumfurahishi mtoa hoja, hatumfurahishi Waziri aliyejibu, hatuwafurahishi wananchi.

Jambo linaweza kuwa gumu. Lakini tunaotakiwa kuamua ni sisi humu Wabunge. Kwa hiyo, mjadala ujiekeleze katika hoja na majibu halafu Wabunge turidhike. Maana yake hatima yake tunapiga kura kuiamua. Kwa hiyo, jibu ni kwamba hoja hii ni ya Bunge sasa kuweza kufikia maamuzi. Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Suleiman Kumchaya wakati huo huo Mheshimiwa Chacha Wangwe ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kutoa pole kwako wewe na familia yako na familia ya marehemu na vilevile napenda kutoa pole kwa Mheshimiwa Magufuli kwa kufiwa na baba yake mzazi. Kabla sijatoa mchango wangu kuhusiana na hoja iliyowasilishwa hapa mbele yetu, naomba nikumbushe tarehe 28 Desemba, 2005 ulitoa picha katika Ukumbi wa zamani na tulishika Katiba ya nchi na tulishika *Quoran* na wengine walishika Biblia na tukasema kwamba tutailinda na tutaitetea Katiba ya nchi. Kwa hiyo, naamini kabisa tuko humu kwa mujibu wa Katiba na tunafanya kazi hii kwa kutumia Katiba. Kuna mtu anasema kwamba nani hajui ni katika kujenga hoja ndiyo nimeanza hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba unilinde.

**SPIKA:** Wewe unaongea unamwa-*address* Spika, hao wengine hawana hoja yoyote ya maana. Wangekuwa na hoja wangejiorodhesha kusema. *(Makofi)*

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Kama nilivyosema kwamba tuko humu kwa mujibu wa Katiba na hili Bunge sio letu sisi, ni la wananchi kwa sababu limepewa madaraka na wananchi kwa mujibu wa Katiba yenyewe inavyosema katika ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Naomba kunukuu: "…….kwa madhumuni ya utekelezaji wa madaraka ya Bunge…" Katika Ibara ya 63(3), kuna vipengele mbalimbali, cha kwanza kikiwa kinalipa Bunge uwezo wa kumuuliza Waziri yeyote swali lolote kuhusu mambo ya umma katika Jamhuri ya Muungano ambayo yako katika wajibu wake. Kwa hiyo, kutokana na jinsi mjadala unavyokwenda inaonekana kama vile kuna makosa yaliyofanyika kwa mtu kutoa hoja binafsi, kitu ambacho sijaona. Hii inakubalika kikatiba, hakuna mtu aliyevunja Katiba kwa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile Ibara ya 63(3)(e), inaturuhusu kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa. Ingawa siku zote tunaambiwa kwamba mikataba ni siri haturuhusiwi kujadili, lakini Katiba inaturuhusu kufanya hivyo. Kwa hiyo, sidhani kama kuna ubaya wowote kwa sisi kujadili hili suala. Nilikuwa naweka msingi wangu vizuri.

Mheshimiwa Spika, vilevile hapa tumeambiwa kwamba tunatumia jina la Rais lakini tunakumbuka kwamba tarehe 30 Desemba, 2005, Rais alisema kwamba mikataba itapitiwa upya. Mheshimiwa Waziri leo ametueleza kwamba mikataba imepitiwa upya na kuna baadhi ya vipengele ambavyo vimebadilishwa na vitaletwa hapa Bungeni.

Tatizo ni kwamba kama kweli haya yote yamefanyika ni kwamba taarifa ilikuwa haijafika na tulikuwa hatujaambiwa vipengele gani vilikuwa vimebadilishwa katika usainishaji mikataba upya. Labda ndiyo maana mikataba mingine imeendelea kusainiwa labda kama *Richmond,* na kadhalika.

Lakini kulikuwa hakuna taarifa yoyote Bungeni kuambiwa kwamba kuna taarifa italetwa ya Muswada ili ije kuwa Sheria ya Madini mpya baada ya kuifanyia marekebisho. Ndiyo kitu ambacho nakiona kwamba hakuna kosa lolote limefanyika kwa kuuliza chochote kwa sababu hatujapewa taarifa kwamba tayari wameshafanya mapitio ya kitu chochote. Wala Rais hajasema kwamba tumekwishafanya mapitio *(review)* ya kile nilichosema tayari kimeanza kufanyika. Kwa hiyo, naweza kuiweka hiyo sawa.

Mheshimiwa Spika, mimi naona bado kuna matatizo kidogo pamoja na kwamba tulikuwa hatujajua tayari mikataba imepitiwa upya na wala Rais hajatuambia kama tayari mikataba imeshafanyiwa mapitio sasa tunaweza kuanza mikataba mipya. Ninachoweza kusema ni kwamba nina maswali kidogo.

Swali langu la kwanza ni kwamba kwa nini mkataba huu wa Buswagi umesainiwa haraka? Yaani kulikuwepo na haraka gani ya kusainiwa na hasa nikarejea ukarasa wa 148 kulingana na majibu ya Mheshimiwa Waziri tarehe 16 Julai, naomba kunukuu; alisema kwamba: " Mgodi wa Buswagi katika tathmini ya mgodi, ni *marginal mine* ambao uhai wake si wa muda mrefu, bila kutumia fursa ya sasa ya bei ya dhahabu uwekezaji wake usingeweza kuwa wa faida…"

Kwa hili ninavyofahamu ni kwamba dhahabu inapanda thamani yake kila siku. Kwa hiyo, ile haraka ya kusema kwamba alikuwa anajitahidi kuwahi soko la bei ya dhahabu sioni kama ni sahihi ingawa sitaki kuhoji alichosema Waziri kwa sababu dhahabu siku zote inapanda thamani. Haiwezi kurudi nyuma yaani kama bei ya leo haiwezi kuwa sawa sawa na miezi sita ijayo. Mimi ndivyo ninavyofahamu. Kwa hiyo, inawezekana labda angeweza kusaini baadaye ingeweza kusaidia kwamba labda dhahabu ingeweza kuwa na bei kubwa na nchi ingepata pato kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, vilevile nikienda kwenye *Hansard,* naomba kunukuu jibu lingine alilosema Mheshimiwa Waziri ni kwamba yeye ametoka katika *private sector,*

kwa hiyo, anajali muda katika masuala ya biashara. Inawezekana kwamba hakukuwa na ubaya wowote katika kusaini ule mkataba huko *London.*

Maana yake inaonekana hapa tatizo ni kusaini *London.* Lakini naomba Wabunge wenzangu tukubali Kamati Teule iundwe ili kuondoa mashaka yoyote kwa sababu wakati anajibu watu wamechukua misimamo tofauti. Yaani kuhusu majibu kwa maana ya hoja iliyoulizwa na jinsi Waziri alivyojibu katika kuweka tu ule uwazi kwa sababu Serikali inasema kwamba inatawala kwa kuzingatia ukweli na uwazi. Na ni sehemu mojawapo ya uwajibikaji kwa kiongozi yeyote kukubali kama kuna *doubt* yoyote, kwamba Kamati Teule iundwe ili iweze kuondoa mashaka yoyote.

Mheshimiwa Spika, suala hili naliona sio la kiitikadi, maana yake inaonekana kama hapa limejengwa kuwa ni la kiitikadi. Mimi sioni kama ni la kiitikadi, bali ni kwa maslahi ya Taifa na tunafanya kazi hii kama nilivyosema kwa mujibu wa Katiba na Katiba inaturuhusu kufanya hivyo. Katika Ibara ya 100 tunaruhusiwa kutoa mawazo yetu na vilevile katika Ibara ya 63 tunaruhusiwa kuuliza swali au kuuliza jambo ambalo linaonekana labda lina utata kwa Waziri au swali lolote.

Kwa hiyo, naendelea kusisitiza kwamba hatutakuwa tumevunja Katiba wala Kanuni za Bunge kwa kuunda Kamati Teule. Naomba Kamati iundwe ili tuweze kujiridhisha hata kama siyo sisi basi wananchi huko nje kwa sababu kila mtu atalichukua kivyake na Mheshimiwa Waziri amesema kwamba inaonekana hapa palikuwepo na nia ya kuchafua jina lake. Wakati mwingine amewaza tu kwamba kulikuwa na nia lakini mimi sioni kama kulikuwa na kitu kama hicho, kwa sababu hoja nzima jinsi ilivyo inauliza tu maswali ambayo yalikuwa yanahitaji majibu.

Hakuna sehemu yoyote ambayo mimi nimeona lugha iliyotumika ni ngumu au mbaya kwa Mheshimiwa Waziri. Vilevile ninachoona kwa upande wa Mheshimiwa Waziri yeye ndiye ametumia lugha ngumu zaidi. Sasa naendelea kusisitiza kwamba ili jina lake lisichafuke kama alivyosema kwamba limechafuliwa, akubali Kamati Teule iundwe.

Nchi yetu hii tunasema kwamba inatawaliwa kwa mujibu wa sheria, kuna utawala bora, kuna taratibu, hivyo naomba ili haki hiyo iwepo na huo utawala bora uonekane, Waziri aonyeshe uwajibikaji wake na uwazi kwa kukubali Kamati Teule iundwe.

Hili kama nilivyosema siyo suala la kiitikadi ni kwa ajili ya kuondoa utata; na ni suala tu la kitaifa kwa sababu hata katika Katiba yetu imeonyeshwa kwamba tunaruhusiwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, sina zaidi, naomba kuunga mkono hoja zaidi ya asilimia 100. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii iliyotolewa na

Mheshimiwa Zitto Kabwe na kujibiwa vizuri sana na Waziri wa Madini na Nishati, Mheshimiwa Karamagi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kusema kwamba hakuna haja ya kuunda Kamati Teule ya kuchunguza utaratibu mzima wa mikataba na sheria ya madini kutokana na hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Zitto Kabwe. Ninasema hivyo kwa sababu majibu yaliyotolewa yako wazi kabisa.

Kitu chochote ambacho kinaeleweka kisichokuwa na utata kuna haja gani tena ya kuunda Kamati Teule? Tunataka tuunde tupate nini? Tupoteze pesa za wananchi bila sababu yoyote?

Juzi hapa tumetumia karibu shilingi milioni 400 bila sababu yoyote. Narudia tena, hivi kweli leo turudi huko huko kwa kitu kinachoeleweka? Mimi ningekubaliana na Mheshimiwa Zitto Kabwe kama Mheshimiwa Waziri asingekuja na kutoa ushahidi tosha tena ulioandikwa. *(Makofi)*

Lakini tuunde tu, hiyo si kweli hata kidogo! Mheshimiwa Zitto Kabwe anasema hivi; naomba kunukuu ukurasa wa tatu wa hoja yake: "Kwa kusainiwa kwa mkataba mpya wa madini wa mgodi katika (mradi wa Buzwagi) kati ya Serikali na Kampuni ya Serikali na Kampuni ya *Barrick* na sababu za mkataba huo kusainiwa nje ya nchi, *London,* Uingereza. Na vile vile kwa nini mkataba huo umesainiwa wakati bado Serikali inafanya durusu *(review)* ya mikataba kufuatana na maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ndugu Jakaya Mrisho Kikwete."

Mheshimiwa Spika, mimi hapa inanishangaza kidogo, na inanishangaza hasa baada ya kupata maelezo kamili kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Hapa tunachozungumza ni maudhui ya mkataba huu sio wapi mkataba umesainiwa. Kama kungekuwa na maelezo ya mkataba huu uliosainiwa *London* yanayohatarisha maslahi yetu hapo lingekuwa jambo lingine. *(Makofi)*

Kusainiwa *London* tu iwe ni hoja ya kuunda Kamati Teule, si kweli hata kidogo! Sababu zilizotolewa na Mheshimiwa Waziri zinatosha kabisa kuonyesha kwamba hakukuwa na madhara yoyote ya kusainiwa mkataba huu huko *London,* Uingereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 5 wa hoja ya Mheshimiwa Zitto Kabwe, anasema hivi: "Mheshimiwa Spika, kumbukumbu hizo zinaonyesha kwamba Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 *(Finance Act No. 14 of 2001)* ilifanyiwa marekerisho kadhaa yakiwemo marekebisho ya Sheria ya Madini Kifungu cha 87, ambapo kifungu kidogo cha 3 cha kifungu cha 87 kiliongezwa kidogo, hicho kinasema nanukuu…"

Akanukuu kama alivyonukuu. Alipokuja Mheshimiwa Waziri ameeleza kinaganaga ukweli wa kifungu hiki, kwamba ilivyokuwa katika hoja yake si kweli. Na mabadiliko haya yalifanyika rasmi, ushahidi umetolewa. *(Makofi)*

Leo tunang'ang'ania tuunde Kamati Teule, ya nini? Mimi wasi wasi wangu kwamba ndani ya Bunge hili panaweza kuwa uwanja wa siasa badala ya kuwa uwanja wa kuwatumikia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchaguzi tulimaliza nje, hapa ndani sote sisi ni Wabunge kazi yetu kubwa ni kuwatumikia wananchi na ndivyo viapo tulivyoapa tarehe 28 Desemba, 2005.

Mheshimiwa Spika, hakuna hata Mbunge mmoja humu ambaye yuko hapa hajali maslahi ya wananchi hata kidogo na ndiyo maana kila tunaposimama, tunazungumza maslahi ya wananchi. Nomba twende tufike mahali tuanze kutumia Ukumbi huu kama jukwaa la kujijenga kisiasa, tutafanya makosa makubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, lazima niseme ukweli, binadamu ni binadamu, awe mtu wa kawaida, awe kiongozi, awe Waziri, Naibu Waziri, Mbunge, anahitaji heshima, anahitaji kulindwa ili heshima yake isiharibike. Tunapokuja kuzungumza mambo haya lazima tujue kwamba, unachokizungumza hakitamshushia heshima yake binadamu mwenzangu kama mimi. Ndipo tunapotakiwa tuseme ukweli katika mambo yetu yote ambayo tunayazungumza hapa katika Bunge letu hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa tisa, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, anasema hivi naomba kunukuu: "Mheshimiwa Spika, suala ambalo linanipelekea kuomba kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge kuchunguza Mkataba huu mpya ni kuhusu uharaka uliopelekea Waziri wa Nishati na Madini kusaini Mkataba huu. Sheria ya Madini bado haijarekebishwa, je, Waziri anatumia vigezo gani kusema Mkataba Mpya wa Buzwagi aliousaini London, hauna mapungufu."

Mheshimiwa Spika, tumepata majibu yake, nia yetu Watanzania ni kutaka kwenda kasi. Huyo Baba wa Taifa ambaye wenzetu wanamtumia hapa bila utaratibu, alisema hivi "wakati wenzetu wanatembea sisi tukimbie." Huku ndiko kukimbia kwetu. Mheshimiwa Waziri, amekuwa na safari ya London, ameikuta *Board* ya *Barrick* inafanya mkutano, nafasi ndiyo ile ile Watanzania tunataka kukimbia, hivi arudi Tanzania awaite waje huku tena, Tanzania tuko peke yetu hapa duniani; si kweli maana yake nini huku maana yake kutokujali hamu ya wananchi wanaotaka kupiga hatua katika maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hakuna baya alilolifanya Mheshimiwa Waziri, kusaini Mkataba huu London. Alichofanya ni kujali maslahi ya Watanzania, ametueleza hapa jinsi tutakavyofaidika na mambo chungu mzima.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme jambo moja, ni kweli kabisa Baba wa Taifa, alitulindia madini haya, ili tufike mahali tuyatumie vizuri. Nataka kusema hivi na ndiyo maana tumefika, tumewaambia makampuni haya makubwa makubwa kwa sababu ya

elimu hiyo ambayo Baba wa Taifa aliisubiri kwamba, jamani na sisi tunataka kufaidika na madini haya. Hiyo ndiyo elimu ambayo huko nyuma tusingeweza kufanya hivyo, lazima tujivunie kwamba sasa tunaweza kusema hapana. Huko nyuma tulikuwa hatuwezi kufanya hivi.

Mheshimiwa Spika, naomba kurudia tena, sisi tuna kazi moja tu ya kumtumikia Mtanzania na ndiyo kiapo chetu na ndiyo kazi yetu. Kwa hiyo, tunapokuja hapa tuje na uhakika na yale ambayo tunayazungumza ili tuifanye kazi hiyo vizuri na wananchi wakisikia wajue kweli Wabunge wanafanya kazi yetu. Tuko hapa kwa niaba ya Watanzania milioni 36. Ninawaomba wadau wote wa maendeleo katika Tanzania walikubali hili, tuache tabia ya kujengana bila sababu yoyote, tutafika mahali tutahesabiana nani alikuwa anatumikia wananchi na nani alikuwa anataka kujijenga yeye mwenyewe. Haya mambo tunayoyasema hayakuwahi kutokea tu Tanzania hapa, yametokea katika nchi nyingine nyingi tu.

Mheshimiwa Spika, kengele ya kwanza imelia ya pili karibu italia, nasema kwa hili ambalo limeeleweka kwa majibu sahihi ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, hatuna haja hata kidogo ya kuunda Kamati Teule bila sababu za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu. Kwanza kabisa, napenda kukupa pole kwa msiba wa mjomba wako, ambaye Tanzania inamtambua kama mwanaharakati wa kweli, ambaye alitumia muda wake mwingi sana kuwapigania wananchi na hakuona kama chama kilikuwa ni kigezo kikubwa, ndiyo maana aliweza kuwa hata upande wa Upinzani. *(Makofi)*

Pia napenda kumpa pole Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa John P. Magufuli, kwa kifo cha baba yake mpendwa. Mheshimiwa John P. Magufuli, ameonesha kwamba na yeye ana uwezo wa kusimamia ukweli na ndiyo maana kila wakati anakuwa na maadui wengi. Kwa sababu haki siku zote inaposimamiwa ni lazima wale wasiopenda haki wafanye uadui na waweze kukejeli ili kuifunika haki. Lakini mimi nasema ya kwamba, nikiwa kama Mbunge ambaye nimechaguliwa na nimekuja hapa pamoja na Wabunge wenzangu, tukala kiapo, kwa sababu sisi Wakurya na Waafrika kwa ujumla, tunaogopa sana kiapo. Unapoinua mkono wako hapa na kusema ya kwamba, nitailinda na nitasema kweli daima, kinyume chake ni kwamba, hicho kiapo kitakumaliza wewe. Kwa hiyo, wale ambao wanakiuka viapo vyetu hapa, kwa kutaka kugeuza uwongo uwe ukweli, basi wananchi wanaona, Mungu anaona na dhamiri zao zinawashitaki kwamba haya wanayoyasimamia ni mambo ambayo hayana ukweli wowote.

Kwa kuwa Mungu ni Mungu wa haki na Wananchi wa Tanzania wanachokitaka ni haki, mimi naunga mkono hoja hii mia kwa mia kwamba, ili tujiridhishe na pia Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, ambaye mimi ninamheshimu sana ni msomi mzuri na anafanya kazi kwa bidii, ili hiki kiwingu cha kusema ameharibiwa jina

kiondoke ni lazima kuwe na Tume ambayo itachunguza haya mambo na kuyaweka bayana ili wananchi wote wafahamu na Wabunge, pamoja na mtoa hoja aridhike ya kwamba, kweli hayo mambo yamechunguzwa. Tumeunda Tume nyingi tu hapa na suala la hizi Tume Teule ni la kawaida katika Bunge lolote la *Commonwealth* na tumeunda Tume hata za kumchunguza Mheshimwa Chacha Zakayo Wangwe, kama amesema ukweli, zimetumia fedha zikakaa huko Mara na zikagundua ya kwamba, amesema ukweli. Tumeunda Tume hapa hata za kumchunguza Mheshimiwa Adam K. A. Malima. Hizi Tume zinaundwa ni jambo la kawaida, kwa nini hapa Wabunge mnaona uzito sana na mnaona shida sana Tume hii kuundwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, unachanganya mambo bure. Kanuni ya 104 inaunda Kamati Teule, hata neno Tume sijui mnalipata wapi. Hayo yote mengine unayoyataja, Spika alikuwa anateua Wabunge wachache kwenye Kamati kuweza kumshauri juu ya ukweli wa jambo ni tofauti kabisa na Kamati Teule, chini ya Kanuni ya 104. Ningeomba Waheshimiwa Wabunge, tuna hoja ya Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, tunayo majibu ya Mheshimiwa Waziri, yanasambazwa kwenu hivi sasa. Hivi kuna ugumu gani kwenda kwenye hoja, mbona mnazungumza mambo, mnajaribu Baba wa Taifa mwende wapi, twende kwenye hoja tujaribu kuzijibu ili tuzifafanue.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru katika yote, uniongezee dakika zangu tatu ili nimalizie. Hili ni tatizo la Kiswahili, mimi ni lugha yangu ya tatu, Tume, Kamati mimi nazungumzia *Select Committee* basi tuseme ni Kamati Teule, ndiyo maana yake na ndiyo tunayoizungumzia hapa. Ninasema hili liliagizwa na Rais, siku alipozungumza hapa Bungeni akasema ya kwamba, Mikataba itapitiwa. Kwa hiyo, sio lazima tumsubiri yeye aje kutuambia hapa, ameshatoa agizo kwamba Mikataba ichunguzwe na hapa naona imeandikwa ya kwamba, ni Tume Teule ya Bunge kuchunguza mapitio ya Mikataba ya Madini na Mazingira.

Kwa hiyo, wakati umefika sasa ili haya mambo yachunguzwe kwa sababu wanataka kuyajua na si hayo tu, mimi naweza nikakupa mfano kwamba, Waziri wa Nishati na Madini si wa kwanza kufanya kitu ambacho kinaonekana kiko kinyume, hata waliotangulia na wote wa Wizara hiyo ni lazima wachunguzwe vilevile, wengine wanashika nafasi za juu sana sasa hivi. Hata mwaka 1980, Sheria ya Madini inatamka bayana ya kwamba, maeneo yaliyo kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo na yale ya wachimbaji wakubwa, yatakuwa hivyo na wasiingiliane. Tunaona ya kwamba, maeneo ya Mara yote yalitengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo kuanzia mwaka 1980 na Mawaziri waliyalinda hadi mwaka 1996, lakini ilipofika tarehe 14 Juni, 2006, alikuja Waziri ambaye aliyageuza yale maeneo na kuwapa wachimbaji wakubwa bila ridhaa ya wananchi na bila kuzingatia sheria inakataa. Hilo nalo linahitaji kuchunguzwa, ni sehemu ya haya.

Kuna mengi sana ambayo yanahitaji kuchunguzwa katika migodi yote ambayo imepewa makampuni makubwa, pamoja na hii Kampuni ya *Barrick*, ambayo sasa hivi tunaamini ya kwamba, ina ukaribu sana na Serikali na Mikataba inaweza ikasainiwa hata Motrio Cananda, lakini hiyo Mikataba basi iletwe hapa tuione, wananchi nao wajiridhishe kwamba kweli hiyo Mikataba ilikuwa ni sahihi. Kuna tatizo gani, kwa nini

inakuwa hofu kubwa sana halafu Wabunge hapa wanataka kufanya kitu kama ushabiki? Hii ni kazi ya wananchi tumepewa hapa kesho na kesho kutwa watakuja wengine tunataka iwe *on record* kwamba, hayo mambo ambayo yanasemekena yalikuwa ni kinyume yamekuwa *straight*.

Kwa hiyo, mimi navyoona ni kwamba, tusiwe tunatumia Bunge kama sehemu ya ku-*justify* mambo ambayo si ya kweli. Tumeapa kwamba tutailinda Katiba na ningependa kutumia hii nafasi kusema ya kwamba, viongozi wetu ambao ni Mawaziri, wawe wanasimama kutetea kiapo chetu na wasitake kugeuza hili Bunge kama sehemu yao ya kupindisha Sheria za Katiba ya nchi. Kwa mfano, natoa mfano hai, hivi majuzi niliuliza swali kwa nini Tarime kwa mfano, itawaliwe kinyume cha Katiba na Sheria? Akasimama Waziri wa Utawala Bora, akasema kwamba, wale watu sio Watanzania kama Watanzania wengine, tangu ukoloni bila Katiba. Akasimama Waziri Mkuu naye akathibitisha hivyo hivyo kwamba...

**SPIKA:** Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, nenda kwenye hoja, tuna hoja ya Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, vinginevyo nitakuzuia kabisa kusema kwa sababu huelekei kuchangia hoja.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa natoa mfano, jinsi Mawaziri wetu wanavyokiuka Katiba hapa Bungeni na ingefaa waombe radhi kwa hayo waliyoyatamka kwa ajili ya watu wa Tarime. Mimi nasisitiza ya kwamba, kitu cha kuogopa mimi sina bwana, mimi nawakilisha wananchi hapa. Nasema, hii Tume, yaani hii Kamati Teule ya Bunge iundwe ili ukweli uonekane.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Kanuni.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU:** Kanuni ya 55, naomba mwongozo wako Mheshimiwa Spika, kwa sababu mchangiaji wa hoja hii, naona sasa hivi anageuza hoja hii kuwa ni kama uwanja wa kuanza kuleta malumbano na hoja ambazo hazina msingi na kutoa matamshi ambayo yanaendana na kupotosha watu. Kwanza, naomba umtake aeleze na atoe ufafanuzi kwamba ni kwa vipi Mawaziri wanavunja Katiba na wanakwenda tofauti na Katiba inavyoagiza. *(Makofi)*

Lakini pili tunamwomba Mheshimiwa Mbunge, anavyozidi kuchangia aende kwenye hoja na asianze kutafuta mambo ambayo hayahusiki. Bunge hili sio mahali pa kuhalalisha uwongo kama anavyodai kwamba sasa hivi tunageuza uwongo kuwa ukweli sio kweli. Ukweli umewekwa wazi na Mheshimiwa Waziri na kama hoja basi hoja itolewe kupinga yale yaliyozungumzwa na Mheshimiwa Waziri katika kujibu hoja za mtoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo sio kuuliza swali, kila mtu ana fursa ya kuuliza swali na akajibiwa, tatizo ni jinsi lilivyoulizwa kwamba, Mheshimiwa Waziri amedanganya!

Ukianza na shutuma umejibiwa ukweli sasa Bunge linatakiwa hapa kusema kwamba, je, hiyo shutuma ilikuwa ni ya ukweli? Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwanza, nikuhakikishie kwamba, dakika zako tunazihifadhi, lakini ni wewe mwenyewe unajisababishia matatizo, kwa kwenda nje kabisa ya mada na Kanuni haziruhusu. Namshukuru sana Waziri wa Nchi, anatukumbusha hilo. Tuhuma ya kusema kuna Mawaziri kadhaa wanavunja Katiba ndani ya Bunge ni nzito sana, lakini hazihusiani na mada hii, kilicho mbele yetu hapa ni Serikali kutiliana sahihi Mkataba wa Mgodi wa Buzwagi, wala sio Sera ya Madini, kama wengine mnavyoendelea. Mimi napenda Waheshimiwa Wabunge, turudi kwenye mada yenyewe ili tuweze kujua ukweli uko wapi na uwongo uko wapi.

Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, ametoa hizo tuhuma kama 11, Waziri amezijibu kwa mpangilio moja baada ya nyingine, semeni majibu yanatosheleza wapi hayatoshelezi, tutafikia mwisho vizuri tu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Chacha Wangwe kwa maelekezo hayo hebu endelea sasa kwenye mada.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, mimi ninaheshimu maelekezo yako na ninaamini kabisa ya kwamba, unaongoza Bunge letu kwa njia nzuri. Mimi nilikuwa najaribu kuelezea kile ambacho kimezungumzwa hata na Wabunge wenzangu hapa ya kwamba, Mheshimiwa Waziri hadanganyi na hoja iliyopo hapa ni kwamba, anadanganya na mimi nikawa natoa mifano hai, ambayo nimeishuhudia hapa na Wabunge wameishuhudia na wananchi, jinsi ambavyo Mawaziri wanadanganya hapa Bungeni.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika - kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Haroub Said Masoud.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, natumia Kanuni ya 50(8)(b) na naisoma kama ilivyo, inasema: “Kutumia haki yake ya kusema kwa madhumuni ya kutaka kuchelewesha Shughuli za Bunge.” Mhusika amefahamishwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, lakini bado anaendelea na kwa nia hii ina maana anataka kusababisha Shughuli za Bunge zisiendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwenyewe umemfahamisha vizuri, sasa sielewi kama hajui kanuni au anataka kuibeza kanuni hii, naomba kuwasilisha? *(Makofi)*

**SPIKA:** Nampa nafasi ya mwisho Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, kurudi katika mada yenyewe. Tafadhali rudi katika mada iliyo mbele yetu, ukirejea tena kwenye njia zako hizo ambazo hazielewiki, itabidi nikusitishe.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kutambua kwamba, wewe ni *preciding* wa ku-*guide debate* hapa Bunge. Hawa wanaojaribu kunishika koo, wangeacha nimalize kujenga hoja lakini basi, narudi kwenye hoja, maana tunafahamiana hapa. Ni kwamba, hoja iko pale pale, ningeomba Waheshimiwa Wabunge ambao tunawawakilisha wananchi, waruhusu Kamati Teule ya Bunge iundwe kwa ajili ya

kuchunguza hii Mikataba yote na mambo ambayo yamekuwa ni kero kwa wananchi, kuhusiana na mambo ya migodi kuanzia Mikataba na yale yaliyojitokeza juzi ya kuendelea kusaini Mikataba mingine wakati ile aliyoisema Rais haijachunguzwa.

La kwangu ni hilo. Lakini pia naomba uendelee kufanya nguvu ili hili Bunge lizidi kuwa la kidemokrasia na lisiwe ni Bunge la mashabiki, ambao wanakuja hapa kufanya kama kijiwe cha chama chao hapa. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J . LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ili na mimi nichangie katika hoja hii muhimu iliyo mbele yetu. Awali ya yote, nami niungane na Wabunge wenzangu, kukupa pole wewe binafsi na familia yako, pamoja na familia ya mzee wetu, Chifu Abdallah Fundikira, ambaye kwa kweli amelitumikia Taifa hili kwa muda mrefu na kwa uaminifu wa uadilifu mkubwa, pole sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nadhani tayari umetuongoza jinsi gani ya kujielekeza katika hoja hii na mimi nadhani nitatumia yale ambayo umetuambia. Awali ya yote, naomba niunge mkono hoja hii mia kwa mia kwamba, Kamati Teule iundwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda nianze kwa majibu ambayo Mheshimiwa Waziri ametuambia, hili la kwake ambalo amesema kwamba, amechafuliwa sana jina lake. Kimsingi nakubaliana naye, lakini pia hapo hapo akasema haoni haja ya kuundwa kwa hii Kamati Teule.

Mheshimiwa Spika, mimi naona hapa kuna *contradiction,* kama kweli amechafuliwa jina lake kiasi hicho alichosema na naamini ni kweli kwa sababu ni mtu mzima, ana uzoefu mkubwa na ameona kwamba amechafuliwa. Njia pekee ya kusafisha jina lake ni Kamati Teule kuundwa, kwa sababu itaangalia kama Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto kweli amesema uwongo ama ni yeye. Kwa hiyo, Kamati Teule pekee ndiyo itaweza kumsafishia jina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naelewa kwamba, hapa kama itapigwa kura ni ukweli ulio wazi kwamba, Serikali itashinda, kwa sababu hata tunavyosimama kujielekeza katika hizi hoja imeonekana kabisa kuna mpasuko kwamba, upande wa Serikali wanatetea kusiwe na Kamati Teule lakini upande wetu tunasema kuwe na Kamati Teule. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nashauri, kama mwenzetu alichafuliwa jina, njia peke yake ya kumsafishia ni kuundwa kwa Kamati ambayo itatoa taarifa kamili ya nani amesema ukweli na hapo wananchi wataelewa kwa sababu tukipiga kura hapa nakubali kabisa kwamba, wananchi hawataelewa kama kweli Mheshimiwa Waziri, anasema kweli au Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto amesema kweli. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tukubaliane kama kweli tunataka kumsafishia Mheshimiwa Waziri jina lake, Kamati Teule iundwe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hatua ya kwanza Mheshimiwa ni kujadili kama majibu ya Waziri yanatosheleza ama hayatoshelezi. Mantiki inataka tutathmini majibu ya Mheshimiwa Waziri, kila saa nawarudisha huko hamkubali, kama huna hoja wala usijiorodheshe tu, maana yake kama huwezi kusema tathmini ya aliyoyasema Mheshimiwa Waziri, sasa tutaridhika vipi Bunge zima kuunda ama sivyo itakuwa kila anayejisikia anaomba Kamati Teule, hili litakuwa Bunge la Kamati Teule tu sasa. *(Kicheko)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa mwongozo wako, lakini nadhani nilichokuwa nakisema ni kujibu kile alichosema Mheshimiwa Waziri kwamba, haoni haja ya kuundwa kwa Kamati Teule, lakini mimi nasema kuna haja. Kwa sababu kama kweli yeye anaona hakuna sisi pia tunaona kuna haja, sababu ya hizo hoja ambazo wamezileta ambazo mimi nadhani hazijajibu hoja zote za Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto.

**SPIKA:** Zitaje sasa hizo hoja.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, labda niende kwenye suala zima la ajira. Mheshimiwa Waziri, wakati anajibu amesema kwamba, kampuni hiyo ya Buzwagi itaweza kuajiri wafanyakazi 696. Tutakubaliana kwamba, kumekuwa na wawekezaji wengi katika madini na siku zote ajira hazijapatikana, wengi wanaoajiriwa wamekuwa ni makampuni kutoka nje, kwa hiyo, bado nadhani hii si hoja. Lakini pia amezungumzia suala la tofauti kati ya kudurusu Sheria na kudurusu Mikataba.

Mheshimiwa Spika, mimi naamini kabisa Mikataba hii inaandikwa kisheria, sasa ninashangaa hii *contradiction* iliyoko inatoka wapi, yeye anadai kwamba Mikataba imeshafanyiwa *review* lakini hapo hapo anasema Sheria ndiyo hazijafanyiwa *review?* Sasa mimi najiuliza hivi hii Mikataba inafanywa bila Sheria, kwa sababu naelewa Mikataba mingi inafuata Sheria, sasa kama sheria hazijawa *reviewed,* hii Mikataba inakuwaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini labda niende kwenye hoja za Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, kama nilivyosema awali, naunga mkono lakini mimi nadhani tatizo hapa sio suala la Mkataba umesainiwa wapi, kama alivyosema mwenzangu ni kwamba, hata ungesainiwa Nairobi, ungesainiwa Marekani sisi hatuoni tatizo. Lakini tatizo tunaloliona sisi ni ule uharaka wa kusaniwa kwa huu Mkataba wakati tulishaambiwa kwamba, bado kuna *review* zinafanyika. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nadhani hoja hapa ni Waziri atuambie kwa nini amesaini Mkataba *whether* ni Dar es Salaam au ni Uingereza, lakini tunataka kujua kwa nini umekuwa na uharaka kiasi hicho cha kusaini Mkataba huo?

Mheshimiwa Spika, lakini lingine nililotaka kulizungumzia, kuna ile methali inayosema "kizuri chajiuza kibaya cha jitembeza." Ninaamini kabisa sisi migodi yetu ni mizuri, kwa hiyo, kama Waziri ni Mtanzania ni hii kampuni iko Tanzania hatuoni sababu kwa nini aende mpaka nje huko kwenda kusaini na je, gharama hizo zilikuwa za watu gani kwa sababu hapa tumeambiwa kwamba hii Kamati itachukua hela nyingi lakini bado gharama walizotumia wao kwenda nje zilikuwa si kodi za wananchi?

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kwamba, naomba niunge mkono hoja kwamba, Kamati Teule iundwe ili tuweze kupata ukweli wa mambo yote asante. *(Makofi)*

**MHE. ADAM K. A. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja hii binafsi.

Mheshimiwa Spika, mimi pia kama walivyofanya wenzangu, nianze kwa kukupa salamu za pole kwa msiba wa mzee wako na mzee wetu, Chifu Abdallah Fundikira, Mungu amlaze mahali peponi, *amen*.

Mheshimiwa Spika, hoja iliyoletwa hapa mimi jana nilisikia na wakati nazifanyia tafakari kama nitachangia au sitachangia, nadhani katika mambo niliyoyasikia moja ilikuwa ni suala la kwa nini Mkataba huu ulisainiwa London na kulikuwa na uharaka gani halafu kwa yale ambayo niliyapata mimi sijui kama nimekosea, nadhani kulikuwa na hoja kwamba, Waziri wangu wa Nishati na Madini anatuhumiwa kwamba, alikiuka sheria na taratibu. Katika majibu yake aliyoyatoa humu ndani ya jumba lako hili Tukufu kwamba, alisema uongo.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa mujibu wa kanuni zako za Bunge na sisi wengine tumepata bahati *by necessity* kuzisoma hizi kanuni na kuzielewa vizuri tumepata kuzielewa sasa hivi na kusema kweli tuhuma ya kumwambia Waziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, ambaye anaapa mbele ya Rais kwamba anakuja katika Bunge hili na kusema uongo ni tuhuma nzito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naungana na wenzangu ambao wanasema kwamba, kama kuna hoja basi ziletwe. Kama ninavyosema, baada ya kupata ule mtihani kidogo huwa siachi mbali kanuni zangu, naomba nisome yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kamati Teule, Kanuni ya 104(1), Kamati Teule yaweza kuundwa na Bunge kwa madhumuni maalum, kwa hoja mahususi itakayotolewa kwa ajili hiyo na kuafikiwa. Hapa pana suala la madhumuni maalum, hoja mahususi ndio zimeletwa kama ndio hizo mahususi zimeshajibiwa. Sasa hoja zimeshajibiwa tunazijengea hoja, bado tunataka Kamati Teule ya nini tena jamani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba kubwa zaidi kwamba, mwaka huu mwezi wa tatu au wa nne sikumbuki, ilifanyika semina ya Viongozi Waandamizi wa Serikali na Mashirika ya Umma na katika hilo ambalo nadhani alikuwa Katibu Mkuu Kiongozi, wakati anatoa mada yake alisema kwamba, lazima tuwe na utaratibu Tanzania hatuwezi kuendesha kama *business as usual*, kama kuna *opportunity* ambayo inayojitokeza ya kwamba tuna *emergency investor* anatokea tunataka tuanze kurudi twende wapi, turudi hizi, tufanye nini *opportunity* inapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri wangu wa Madini, mimi nina *gas* Mkuranga, bado suala linajadiliwa ikitokea *opportunity* ya kuja na *investment* namna hiyo, mimi naomba afanye haraka, hata ikiwa kusaini huko New York au wapi afanye. Lililokuwa linanisumbua mimi ni manufaa ya dhahiri ya mradi huo yapo au tumefanya

haraka kwa sababu kuna jambo lilitaka kujificha? Waziri ametoa maelezo kwamba, alisaini *one* kwa sababu kulikuwa na *window of opportunity* ambayo ilikuwa inaisha Machi, 2007, lakini baada ya kupata ushauri wa *Mining Advisory Committee,* akakaa na kusema kulikuwa na mrabaha na kodi ya milioni zinazotarajia kufikia *198 million US Dollars*, *pay as you earn* milioni 50, mambo ya *investment* za umeme na *infrastructure* nyingine *totalling to 800 million US Dollars*. Sasa *opportunity* kama hiyo kweli unaiacha tu, hili jamani hebu njooni tukazungumzie Dar es Salaam, mimi sijaelewa!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba niseme nimeridhia majibu ya Mheshimiwa Waziri na kwa mujibu wa tafakari ninayoifahamu mimi tangu tukiwa katika kampeni, ari mpya na kasi mpya ndiyo hii. Sasa kama kuna watu wanataka kuturudisha nyuma, kama anavyosema Waziri Mkuu, hao wako kwenye boti lingine siyo boti hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala hili ambalo nimeona hapa kidogo kulikuwa na hoja ya kusema kwamba, mtoa hoja ameuliza swali, ameomba mwongozo, lakini mimi nadhani kwenye ile hoja ambayo ilisema kwamba Waziri amelidanganya Bunge, pale sidhani kama kulikuwa na swali, kwa sababu sikuona mfumo wa swali.

Nimeona suala la shutuma *direct* iliyoenda kwa Waziri wa Serikali na hapa hatuko *by partition* lazima tukubaliane kwamba, lile halikuwa swali bali ilikuwa shutuma na hivyo Waziri ana kila haki ya kujisikia kwamba, amekuwa *defemed* na sababu ya sisi kuzungumza humu ndani ni kuliweka sawa. Sasa sijui kwa nini mtu anasema tunaomba tena Kamati Teule ichunguze kama Waziri a-*feel aggrieve*, jamani mtu akitukanwa si lazima ajisikie vibaya kwa hiyo, mpaka iundwe Kamati Teule ndio ujisikie, kama ametukanwa na alijisikia vibaya anajisikia vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tumo humu ndani na tuna uwezo wa kusema uongo, tumeuona dhahiri, tukikubaliana basi tumekubaliana na lichukuliwe hatua nyingine. Kwa mujibu wa Bunge lako Tukufu na Kanuni zilizopo kwa hivi sasa, mimi nataka kusema kwamba, kwenye upande wa *economic opportunity* iliyokuwa imejitokeza, kwa maelezo haya, labda kama mtoa hoja anataka kusema kwamba maelezo haya hayako sawa, lakini kama maelezo haya yako sawa, mimi nampongeza Mheshimiwa Waziri na ninamkaribisha Mkuranga, atufanyie hivi hivi kwenye suala la gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite pale alipozungumza kaka yangu, Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya kwamba, tunapozungumzia masuala kama haya tutambue kwamba, tunataka tuwe *by partition* na pia tuheshimu *origins* za watu wote humu ndani tunakotoka. Kwa hiyo, mimi naomba niseme tu kwamba, kama alivyosema Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, tunapozungumza humu ndani tukae tukijua kwamba, Watanzania chungu nzima wako huko nje wanatuangalia, tuna *obligation* ya kusema yale ambayo tunaamini ndani ya nafsi kwanza, pili kama ndio kuna hoja nyingine ambazo ni za kujengewa, basi nazo zifanyiwe tafiti na sisi kama wachumi, Wabunge na Wanasheria, tuna *specialization* nyingi humu ndani, *obligation* yetu ni kufanya utafiti wa kina.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nimshukuru Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, sikuona chochote ambacho amefanya ambacho kinaenda kinyume na maagizo aliyopewa kama Kiongozi wa Chama cha Mapinduzi. Naomba nimshukuru kwamba, katika ku-*promote investment* hiyo ndiyo sehemu ya Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi na sisi wengine ambao tunajali tumuunge mkono hapa Bungeni, kila atakaposimama yeye na Mawaziri wenzake kuuhami uchumi wa nchi hii, sisi ni wajibu kuwatetea kwa kila hali.

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho, naomba niseme tu kwamba, haya mambo ya kuleta hizi fitina na ghasia, watu wakae na kujua kwamba tunatazamwa nje. Sasa mnapojenga hoja hizi na mnatumia fursa hizi za Viwanja vya Bunge kuleta maneno ya uongo namna hii, mimi naomba Bunge lako litumie kanuni zilizopo ili mambo haya ya kuliongopea Bunge hapo tutakapothibitisha na tutathibitisha hapa hapa mchana tutajua uongo uko wapi, tukapothibitisha, basi Bunge lako lichukue hatua hapa hapa ili iwe mfano kwa atakayekuja baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na mengi ya kusema lakini nimezidiwa, mengi yamesemwa na walionitangulia. Naomba kumpongeza sana Waziri wa Nishati na Madini, kwa majibu yake mazuri sana na naomba kuwasilisha. Asante sana. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nami nashukuru pia kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kidogo hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza, naomba nichukue nafasi hii kukupa pole wewe mwenyewe, familia ya Marehemu Chifu Abdallah Fundikira, pamoja na Watanzania wote, kwa msiba mzito uliotupata. Pia naomba kumpa pole Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa John P. Magufuli, kwa kifo cha mpenzi baba yake, Mungu aziweke roho za marehemu wote peponi. *Amen*.

Mheshimiwa Spika, naanza mchango wangu kwa kuunga mkono hoja kwamba, kuna kila sababu ya kuundwa Kamati itakayoangalia nini kilichosainiwa kwenye Mkataba uliosainiwa huko nje. Suala la Mikataba mibovu hapa Tanzania ni tatizo kubwa sana na kila mmoja ameona hili suala siyo Wabunge na si Watanzania wanaotuangalia, wamekuwa wakiangalia ni jinsi gani Mikataba mibovu imepelekea Taifa hili pasipoeleweka. Mikataba mingi mibovu imetupeleka pabaya sana, Serikali wakati mwingine imekuwa inaingia hasara kubwa kwa sababu Mikataba inayoingiwa inakuwa haina utaratibu mzuri, haina umakini na hivyo kulileta Taifa hasara kubwa.

Suala la Mikataba ya Madini ni suala zito ambalo ni la msingi kabisa, sisi Wabunge tukiwa kama wakilishi wa Wananchi, tusilichukue kirahisi rahisi hivi hivi. Nina imani kabisa hapa Bungeni hakuna Mbunge ambaye hajawahi kuona na kuguswa na ubovu wa Mikataba ilivyopelekea Taifa hili pasipoeleweka. Watanzania tuna rasilimali nyingi sana, tuna madini mengi sana, lakini kila siku hapa Bungeni tumekuwa tunasema kwamba rasilimali zetu hazitumiki ipasavyo, matumizi yake siyo mazuri, wanaofaidika ni wawekezaji wageni ambao wanaenda kujenga nchi zao na watu wao na sisi Watanzania tunabaki kuwa maskini. Kwa hiyo, tungependa kujua kwa nini Waziri aharakishe kusaini huo Mkataba, ndio kinachotia wasiwasi pale ni kwa nini ameharakisha huo Mkataba?

Mheshimiwa Spika, kulikuwepo na uharaka gani wa kumchukua mwanasheria hapa amfuate kule London kwenda kusaini Mkataba, jambo ambalo rasilimali yetu najua ipo hapa nchini, tunajua kwamba madini yapo hata mwakani, thamani ya kitu inapanda siku baada ya siku, huwezi kuniambia kwamba leo madini pengine labda kilo Sh.5,000 kesho kutwa ije kuwa Sh.2,000, haiwezekani. Thamani ya shilingi inapanda, dola inapanda kila siku, tukiangalia mwaka jana na mwaka huu ni tofauti na hivyo hata thamani ya madini yetu inazidi kupanda. Kulikuwa hakuna ulazima huo, ndio maana inatia wasiwasi, kimesainiwa nini huko ndani?

Kwa hiyo, mimi kwenye hili naunga mkono, ninaomba Wabunge na wananchi ili waweze kuridhishwa na Mkataba huu uliosainiwa na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini katoa vielelezo akiwa kama ni mjibu hoja, mtoa hoja, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto naye atakuwa ametoa vielelezo vyake, basi vielelezo vyote viwekwe pamoja vipitiwe na hii Kamati Huru na kupitia huu Mkataba ili ijulikane kwamba, haki iko wapi na Watanzania wote tuweze kujiridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kasema kwamba, kazi ya kupitia Mikataba imekamilika Novemba, 2006, lakini ningependa kujua sisi Wabunge ambao tunawatetea wananchi na rasilimali za nchi hii kila siku, tunajadili kwamba Mikataba ipitiwe, tulijulishwa hilo? Hatujajulishwa na mpaka sasa hivi kama kweli Novemba, 2006 ilikuwa mwisho wa kupitia Mikataba, mabadiliko yaliyofanyika tunayajua mpaka sasa hivi kwa sababu ninavyofahamu hata hivi karibuni tu yamekamatwa makontena bandarini yanasafirisha mchanga wa madini, kwenda nje. Hili limetangazwa kwenye vyombo vya habari kila mmoja amesikia. Mchanga ule umeyeyuka kwa mazingira yasiyoeleweka. Yote haya tunasema ni kwa sababu ya Mikataba mibovu ya madini. Je, kama kweli imemaliza kupitiwa, mbona bado kuna kasoro nyingi sana?

Mheshimiwa Spika, mimi kwa hapa sina mengi, ninaomba sana iundwe Kamati Teule tuweze kujua kilichosainiwa kwenye huo Mkataba kwa kuanzia na huu Mkataba mmoja, pengine tutajua na mingine ambayo Serikali inaingia pasipo kujua nini kilichosainiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kushukuru kwa kunipa nafasi hii, asante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu na mimi nichangie hoja iliyoko mbele yetu, hoja ya mdogo wangu, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto. Kwanza siiungi mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilifuatilia mjadala uliokuwepo Bungeni siku ile Waziri anawasilisha Makadirio ya Wizara yake na yale mengine yote yaliyojiri siku ile. Kwa bahati nzuri, mimi nimekuwepo kwenye Wizara hiyo, lakini kwa bahati nzuri vilevile sheria hii imetungwa mimi nikiwa Naibu Waziri pale. Sasa nilipata hofu na kwa kweli nilikuwa nashawishika nimuunge Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto mkono kama Mkataba huu ungekuwa umesainiwa na Mheshimiwa William M. Ngeleja, kwa sababu kwa mujibu wa sheria hana *instruments* za kusaini Mkataba kama Naibu Waziri. Kwa sababu

hata mimi nilipokuwa Naibu Waziri, sikuwa na *instruments* za kusaini au kufuta chochote kwa mujibu wa sheria. Sasa nilikuwa napata hofu, pengine Mheshimiwa William M. Ngeleja ndio alisaini, nikafikiri pengine hilo ndio kosa, kumbe kosa ni Waziri kusaini Mkataba huu London. Waliotangulia kusema wameeleza na Mheshimiwa Waziri mwenyewe kaeleza, sababu zilizopelekea yeye na uharaka gani uliopelekea Mkataba ukasainiwa kwa wakati ule na huko ulikosainiwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lucy B. Msafiri, alipokuwa anazungumza hapa ametueleza tumekuwa nazo *video conference* nyingine zinaitwa *tele-conference,* mtu mmoja yuko Tokyo mwingine anaweza kuwa hata yuko kwetu Ujiji na mwingine akawa yuko London na mkutano ukaendelea (umeme upo Ujiji japokuwa wa kubabaisha) na mkutano ukaendelea na watu wakafikia uamuzi ambao waliukusudia au kukubaliana au kutokukubaliana. Sasa kwa Mheshimiwa Waziri, kusaini Mkataba London lilikuwa si tatizo, maudhui yaliyoko kwenye Mkataba na kwa bahati nzuri Mkataba huwa ni *document* ambayo mtu mwenye mashaka, anaweza akaipitia na akaisoma akaona upungufu uliopo kwenye Mkataba ule. Mimi nilidhani mdogo wangu, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, angeomba auone Mkataba ule kama una upungufu au hauna? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lingine lililoko kwenye hoja ambalo Mheshimiwa Waziri amelijibu vizuri ni suala la *Environmental Impact Assessment,* ambayo ni moja ya hoja ambayo Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, ameitoa hapa. Mheshimiwa Waziri, ameeleza vizuri kabisa kwamba, hatua hiyo inafikiwa wakati mtu kapewa *mining licence*, leseni ya kuchimba ambayo mpaka leo tunavyozungumza, Mheshimiwa Waziri kaeleza vizuri kwamba, leseni hiyo haijatolewa sasa haya mashaka ya *Environmental Impact Assessment* kwamba kibali kimetolewa, mashaka haya yanatoka wapi? Mheshimiwa Waziri, vilevile ameeleza, nashukuru sisi tumegawiwa maelezo yake hata kabla hatujatoka, kaeleza vizuri faida itakayotokana na kusaini Mkataba huo na vitu gani ambavyo kama alivyosema Mheshimiwa Adam K. A. Malima hapa ni vitu gani tungevikosa kama Mkataba huu ungechelewa kusainiwa.

Mimi nilidhani tungekuwa na kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa uharaka aliouchukua, kwa kuweza kutafakari kwa haraka kwa sababu angechelewa ndio unakuja ule usemi wa Kiswahili "chelewa chelewa utamkuta mtoto si wako." Sasa Mheshimiwa Waziri, hakutaka amkute mtoto si wake, aliona apeleke posa achumbie tayari apate mtoto huyo. *Document* hii ambayo Mheshimiwa Waziri ametupa hapa, ina vielelezo vyote, kuna viambatisho ambavyo Mheshimiwa Waziri, kafanya juhudi kaviweka ili kwa yeyote mwenye mashaka kwa yale ambayo Waziri mwenyewe ameyaeleza, kutetea yale aliyoyafanya, kujibu ambayo Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto ameyaeleza, aweze kupitia ili tutakapofika kwenye majumuisho, Bunge hili kama walivyotanabaisha wasemaji waliotangulia, lipate kuchukua uamuzi kwa sababu hoja hii si ya Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto tena, hoja hii ni hoja ya Bunge na Bunge ndilo lenye mamlaka ya kuamua hoja hii tuipeleke wapi. Kumekuwa kuna mashaka hapa, mtu amesimama anasema najua tayari tukisimama kupiga kura; unaanza vipi kuwa na mashaka kabla hatujafikia hatua hiyo? *(Makofi)*

Tunapoeleza kwamba, tunawatumikia Watanzania ni kweli, sisi wote hapa kwa pande zote tunawatumikia Watanzania. Katika kuwatumikia Watanzania hao, ndio maana naamini Mheshimiwa Waziri pengine ili kuandaa kujibu hoja hizi, hakupata usingizi na katika kuwatumikia Watanzania amejinyima usingizi ili awatumikie Watanzania, atoe majibu yaliyo sahihi. Kama hivyo ndivyo na ni kweli ndivyo ilivyo, haya aliyotoa Mheshimiwa Waziri, kwa maoni yangu na ninaamini ni kwa maoni ya wengi na hasa wale walionitangulia kuzungumza, yamekidhi na yamejibu hoja ambazo Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, ameeleza na kwa misingi hiyo, hakuna sababu ya kuunda Kamati Teule ya kuchunguza, kwa sababu unaanzisha Kamati kama Mheshimiwa Waziri asingekuwa ametoa majibu ya kujibu yale ambayo tuhuma zimetolewa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi sina ya ziada, ninaamini kabisa Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, atakuwa ameelewa, amefuatilia na Waswahili wanasema muungwana akivuliwa nguo anachutama. Asante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Manju S. O. Msambya, baada ya mazungumzo yake umeketi au umechutama? Namtania tu jirani yangu, yeye ni Kigoma Kaskazini na mimi ni Urambo Mashariki. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, bado ninao wachangiaji watano ambao tunao muda wa kuweza kuwasikiliza jioni. Nisisitize tu hapa, hoja hii ya Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, inajadiliwa sasa na Bunge. Ametoa maswali na hoja mbalimbali ndani ya ile hoja yake, kwa mujibu wa utaratibu wetu wa kanuni kuhusu masuala kama haya ya hoja binafsi, Waziri mhusika, Waziri wa Nishati na Madini, ametoa majibu na yamesambazwa. Ninawaomba nyie wa jioni, maana yake ndio tutafikia hatma ya kupiga kura, mjielekeze kwenye hayo yanayogawiwa. Mheshimiwa Phares K. Kabuye hajapata na ni mchangiaji, tafadhali yagawiwe, jioni tuna kazi ambayo wananchi wanaitazama hapa nayo ni kuamua kama yale maswali ya Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto yamejibiwa na kama yamejibiwa na Bunge itakuwa hatua ya Kamati Teule haina maana. Lakini kama mkiridhika hayajajibiwa, hapo ndio unaanza kuzungumzia sasa kuunda Kamati nyingine nje na nikumbushe tu Kamati Teule kwa mujibu wa Kanuni ya 105, Spika anaiunda kutoka miongoni mwa Wabunge. Kwa hiyo, sisi hawa hawa siyo kwamba utatafuta utaalamu mwingine ni Wabunge. Kwa hiyo, kama kwa umoja wetu tutaridhika kwa njia moja au nyingine, basi hatua inayofuata ni dhahiri kabisa, yaani kama tukiona majibu yanatosheleza tuna uamuzi na tukiona hayatoshelezi tuna uamuzi.

La pili, nilikuwa nakumbusha tu kwamba, vijana wetu hawa wanaogawa karatasi, *page boys and page girls* mara nyingine mnawapa vitu vingine ambavyo ni binafsi kabisa na kuwalazimisha kwenda mpaka kantini; picha, sijui vitu gani, sasa wanatakiwa wahudumie Shughuli za Bunge humu. Naomba sana, wakiyaona mambo yenyewe ni binafsi, kwa kweli nimeshawaambia wakimbie tu, waweke kwenye *pigeonholes* basi inatosha. Lakini kumfuata Mheshimiwa Mbunge mpaka kwenye Jengo la Utawala kwa karatasi ambayo ina mambo binafasi ni kudhoofisha huduma ndani ya Mkutano huu. Kwa hiyo Katibu wa Bunge asimamie na twende na utaratibu huo tu. Tuwape kazi ambazo zinaendeleza Shughuli za Bunge, badala ya hayo mengine ambayo hayahusiki.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo na muda uliosalia hautuwezeshi kumwita mchangiaji yeyote, sasa nasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni leo.

*(Saa 06.53 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka ziliposititishwa Shughuli za Bunge pale saa saba, nilikuwa bado ninao wazungumzaji watano. Nitaona kama wote wanaweza kupata muda, kwa sababu inabidi mtoa hoja hatimaye apate nafasi ili aweze kuhitimisha hoja yake. Mtoa hoja hayupo ana udhuru? Basi vyema.

Sasa ninao wafuatao, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Phares K. Kabuye, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir na Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu. Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed ameniletea ombi la kuchangia, tutaona kadri inavyokwenda, maana yake wengine wanachangia dakika tano, kumi wanamaliza, sasa inanishinda kuweza kutabiri kabisa.

Lakini kwa sasa namwita Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, wakati huo huo Mheshimiwa Phares K. Kabuye ajiandae.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami kuwa mmoja wa wachangiaji wa hoja iliyo mbele yetu mchana huu, ambayo imeanza toka asubuhi.

Awali ya yote, napenda nianze kwa kusema kwamba, baada ya majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kwa kweli nimeridhika kwamba, hakuna sababu ya Bunge hili kuunda Kamati Teule, kwa ajili ya kufuatilia mambo aliyoyasema mtoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya hoja za mtoa hoja ni kwamba, anadadisi kusainiwa mkataba nje ya nchi. Sasa suala hapa si kusaini mkataba nje ya nchi au ndani ya nchi, isipokuwa la msingi ambalo mtoa hoja angepaswa kutuambia ni kwamba, je, katika kufanya hivyo kuna sheria yoyote ya nchi iliyovunjwa? Kama hakuna sheria ya nchi iliyovunjwa kwa sababu mkataba umesainiwa nje au umesainiwa mahali popote, basi sioni kama kuna sababu ya kuendelea na malumbano juu ya jambo hili kwa ajili tu mkataba ulisainiwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kwamba, kwa nini mkataba huu ulisainiwa wakati zoezi la kudurusu mikataba iliyotangulia bado linaendelea. Kwanza ni vizuri tufahamu kwamba, Kampuni ya *Barrick* ni miongoni mwa makampuni yanazochimba madini hapa nchini na ambayo mikataba yao au mikataba yake ni miongoni mwa mikataba ambayo tayari Serikali inaidurusu. Kwa hiyo, kutokana na uzoefu ambao Serikali imepata wakati wa kudurusu mikataba mingine ya nyuma ya *Barrick* ni dhahiri

Serikali itatumia uzoefu huo au imetumia uzoefu huo katika kuingia mkataba huu wa maendeleo, yaani *Mining Development Agreement,* ambao ni mwanzo tu wa kuiwezesha kampuni hii ya *Barrick* kutengeneza *feasibility study, design* na mambo mengine yanayohusiana na mradi huo kabla ya kupata *mining licence* na kuanza kuchimba. Kwa maana hiyo, ni kwamba, utakapofika wakati wa kupata *licence* ya kuchimba, itatolewa hiyo *licence* pamoja na mkataba ambao utaonesha *terms and conditions* ambazo ni lazima *Barrick* azifuate katika utekelezaji wa mkataba huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la msingi hapa ni kwamba, Serikali yetu imefanya jambo zuri la kiungwana hata baada ya kufahamu kwamba kulikuwa na matatizo katika mikataba iliyotangulia, huo ambao ni sehemu ya majadiliano ya leo, hatukuivunja hivi hivi tu baada ya kufahamu kwamba ina matatizo na hatukuitengeneza vizuri. Tulifanya hivyo kwa kuzingatia jambo moja kubwa, pamoja na mengine kwamba, Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Kimataifa inayojulikana kama *Multiletaral Investment Guarantee Agency (MIGA).*

Ukishakuwa mwanachama wa *MIGA*, unawapa matumaini makubwa sana wawekezaji kutoka nje kwamba nchi hiyo ambayo ni mwanachama wa *MIGA* inafaa kwenda ku-*invest* kwa sababu hawawezi wakukufanyia mambo ya kihunihuni, hamuwezi kuingia mkataba leo kesho wakaubadilisha, haiwezekani. Kwa sababu tukifanya hivyo, tutakuwa tunajiharibia sura yetu mbele ya *international community* kuifanya Tanzania kama *destination* ya *investors*. Kwa hiyo, ndio maana tumezungumza nao hao wenye makampuni ambapo *Barrick* ni mojawapo ambayo yalitangulia katika kuwekeza katika eneo hili la madini.

Mheshimiwa Spika, eneo la *15%, interest on unredeemable capital,* hili nalo mtoa hoja amelivalia njuga na kusema kwamba ni tatizo. Sasa mimi kabla sijaendelea zaidi nilitaka nitumie fursa hii kulielezea Bunge letu Tukufu, kwa maana ya kuelimishana tu na kuliweka jambo hili wazi zaidi ni kwamba, kile kitendo tu kwamba hii 15% *interest on unredeemable capital* ilikuwepo kama *interest* juu ya *capital* ambayo haijakuwa *redeemed* ilikuwa ni kosa na gharama ya bure kwa Taifa letu. Kosa lenyewe lilikuwa linaifanya Taifa hili liendelee kulipia gharama za mwekezaji ambazo *initially* zilikuja hapa nchini au zinapaswa kuja hapa nchini kama mtaji *(equity).* Malipo au *reward* ya mtu anayeleta *equity* kama *risk capital* ni *dividends* sio *interest*. Hapo awali Serikali ilipokuwa imeweka kwamba kama katika mwaka wa kwanza na wakati ule kabla hatujafanya *review* ya mikataba, iliruhusu *recovery* ya 100% ya *capital* iliyokuwa *invested*.

Katika *review exercise* Serikali ikaona kwa kufanya hivyo, tungechelewa sana kuanza kupata faida kutoka kwenye miradi hii kwa sababu *depreciation* ya 100% ni kwamba unamfanya yule mwekezaji aliyeleta mtaji wake kwanza arudishe mtaji wake kwa asilimia 100, akishamaliza ndio tunaanza kufikiria na gharama nyingine. Serikali imelibadilisha hili na sasa chini ya taratibu ambazo Serikali imefanya, mwekezaji atakuwa amepewa ruhusa ya ku-*recover* 80% mwaka wa kwanza na 50% *subsequent years.* Dhamira ya kufanya hivyo ni kupunguza makato ya gharama ambayo kampuni iliyokuja kuchimba madini ili sehemu ya mapato yanayosalia baada *depreciation* yawe

makubwa zaidi kiasi cha kuliwezesha Taifa kuanza kufaidika kwa kupata *cooperate tax* kutoka kwenye Sekta ya Madini. Haya ndio yaliyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la *15% interest on unredeemable capital,* hoja ni hiyo hiyo, mantiki yake ni kwamba imeondolewa ile 15% kwenye *unredeemable capital* ili ile, *unredeemable capital* isizaliane tena kwa kutumia asilimia 15. Kwa sababu kadiri inavyoendelea kuzaliana ile *unredeemable capital* haitomalizika kulipwa. Kwa hiyo, siku zote sisi tutakuwa tunamlipa yule mchimba madini tu ndio maana imeondolewa. Kwa kufanya hivyo, mimi nilidhani mtoa hoja angeipongeza Serikali kwa kuja na utaratibu huu wa kuiondoa kabisa ile *15% interest on unredeemable capital. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yake ni kwamba, haikuja Bungeni ili iweze kuondolewa. Nyaraka za Waziri zimeonesha dhahiri kwamba, iliondolewa kwa kupitia Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwanza ni kitendo kizuri, kinamfanya mwekezaji wa nje aanze kulipa kodi mapema. Pili, kiliondolewa kwa kupitia Bunge lako Tukufu kwa kupitia *Acts* na *Financial Bills,* ambazo zilikuja humu kama tulivyooneshwa leo na miongoni mwa hizo tunazo hapa kama vielelezo. Kwa hiyo, hiyo nayo sio hoja ya kusema kwamba tuunde Kamati Teule ili tuweze kuitazama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea haya, nataka kusema kwamba, huyu *Barrick* ambaye ndiye amepewa mradi huu tunaouzungumza leo, yeye alikuwemo katika mazungumzo ya awali kwenye miradi ya nyuma. Kwa hiyo, Serikali imeshazungumza naye huyu na inafahamu matatizo, maeneo yenye matatizo katika mikataba *Barrick* anaelewa na Serikali inaelewa.

Kwa hiyo, tumeingia naye katika mkataba huu sote wawili tukiwa tunajua kwamba, hata kabla ya sheria mpya ya madini kuja tena na kupitishwa upya, maeneo yenye matatizo yamekwishaeleweka na kwa maana hiyo, huu Mradi wa Buzwagi nao umefaidika katika yale majadiliano yaliyokwishafanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo na kwa sababu muda wetu hautoshi wote kuendelea na haya majadiliano nadhani nitumie fursa hii kusema kwamba, baada ya kutoa hoja hizo sioni sababu za msingi za kukubali kuunda Kamati Teule ya Bunge kwa ajili ya suala hili, kwa sababu mtoa hoja ameshindwa kudhihirisha kwamba kweli aliyoyasema ni kweli na sisi kupitia Waziri wetu wa Nishati na Madini, amemjibu kikamilifu na kumuonesha kwamba hoja yake haina msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, asante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana. Msemaji wangu anayefuata hayupo kwa hiyo, ninamwita wa upande wa Upinzani, Mheshimiwa Phares K. Kabuye hayupo, kwa hiyo namwita Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, naunga mkono hoja mia juu ya mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, alichokifanya kwanza ametujulisha Watanzania kwa mara ya kwanza kwamba, kuna mkataba umesainiwa nje ya nchi ambao hatukuwa na taarifa nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hicho ni kitendo kimoja kizuri kwamba, taarifa ambayo Serikali haikutupatia, kwa kupitia kwake sasa Serikali imetupa taarifa rasmi. Namshukuru sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pili, nimekuwa naangalia maelezo ya Mheshimiwa Waziri, namshukuru sana na nampongeza sana yeye ni rafiki yangu sana lakini kuna moja ambalo amelisema kwamba bila ya utafiti basi hupaswi kuzungumza. Sasa ili ufanye utafiti lazima upate taarifa. Kwa mujibu wa Katiba kifungu cha 63 na Sheria ya *Immunities and Privileges Act*, kifungu cha kumi, kinatupa mamlaka sisi Wabunge kuomba nyaraka zozote Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe binafsi tarehe 17 Julai, 2007, nilimwandikia Waziri, Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, nikimwomba taarifa ya miaka mitatu ya Alex Stewart na nikanakili barua hii kwako na kwa Waziri Mkuu. Waziri Mkuu ndani ya Bunge hili alisema kwamba, Serikali haizuii nyaraka. Kwa taarifa yako Mheshimiwa Spika, mpaka leo hata barua kujibiwa sijajibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, alimwandikia Waziri akiomba apatiwe Mkataba wa Buzwagi tarehe 17 Julai, 2007 lakini Mkataba huo hakupewa mpaka leo. Sasa, hivi Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, afanye vipi *research* wakati umemnyima nyaraka, wakati sheria na Katiba ya nchi inamruhusu Mheshimiwa Mbunge yeyote kupata nyaraka hizo? Sasa mnaweza kutulaumu kwamba hatufanyi utafiti ni kweli utafiti tunaofanya ni finyu kwa sababu Serikali inatunyima nyaraka na tunazidai kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini tunaomba sasa Kamati Teule iundwe? Pengine kwa kupitia Kamati Teule, hizi nyaraka zitapatikana na sisi tuna *experience* na hiyo. Tuliunda Kamati Ndogo ya *PAC* tukapata nyaraka ya *Williamson Diamond,* lakini kwa njia ya kawaida ndani ya Bunge hili ilishindikana kupata nyaraka. Kwa sababu hiyo, tunauona kabisa umuhimu wa kupata nyaraka na hasa huu Mkataba uliosainiwa nje ya Tanzania, upatikane uje hapa tuone ukoje na tutaupata kwa kupitia Kamati Teule. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, katika majibu ya Mheshimiwa Waziri, ameeleza manufaa ambayo tutayapata baada ya kusainiwa Mkataba huu na mradi huu utakapokuwa umeanza. Kwa taarifa tulizonazo sisi hapa alizotupa Waziri kwamba, mradi huu ni mdogo sana unatoa *ounce* 1.8 kwa tani moja ya mchanga, lakini kampuni hii imewekeza kwenye mradi unaotoa *ounce* 12 kwa tani. *Experience* tuliyonayo sisi, *Williamson* kila siku walikuwa wanasema hawapati faida, lakini wanaendelea kuwekeza. Waziri katika maelezo yake humu anasema faida tutakayopata ni dola 198 milioni. Ukiangalia kitabu cha *revenue* kwa Wizara hii kwa miaka mitatu, mapato yaliyopatikana ni 77 bilioni. Sasa

unajiuliza hizi 198 milioni zinazosemwa baada ya mradi huu kuwekezwa, zitatoka wapi ikiwa mradi utakaowekezwa unatoa 1.8 *ounce* kwa tani moja hizi 198 bilioni zitapatikanaje? Haya ni maswali yanayotakiwa kujibiwa ndani ya Kamati na si mahali pengine popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema pamoja na majibu haya ya Mheshimiwa Waziri, bado kuna maswali 100 unaweza kujiuliza. Tunaambiwa juu ya uwezekano wa kupata ajira 600 kwa mradi mdogo huo; mradi mkubwa je, unatoa ajira ya watu wangapi? Maana inatakiwa unapoleta maelezo, lazima ulete na takwimu za ulinganisho zinazosema kwa mradi huu mkubwa basi tumepata ajira hizi na kwa mradi huu mdogo tutapata ajira hizi, ndio itatusaidia. Sasa ni Kamati tu itakayotusaidia kutupatia majibu haya, hivi hivi hatuwezi kupata majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine tumeambiwa kwamba, faida tutakayopata ni kubwa sana, dola 568 kwa ajili ya miundombinu na kadhalika, lakini hatuelezwi kilomita ngapi zitajengwa, hatuelezwi *megawatt* ngapi za umeme na kadhalika. Kwa hiyo, kuna masuala mengi tu hii Kamati Teule ikiundwa ndio itapata majibu kama haya ni sahihi au siyo. Kwa hiyo, sitaki kusema Mheshimiwa Waziri hakusema sawasawa, lakini nasema bado kuna utata wa taarifa. Kama taarifa ya Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto ina utata, hii ina utata zaidi maana yake ina *figures* ambazo lazima u-*clarify* kwamba ni *figures* sahihi zilizoletwa hapa. Bila kutushawishi sisi na kusema tu kwa juu juu kwamba, kuna manufaa wakati *experience* yetu ya madini, ukisoma taarifa zote za Bunge hili, za Wabunge, za Kamati za Bunge, wanalalamika mapato yanayopatikana kutokana na madini. Sasa kama leo tutapata manufaa makubwa kwa mradi mdogo tu *Mini- tiger,* naambiwa basi itakuwa faida kubwa sana, tutashukuru sana sisi lakini nasema hayo majibu yatatoka kwenye Kamati Teule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika viambatanisho vya Waziri, ameleta barua iliyoandikwa na Kamati iliyomshauri. Kamati inasema: "Hivyo, Kamati inapendekeza ni vyema Mkataba huu usainiwe kwa mfumo wa kodi uliopo ili kuwezesha mgodi huu uanze kufanya kazi."

Huku tunaambiwa kuna *review* mpya imefanyika ya mikataba lakini kauli zinakuwa tofauti, Kamati inasema isainiwe kwa mfumo wa zamani, *contradiction,* Mheshimiwa Spika ni kitendawili kabisa kabisa. Sisi wenzenu jamani bahati mbaya tunaambiwa hatuna uzoefu, lakini nasema mtusaidie huu utata unapotokea tunahitaji hizi *information* zitusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, ninaomba Serikali itusaidie *best practice* ni Serikali kusaini Mikataba nje ya nchi? Serikali itueleze Mikataba mingapi ya madini imesaini nje ya nchi? Itueleze kama ndio *best practice* kwamba, Serikali ina uharaka wa kusaini Mikataba na kampuni siyo Serikali na Serikali, Serikali na kampuni kwamba *best practice* ni kusaini Mikataba huko nje ya nchi kwa sababu tu mgodi huo eti unawezekana usiwe na *market* baadaye? Hivi dhahabu kubaki pale kwenye ardhi kwani Watanzania wana hasara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo ndio *argument,* pale mapema tuliposema juu ya habari ya Mwalimu pamoja na kwamba tunaambiwa tunam-*quote* vibaya, lakini nafikiri tuna-m-*quote* vizuri tu kwamba, aliona Watanzania bado hatujaweza kukamata rasilimali hii ya madini, tujielimishe basi angalau. Serikali hii inasema sasa tumechangamka tunafahamu, ndio maana tumekubali, lakini Serikali hii hii ndio ina-*review* Mikataba kwamba haikufanya vizuri! Kwa hiyo, ile dhana ya kwamba tumeelimika juu ya jambo hili sio kweli, kama tungeelimika tusingeingia kwenye Mikataba yenye makosa. Hatujaelimika na tumeambiwa ndani ya Bunge hili hili kwamba, mambo haya yanahitaji utaalamu mkubwa na kadhalika. Kwa hiyo sisi tuka-*caution* katika Bunge hili ni vizuri Serikali ikawa waangalifu katika suala zima la kuingia kwenye Mikataba. Leo tunakwenda kusaini Mkataba nje ya nchi, *perception* tu sitaki kusema kuna kasoro ni *perception* kwa madhambi haya yaliyoko tayari kwenye madini, unakwenda kusaini Mkataba nje ya nchi wala hutoi taarifa kwa wananchi, taarifa imetoka baada ya Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto kuibua hoja. Naomba sana Watanzania wenzangu, tuiunge mkono hoja hii, tuunde Kamati Teule itusaidie kwa sababu tutaibua mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, alituahidi niliomba taarifa mbili ya Alex Stewart na Ripoti ya Dr. Kipokola na akaahidi ndani ya Bunge hili hili kwamba atatupa, mmepata Waheshimiwa Wabunge? *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Bado! *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Halafu tunaambiwa hatufanyi utafiti; utafiti gani tufanye sasa na vitabu hamtaki kutupa? Taarifa hamtaki kutupa sasa tufanye utafiti gani? Kwa hiyo, tutakachofanya, tutaambulia hizi hizi mnazotupa hapa tutafanya nazo kazi, basi hatuna nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wengine wamesema ooh! kuna *internet* siku hizi na nini! Hapana Mikataba hii ya madini hairuhusiwi kusainiwa kwenye *internet,* mkatazame sheria vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na naomba kabisa Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwasaidia Watanzania wetu hawa tukubali kabisa tuunde Kamati Teule ya Bunge. *Experience* tuliyoiona sisi tulipounda Kamati Ndogo ya *Public Accounts Committee,* tumegundua mambo mengi sana toka mwaka 1994 Mkataba umesainiwa mpaka leo kampuni husika haijalipa kodi ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa nauliza swali la nyongeza kuhusu *Williamson,* Mheshimiwa Waziri akasema pale *Williamson* kuna mambo mazito pale huwezi kuingia ovyo ovyo, sisi tulikwenda na Kamati yetu na Wabunge wengine wako hapa tumekwenda mpaka kwenye hicho chumba, unaambiwa huingii tumeingia na tukatia mkono tukakamata almasi. Mimi nikauliza ninyi mnasema mtu haingii humu mbona sisi Wabunge mmeturuhusu kuingia na tumechukua almasi tukatazama? Pamoja na kwamba Serikali ina hisa, hakuna Mtanzania yeyote pale ni wao wenyewe wageni watupu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekwenda London, *Valuer* aliyewekwa na Serikali kutathmini almasi zetu, tulipomwambia *Williamson* haijalipa kodi yule Mchecoslovakia alianguka chini, akasema siamini huku Serikali inasema inafuatilia kwa undani na kadhalika! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, kwa maslahi ya Taifa hili, tuungane na Mheshimiwa Rais, kwa kauli yake aliyoitoa ya kupitia Mikataba hii kwa kusaidiana na Wabunge. Tuliiambia Serikali peke yenu kazi hii hamtoiweza lazima mlishirikishe Bunge na njia ya kulishirikisha Bunge ni kuunda Kamati Teule, tutapata mambo mengi ndani yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja binafsi ya Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto.

Mheshimiwa Spika, yaliyopo mbele yetu hapa ni mambo mawili tu. Moja la msingi ni tuhuma ambayo aliitoa Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, tarehe 16 Julai, 2007, ambayo ningependa ninukuu katika *Hansard* ukurasa 181 alisema hivi: "Mheshimiwa Spika, kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri, kuhusiana na Mkataba mpya wa Mgodi wa Buzwagi, ambao Mheshimiwa Waziri ameeleza maelezo ambayo sio sahihi, amedanganya na ameeleza vitu ambavyo kwa kweli sivyo ambavyo vipo katika Mkataba ambao ameusaini."

Mheshimiwa Spika, hii ndio hoja ya msingi. Kwa Mkataba ambao ameuona yeye, hayo yaliyosemwa na Waziri sivyo ilivyomo mle. Sasa mnataka taarifa gani na Mkataba anao na amesema aliyoyaona yeye mle sio aliyosaini Waziri? Mnatafuta taarifa gani tena? Kwa hiyo, Mkataba huu alikuwa nao ndio maana akaweza kufananisha kwamba, yaliyosemwa na Waziri siyo yaliyomo mle, hii ndio hoja ya msingi kudanganya. Sasa hii habari ya Kamati Teule ilikuwa ni mtoto wa hoja ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunazungumza habari ya Kamati Teule, tunaacha hoja ya msingi iliyotukusanyisha hapa leo kwamba, Waziri alidanganya. Waziri asubuhi ametoa majibu, tulitarajia wanaounga mkono hoja hii waeleze basi katika yale majibu ya Waziri la uongo lipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna ubishi kwamba, Ibara ya 8 ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inatoa mamlaka ya msingi kabisa ya Serikali kuwa ni wananchi. Hapana ubishi vilevile kwamba mamlaka haya ya wananchi…

**MHE. KABWE ZUBERI ZITTO:** Mheshimiwa Spika - kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto - kuhusu uratibu.

**MHE. KABWE ZUBERI ZITTO:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 43(7), "Mbunge yeyote hataruhusiwa kufufua jambo lolote ambalo Bunge lilikwishakuamua ama katika mkutano huo uliopo au ule uliotangulia."

Mheshimiwa Spika, hoja iliyopo Mezani kwako ni hoja yangu ambayo nimeisoma hapa na sio hoja iliyotolewa tarehe 16 Julai, 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba utupe utaratibu ili Wabunge wachangie hoja ambayo nimeitoa Mezani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Wabunge, hoja aliyoitoa Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, iliyo mbele yetu sasa ina chimbuko lake, hata yeye mwenyewe ukisoma katika hoja yake inaanzia kule kule. Kwa hiyo leo hawezi kusema ameleta hoja mpya kabisa, ambayo haina msingi wa nyuma na wakati wote ananukuu maneno aliyosema Waziri. Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed naye amesimama hapa, wote wananukuu yaliyosemwa na Waziri, basi pande zote zina haki ya kuanzia kwenye mzizi mpaka tufike mwisho kwenye matawi. *(Makofi)*

Endelea Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ukiona Mpinzani wako hafurahishwi na jambo lako, usiliachie ukiona anafurahiwa nalo hilo baya liache mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri vilevile kwamba, hakuna ubishi kwamba mamlaka ya wananchi waliyopewa katika Katiba Ibara ya 8, kwa kiasi kikubwa yanapitia kwetu sisi Wabunge wao.

Sina ubishi vilevile kwamba, Ibara ya 100 ya Katiba inatupa Wabunge uwezo wa kutoa maoni yetu, kujadili kwa ukubwa kabisa, lakini ninapenda tukumbushane kuwa uhuru huo tunaopewa na Ibara ya 100 ya Katiba siyo uhuru holela. Bunge haliwezi kugeuzwa kuwa kijiwe cha mambo ya hisia, majungu na kupakana matope. Huu siyo uhuru wa kukiuka haki na wajibu kama vinavyoainishwa katika Ibara ya 12 – 30 ya Katiba. Uhuru usiokuwa na mipaka siku zote ni kuingilia uhuru wa mtu mwingine. *(Makofi)*

Nimesikia hoja ya Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto leo, nimesikia na majibu ya Mheshimiwa Waziri, kwa maoni yangu ushahidi uliotolewa na Mheshimiwa Waziri hapa kujibu hoja 11 za Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, unaonesha kabisa bila wasiwasi kwamba, tuhuma za Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto zilikuwa ni hoja hewa. *(Makofi)*

Zimechukuliwa zilikochukuliwa tuhuma hizo zikaingizwa Bungeni, bila kufanyiwa uchunguzi wa ukweli na usahihi wake. Alipoitoa hoja hii tarehe 16 Julai, 2007 tulimsikiliza na kweli wengi tulisisimkwa kwamba, Waziri wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, anathubutu kufanya ufisadi wa namna ile. Tulimpa *benefit of doubt,* pengine alikuwa na hoja za kwelikweli na angeweza kuleta ushahidi kwa tuhuma hizi na siku hiyo ni leo. Ndiyo maana hata siku ile hatukumpiga *stop* kwa kutumia kifungu cha 50(1), maana *benefit of doubt* ilikuwa ni haki yake ya msingi.

Mheshimiwa Spika, leo ni mwezi mzima toka Mheshimiwa atoe tuhuma hizi dhidi ya Mheshimiwa Nazir M. Karamagi. Kipindi chote hiki wananchi wamekuwa wakisikia na kusoma kwenye vyombo vya habari, juu ya matope haya, Waziri wa Nishati na Madini kwamba si muadilifu, si msafi. Kwa kushindwa kuthibitisha tuhuma zake leo, ndugu yangu, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, amemvunjia heshima, kamvunjia sifa, kamvunjia na hadhi Waziri wa Nishati na Madini.

Haya yangesemwa nje ya Bunge, hapana shaka kuwa ingekuwa ni kesi nzuri sana ya *defamation* Mahakamani, kwa bahati mbaya haya yamesemwa Bungeni, ambapo Kanuni zetu hazimruhusu Mheshimiwa Naziri M. Karamagi, kudai fidia.

Mheshimiwa Spika, ni Bunge lenyewe tu ndiyo lenye Mamlaka ya kuona hatua ipi ichukuliwe, baada ya mjadala huu kuisha na lazima hatua zichukuliwe ili mchezo wa aina hii wa mtu kukusanya taarifa nje kuzileta humu ndani, ukome mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *Shakespere* anasema katika *Othelo* na ninaomba kumnukuu: "Jina zuri kwa mwanamke na mwanamume ni Johari, ni tunu. Anayeniibia mkoba wangu wa fedha anaiba takataka, lakini anayeninyang'anya jina langu lililo zuri ananifilisi kabisa."

Mheshimiwa Spika, mimi namthamini sana ndugu yangu, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, bali ninaithamini sana heshima ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukiukwaji huu wa Kanuni ya 50(1) ya kumsemea mwenzake uongo, ya kumpaka matope, nahisi aliyedanganya ni huyu mtoa hoja kuliko yule aliyebambikiwa tuhuma hizi na kwa msingi huo, utanielekeza kama nitakuwa nakosea. Ninaomba mimi nitumie Kanuni ya 59(3) kwamba, kwa tabia hii ambayo imefanywa na ndugu yetu, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, asimamishwe kazi ya Ubunge kuanzia leo na Mkutano wote wa Tisa unaokuja, tukutane naye hapa Bunge la Januari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mwenzetu Mheshimiwa Mudhihiri M. Mudhihiri amewahi mno, kwanza wachangiaji bado wapo, hatuna haraka jambo ni kubwa na zito, twende bila papara, bila jazba na twende vizuri tu tutafika, maana bado wasemaji ninao na ni wasemaji wazuri, mtawasikia mtafika mahali ambapo inafaa kuona tunafanya nini kabla sijamwita mtoa hoja.

Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Phares. Kabuye, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter J. Serukamba.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Mimi kama mwalimu, utaniwia radhi nianze na utangulizi.

Ndugu zangu, mambo ya madini ni mambo ya kuangalia sana na waliofanya mchezo leo hii wanalia. Afrika ya Kusini imeboresha miundombinu kwa sababu dhahabu zote na almasi zimechimbwa na wale Wazungu waliojiita wenyeji, zikatengeneza nchi. Leo hii *Rand* yao ni sawasawa na dola saba hadi sita. Ghana ambao almasi zao na dhahabu zilipelekwa na watu wa nje kama tunavyofanya leo hii *Sen* ya Ghana 9000 ndiyo sawasawa na dola, muiangalie sana. Kongo nao mali yao imepelekwa. Nimezaliwa nasikia kwamba kuna Mgodi Geita sisi tunaita *Keita, akasezia Keita bandu.* Leo hii Wananchi wa Geita ndiyo wanaoambiwa kwamba, wana hali mbaya za kimaisha. *(Makofi)*

Mali tuliyopewa na Mwenyezi Mungu, lazima tuisimamie na wananchi wana matumaini na Bunge hili, hawana popote pale pa kwenda. *(Makofi)*

Sasa naanza, ni kweli kabisa kusaini Mkataba wa Dhahabu, dhahabu kuisainia London una mashaka. Hivi alikuwa anatembea nchi za nje alikwenda na Mkataba huo? Gharama iliyotumika kupeleka Mkataba huo nani aliyeilipa? Hivi kweli tumefikia hali ya kwenda kubembeleza wawekezaji kwa dhahabu na almasi? Bwana Mkubwa anasema Waziri wa Tanzania lete Mkataba hapa, unakimbia! Nasema tuunde Kamati, kuna wasiwasi hapa kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunagawa mali, tunabembeleza njoo tukugawie mali? Hakuna haraka, ninafahamu kabisa mgodi huo ulianza zamani, hawahawa walikuwa wameanza eti wamewapa tarehe mwezi wa tatu ndiyo mgodi ulikuwa umeanza wameanza mambo mengi, ulikuwa unatakiwa kufunguliwa wasingeacha hiyo mali tu. Kwa hiyo, wasiwasi wa kwenda kusaini London ulitokana na Waziri na wala siyo wawekezaji walikuwa wameshawekeza pesa nyingi wasingeacha. Sasa wanakimbiakimbia London, kwa nini saini isisainiwe Kahama na ndugu yangu, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba wakaangalia, lakini London? Kuna kitu hapo, ndiyo Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto anasema Kamati Teule iende ikaangalie kisa cha kwenda London. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *Barrick* mimi ninaufahamu mgodi wa Tulawaka umekwisha ile *open cutting* imekwisha sasa wanafanya *underground* wana haja ya kutafuta migodi hawawezi kukupa kwamba tarehe fulani usipokuja hatuwezi kufungua migodi, haiwezekani haya ni mambo ya kufumba tu. Taratibu zilifuatwa kama zilifuatwa angalieni kile kibali kilichotolewa na Mwanasheria Mkuu halafu angalieni na yale Maazimio ya Halmashauri inayoshauri Madini ni tarehe 1, tarehe 16/02 wote kweli walikuwa wanakimbia.

Mheshimiwa ulikuwa na haraka kweli hapana! sijui mlifanyaje, tarehe 16 wote, Mwanasheria Mkuu ameandika harakaharaka kikao kikakaa hapana! Kwa kweli ulikuwa na haraka na hicho kitu kilichokuwa kinakufanya haraka, kipo ndicho tunachotaka Kamati iende ikajue, haraka ya nini? *(Makofi)*

Angalieni tarehe moja hiyo sijui walifanyaje hayo mambo, kwa nini tusiwe na wasiwasi, wananchi waliotuleta hapa tuwe na wasiwasi kwa niaba yao; haraka ya nini hiyo? Siku moja angalieni.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ukiangalia ushauri wanasema kabisa kwamba, wafanye kabla ya mfumo wa Kodi kuboreshwa, aliruhusiwa kabla ya mfumo wa Kodi kuboreshwa asaini. Hivi kweli wewe unasimamia madini yetu ndugu yangu? Kabla ya mfumo wa kodi kuboreshwa? Jamani someni, amesaini kabla ya mfumo wa kodi kuboreshwa ndiyo anatuambia ulikuwa umeboreshwa labda baada ya kusaini alikaa sana baada ya ushauri.

Lakini pia anasema kwamba, wale wanaohusiana na mkakati wa kupitia Mikataba ya Madini kama angesubiri wao walihitaji muda mrefu. Kwa hiyo, alifanya kabla ya mkakati wa kupitia Mikataba ya Madini haujafanyika, ile inaitwa *GNT* ilikuwa haijakaa kujadiliana. Sasa anasema utaratibu ulifuatwa, hakuna upungufu haya si mapungufu ndugu yangu? Si mapungufu haya? Mfumo wa kodi haujaboreshwa, Mikataba haijapitiwa, sasa unasema hakuna upungufu; upungufu unataka uweje, uangushe Mbingu? Akaambiwa atumie mfumo uliopo, ule wa zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tuangalie haya ya kudanganywa wakati ile ya kumshauri ilipokaa yeye ndiye alikwenda kuwashawishi kwamba, soma kawaambie kwamba hiki kitu kina faida mnishauri haraka pitisheni, someni ushauri wao. Wanasema yeye ndiye aliyetoa hoja, siwezi kusema kuwa alishinikiza maana nitatakiwa kuthibitisha. Ndiyo walishauri wao alikuwepo anawaambia huu mgodi una faida wanasema wenyewe kwamba, baada ya kuhakikishiwa kwamba, mgodi una faida na mgodi mdogo una faida kuliko Tulawaka. Mambo haya ndiyo Kamati Teule inataka iangalie, hiyo faida inayosemwa, mimi ninao Mgodi wa Pangea, Tulawaka. Tumehangaika na wananchi kujenga shule, Mheshimiwa Waziri Mkuu amepata dosari kwamba, aliamrisha watu tuwapige wajenge shule, hivi migodi tuliyonayo yote mbona haikuleta pesa za kujenga shule? Huu mgodi mdogo ndio utakaoikomboa Tanzania? Lazima tuangalie. *(Makofi)*

Tumejenga Zahanati, lazima wananchi twende kuwahangaisha, migodi tunayo mingi huu mgodi ndio utakaoleta neema? Nina mashaka na wasiwasi, yaani *Question Mark*? Hii *Question Mark* inahitaji Kamati iende ikatafute ituletee sasa jawabu tusije tukaambiwa ambiwa tu mambo, watu wakaanza kuja kuchukua madini na wanachukua. Kama kweli wangesema mwekezaji wa kuja kupeleka muhogo wa Mtwara, hapo tungekimbia kumtafuta. Lakini dhahabu? Dhahabu? Unakwenda kumbembeleza mpaka ndiyo unakwenda London? S

Sasa Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto akiwa na wasiwasi ni matatizo, wewe huwezi kuwa na wasiwasi kama Mtanzania? Huwezi kuwa na wasiwasi juu ya haya?

Kama mtu anasema Mheshimiwa Phares K. Kabuye, nyumbani kwako kuna kitu cha wizi; mimi nikisema usije kusachi hivi kweli hakuna mashaka?

**WABUNGE FULANI:** Yapo!

**MHE. PHARES KASHEMEZA KABUYE:** Hivi kweli Kamati inaogopa? Huna tatizo lolote, nenda uje utukejeli Kamati iseme hakuna kitu tulidanganya mjisifu, sasa unaogopa nini ndugu yangu na Serikali yetu tukufu?

Mheshimiwa Spika, uko wapi Utawala Bora sasa? Uko wapi uwazi wa Serikali yetu? Toa Kamati ije, mtusimange hapa Kamati iseme hakuna kitu ni uzushi, sasa wewe uzushi unauota wewe mchangiaji hapa umefanya utafiti mpaka unasema ni uzushi; ni uzushi gani? Tuhuma inaamuliwa na Mahakama, sasa ni tuhuma tutengeneze Kamati ambayo itakwenda ndani.

Mimi huo Mkataba sijauona lakini hii Kamati itauona na mtu anasema tena Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto alikuwa nao; hivi Serikali yetu imeshatangaza kwamba imeibiwa nyaraka? Walipata wapi huo Mkataba? Mheshimiwa Waziri, umeibiwa nyaraka bwana; walipata wapi sasa? Ni lazima tuangalie. *(Makofi)*

Mimi nilikuja nimeaga kwa kufa na kupona kwa ajili ya wananchi, mkiona nimefunga virago nimefukuzwa Ubunge, msishangae ni kwa ajili yenu.

Kwa hayo machache, naunga mkono asilimia elfu kumi, asante sana. *(Kicheko/ Makofi)*

**SPIKA:** Bado nawasihi Waheshimiwa Wabunge twende kwenye hoja, kuna hoja imetolewa na Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, majibu yametoka sasa mchango kama wa Mheshimiwa Phares K. Kabuye unafurahisha, lakini hauingii katika maudhui, hauingii kabisa katika maudhui ya hoja. *(Makofi)*

Kama hoja itakuwa kwamba tusipouona Mkataba wowote tunaunda Kamati Teule, itakuwa ni Bunge la kitoto kabisa. Kwa hiyo, suala hapa siyo kuona Mkataba lakini pima majibu ya Waziri kama yanatosheleza, hiyo ndiyo hoja yenyewe.

Msemaji anayefuata ni Mheshimiwa Peter J. Serukamba, wakati huo huo na Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, ajiandae.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nami nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango kwa hoja iliyo mbele yetu.

Kwanza, nianze kwa kusema hoja hii siiungi mkono kabisa, lakini jambo la pili nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake mazuri sana. Ni majibu ambayo hakuishia kwenye kueleza, ameweka na viambatanisho. *(Makofi)*

Lakini ukiangalia mtoa hoja katika hoja zake ana mambo makuu mawili, ambayo yeye ndiyo anataka leo tuyajadili. Anasema na nitaomba nimnukuu: "Kusainiwa kwa Mkataba Mpya wa Madini wa Mgodi wa Mradi wa Buzwagi kati ya Serikali na Kampuni ya *Barrick.* Sababu za mkataba huo kusainiwa nje ya nchi, yaani London Uingereza na wakati unasainiwa na wakati *review* zinaendelea na kuondolewa kipengele cha *15%, capital allowance on redeemable qualifying capital expenditure* bila kibali cha Bunge lako Tukufu."

Majawabu haya na hoja zake zimejibiwa vizuri sana na Mheshimiwa Waziri, lakini yapo mambo kwanza Rais wetu aliagiza *review* zifanyike, *review* zimefanyika, *Barrick* ndiyo watu wa kwanza waliokubali wakafanya hizo *review* na wakasaini *MDAs.* Kwa kweli *concerns* za Rais zimetekelezwa katika hii *MDA* mpya na *new understanding* ambayo ipo sasa kati ya *Barrick* na Tanzania ni kulingana na tulivyo-*negotiate* na hili mimi lazima nimpongeze Waziri na niipongeze Serikali na niwapongeze wenye makampuni ya madini yote, kukubali kufanya *review* na masharti tuliyosaini Mkataba ni kwa kufuata masharti mapya.

Lakini linakuja suala la pili ambalo ni la msingi mkubwa wa hoja yake, yaani Mkataba kusainiwa London. Nimewasikiliza wote hasa rafiki zangu wa upande wa Upinzani, wanaounga mkono hoja hii, hakuna hata mmoja ambaye amesimama akatuambia ni sheria namba ngapi ya nchi hii ilivunjwa kwa kusaini Mkataba London? Hayupo hata mmoja aliyetuambia kwamba, kwa kusaini Sheria ya Nchi imevunjwa, nani asimame hapa atuambie?

Lakini cha muhimu hapa, jamani kilichofanyika London ni *ceremony* tu lakini *negotiations* zote za Mkataba huu zimefanyika Tanzania, Kamati zote zimekaa Tanzania, Mkataba ukaandaliwa Tanzania, lakini Waziri wetu ndiye mwenye Mamlaka na ndiye mwenye *instrument* ya kusaini mwisho wa siku imemkuta kila kitu kiko tayari, *already* yuko safarini kwa sababu tuna ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya, akasema lete nisaini. *(Makofi)*

Sasa ni Mikataba mingapi sijui wenzetu watuambie, tumesaini nje ya nchi mbona hawajalalamika?

Mheshimiwa Spika, lakini pia ninachotaka kusema ni kwamba, wanasema Buzwagi ni *Marginal Mining*, mimi nasema Buzwagi ni *Marginal Mining* kwa sababu *deposits* zake ni kidogo sana, lakini kwa sababu tumefanya *review* mgodi huu utatusaidia na Waziri ametuambia hapa kwamba, tutapata dola za Kimarekeni milioni 818.3. Kuna mtu amesema hapa atuambie hela hizo zitafanya kazi gani, lakini ni suala la hesabu tu, akiamua sasa atajua ni kiasi gani zitafanya kwa maendeleo ya nchi yetu, akiamua tupige hesabu inawezekana tu. *(Makofi)*

Lakini pia tunakuja suala la 15%, 15% hii ya hili *redeemable* kwa *capital allowance*, ndugu zangu hebu tulielewe hili jambo maana yake nini?

Waziri ametoa majawabu yake hapa, lakini akaenda mbali zaidi, ametupa na sheria na watu wote waliosimama hapa ambao ni Wapinzani, sikumwona hata mmoja ambaye ana-*question* hii sheria tuliyoipitisha kwenye Bunge hili. Matokeo yake tunakwenda kuchagua sentensi moja wana-*capitalize on that*, tunayo Sheria hapa nani ameikataa?

Tuliipitisha hapa na Waziri amesema kwa bahati mbaya Mheshimiwa Mbunge, hakuelewa kwamba, kuna Sheria ya Madini na kuna Sheria ya *Income Tax Act* ya mwaka 1973. Tunachokiongelea hapa ni sheria ya mwaka 1973, siyo Sheria ya Madini, *unless* watu hatuelewani vizuri. Lakini katika hili huyu bwana amejichanganya. *(Makofi)*

Lakini lililofanyika ni haya yafutayo: Kwanza, hiyo *capital allowance and redeemable qualifying capital expenditure* haimo katika Sheria ya Madini lakini hii imerudishwa kwenye *MDAs* zote, maana yake ni kwamba, sasa Serikali yetu ita-*benefit* kwa hiki kipengele kuondoka *unless* watu waniambie kwamba, hawataki Serikali yetu i-*benefit*. Kama mtu alikuwa umempa *allowance relief* ya 15%, leo unaiondoa maana yake wewe unafaidi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, katika hili mimi ninachosema, kilichofanyika hapa kwanza ni kumpongeza Waziri kwa kuhakikisha hii *relief* ya 15% inaondoka.

Mheshimiwa Spika, kuna mtu alikuwa anaongea hoja hapa kwamba, madini yana bei kubwa sana duniani hatupaswi kuyaa……

Lakini ngojeni niwaambieni *Gold Price* duniani ina-*fluctuate.* Nataka niwaeleze ni kwa nini *essence* ya kusaini Mkataba huu ilikuwa ni muhimu sana. Sasa hivi baada ya Septemba 11 na Afghanistan, *Iraq War* na *terrorism,* bei ya *gold* ndiyo ikapanda, kwa hiyo, kukishatokea *instability* kwenye *global scale* ile bei ya *gold* inapanda. Kwa hiyo, *economies of scale* ambazo huyu bwana alikuwa anatuambia ukiangalia Buzwagi tunapata 1.8 *gram,* katika tani moja kwa vyovyote mtu kama ingekuwa *price ya Gold* haiko juu, hakuna ambaye angesaini Mkataba huo. Lakini leo bei ya *gold* ni kubwa sana duniani kwenye *financial markets* zote duniani, *stocks* ambazo ni *expensive* ni *stocks* za *gold* katika hali ambayo kuna *instability* duniani na ndiyo maana *investors* wote wanakwenda kwenye hii wanayoiita ni *self of heaven,* yaani *gold* ni *self of heaven*.

Kwa hiyo, ninachotaka kusema, tulicho-*benefit* kutokana na Mradi wa Buzwagi ni kikubwa sana kama nchi. Sasa mimi najiuliza hivi tunataka tuunde *Selective Committee* ifanye kazi gani? Yameulizwa maswali, yamejibiwa tena siyo kujibiwa peke yake na viambatanisho, lakini bado mtu hataki anataka nini sasa? *(Makofi)*

Wenyewe mmesema asubuhi hapa kwamba, tuondoke kwenye suala la siasa na mimi nasema tuondoke huko twende kwenye ukweli. Waziri amejibu maswali na ameweka na ukweli sasa tunataka Kamati ya nini na ifanye kazi gani?

Mheshimiwa Spika, Bunge lako hili hatuwezi kufanya kazi za mtu akikaa akifikiri jambo analitengeneza sisi tunalibariki tu, haiwezekani! Haiwezekani tuipake matope Serikali inayoafanya kazi kubwa namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba kwa hoja alizoleta Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto hakuna na bahati nzuri hata yeye alisema, anauliza maswali amepata majibu yake lakini *on top of it,* amepewa na viambatanisho vya majibu, pale ambapo alikuwa haelewi ameelekezwa, sasa tunataka nini? Mimi naamini alighafilika tu na tumemsaidia vya

kutosha, mimi ndicho ninachoamini tu hapo. Kwa hiyo, mimi nataka kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kweli leo ametusaidia sana. *(Makofi)*

Napenda pia kuipongeza Serikali na kuyapongeza Makampuni ya Madini yaliyokubali, tumefanya *review* zetu na sasa nchi yetu inafaidika na madini yetu. Hoja hizi tumesaini London ni hoja ambazo hazina *justification,* kwa sababu hakuna aliyesema tumevunja sheria gani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nami nakushukuru kwa kunipa nafasi hii adhimu. Pia nami niungane na wenzangu, kukupa pole kwa mambo mbalimbali yaliyotokea.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niwapongeze wenzangu wote, ambao wameikataa hoja hii na bila kusahau na mimi nasema kwamba, siungi mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unapokataa kitu uwe na sababu na mimi nina sababu zangu, lakini naomba kwa ruhusa yako, nianzie pale katika kipindi ambacho Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, alifanywa akae kitako baada ya kuitaja tarehe 16 na ikakataliwa kwamba tarehe 16 siyo. Bado narudia kwamba, mtoa hoja amelidanganya Bunge tangu tarehe 16 Julai, 2007 pale aliposema na naomba kunukuu: "Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 16 Julai, 2007, mara baada ya hoja ya Waziri wa Nishati na Madini kuamuliwa Bungeni. Sasa ninakwenda chini kidogo kwamba, nakusudia kuleta hoja ya kuunda Kamati Teule kuchunguza Mkataba mpya wa Madini ambao Waziri wa Nishati na Madini ameusaini bila kuzingatia maagizo ya Rais."

Katika tamko hili bila kuzingatia maagizo ya Rais, Mheshimiwa Waziri ameshalitolea tamko na imethibitishwa kwamba, Mheshimiwa Waziri hakukiuka Agizo la Rais. Hapa tunasimama pale pale kwa Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir kwamba, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, amelidanganya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mimi nimekwenda mbali zaidi na hasa hoja hii ilivyokuwa inatoka upande huu. Lililofanywa na Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Serikali ni kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Ilani ya Chama cha Mapinduzi imeweka wazi kwamba, itahakikisha Pato la Taifa linakua kwa kiwango kinachotakiwa. Sasa anapotuambia kwamba, Mheshimiwa Waziri katika Mkataba ule kuna dola milioni 818, hizi zinawasaidia Watanzania hazimsaidii mtu mwingine yeyote, lakini Mheshimiwa Waziri alipozungumzia suala la ajira kwa Watanzania 696, tupo kwenye Ilani ya Uchaguzi na tumeweka ahadi hapa kwamba, tutatoa ajira kwa Watanzania milioni moja. Bado yupo kwenye mstari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nirudie matamshi yafuatayo; Serikali makini huwa na Wabunge makini, wenye kufuata maadili ya kutodanganya wananchi wake. Lakini hiyo hiyo igeuzwe, Mbunge asiye makini, ambaye anakurupuka, asiyefanya utafiti, asiyetaka kujua undani wa mambo ulivyo ni hatari katika Taifa hili. *(Makofi)*

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, kanuni.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Kanuni ya 50.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, suala la mwongozo halipo hapa.

**SPIKA:** Nimeruhusu kuhusu utaratibu, tumsikie tu.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Spika, kipengele cha nane kinasema: "Ni marufuku kwa Mbunge yeyote kutoa lugha ya kuudhi." Mambo ya kukurupuka nadhani yanaudhi sana na si lugha nzuri ya Bunge na legelege, hakuna kipimo cha kupima Wabunge hapa, wote tuko sawa. Nashukuru.

**SPIKA:** Sasa sikuelewa Mheshimiwa Phares K. Kabuye, ulichohitaji ufafanuzi ni nini kwamba, neno kukurupuka linaudhi ama?

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Spika, neno kukurupuka linaudhi kwa sababu Wabunge wamechaguliwa kwa umakini na watu waliowaleta hapa. Legelege pia linaudhi, Mbunge legelege maana yake waliomchagua ni legelege. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sikubaliani na tafsiri hiyo, kwa sababu inawezekana kabisa Mbunge akakurupuka hata akiwa na busara. Kukurupuka ni neno la kawaida tu la Kiswahili na isitoshe tumpe haki Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir naye amalize, ataeleza hilo, maana yake ameanza tu kusema mwenzie amekurupuka, tunataharuki, hakuna haja. Huu ni mjadala wa afya kabisa, kila mtu apewe nafasi aseme lile analoweza. Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir hebu endelea. *(Makofi)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na kanitia wasiwasi kidogo Mheshimiwa Mbunge aliyekaa hivi sasa, kwa sababu katika maelezo yangu, sikumtaja Mbunge yeyote, nimetoa aina ya Wabunge, sasa kwa nini anaingia wasiwasi yeye tu? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilichosema mimi ni kwamba, Mbunge asiye makini anayekurupuka, asiyefanya utafiti, asiyetaka kuujua undani wa mambo yalivyo ni hatari kwa Taifa. Sijamtaja Mbunge yeyote hapa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maelezo yaliyotolewa na pande zote mbili, mtoa hoja na Mheshimiwa Waziri, kuna suala ambalo limezungumzwa hapa, suala la hoja linalotenganisha Bunge na Serikali, ambalo limo katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, naomba nikupe nasaha kidogo, usiwe unatulea kama babu na mjukuu. Unajua unapokuwa na mjukuu kama unampenda sana, basi inafika mahali

anafanya mambo wakati mwingine yanaondoa utaratibu. Unapotuachia tukafanya baadhi ya mambo yaliyokuwa nje ya kanuni inakuwa matatizo. Kwa mfano, kama hili la sasa hivi Mheshimiwa, ninachosema, babu unatakiwa umruhusu mjukuu wako achezee ndevu na kifua, lakini kuna sehemu nyingine unamzuia na halafu unachukua hatua. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, naomba urejee katika hoja. *(Makofi)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nazungumzia suala hili kwamba ni la Kitaifa si la kisiasa. Mbona hatutaki kuwa wakweli? Lazima tuwe wakweli. Hili ni suala dhahiri ni la kisiasa na haliondoki kwenye siasa, mtoa hoja ni mwanasiasa, Mheshimiwa Waziri ni mwanasiasa. Tumekuja hapa kutoka katika Vyama vyetu vya Siasa, tunachotakiwa sisi upande wa Chama Tawala kutekeleza shughuli za Kitaifa tulizokabidhiwa na wananchi. Sasa unapozungumza kwamba, suala hili si la kisiasa, huna haja ya kuleta hoja hii hapa. Hili ni suala la kisiasa, sote tumeingia humu katika Bunge hili tumetokea katika nyanja za kisiasa hakuna atakayekataa hapa, kama si mwanasiasa huji hapa. Kwa hiyo, suala hili liko dhahiri ni suala la kisiasa.

Mheshimiwa Spika, mengi yamezungumzwa, kutokana na misingi ya mtoa hoja ya kuunda Kamati Teule, mimi naungana mkono na wenzangu wote waliosema hakuna haja ya kuundwa Kamati Teule katika kushughulikia suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa pamoja na tuhuma zote zilizotolewa na Mheshimiwa Waziri na zile ambazo zimetolewa sehemu nyingine, tunafika mahali sasa niombe ruhusa ya kutoa hoja kama ifuatavyo: Kwa sababu ya mambo yote yaliyokuwa yamefanyika na Mheshimiwa Waziri kulithibitishia Bunge letu Tukufu kwamba, yaliyosemwa yote ni uongo, mtoa hoja amedanganya, kuna kauli Mheshimiwa Waziri kasema ni uzushi. Kwa hiyo, narudia katika ombi la Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir na mimi naomba kutoa hoja kwamba, kitumike kifungu namba 59(3) *paragraph* ya (2) naomba ninukuu: "Lakini endapo Mbunge mwingine yeyote ataona kwamba uongo uliosemwa na Mbunge huyo ni mkubwa kiasi cha kuathiri heshima ya Bunge, anaweza hapo hapo kutoa hoja kwamba, Mbunge huyo asimamishwe kazi za Bunge kwa kipindi maalum atakachokitaja katika hoja yake."

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, asimamishwe hadi Januari mwakani ndiyo aingie katika Bunge hili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, msije kunifikisha mahali nikasema mnakurupuka. *(Kicheko)*

Hoja hii tayari tunayo, imetolewa taarifa na Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir. Kwa mujibu wa Kanuni ya 59 hiyo hiyo uliyoinukuu, kama kweli itaendelezwa na nitampa nafasi Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, inaishia hivi: "… kama kuna hoja

nyingine inayojadiliwa wakati huo, basi hoja ya kumsimamisha Mbunge huyo aliyetajwa itatolewa mara baada ya hoja iliyokuwa ikijadiliwa kuamuliwa. Mmeelewa sasa?

**WABUNGE:** Ndiyo.

**SPIKA:** Kwa hiyo, tuchangie hoja tu kwa hivi sasa.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, napenda sana nikushukuru kwa kunipatia fursa hii ili na mimi niweze kuchangia kwa kifupi katika hoja iliyo mbele ya Bunge lako Tukufu. Lakini kwanza nianze kukupa pole sana kwa msiba uliokusibu wa kupotelewa na mjomba wako, Chifu Abdallah Fundikira, Chifu wa Unyanyembe. Taifa limepoteza kiongozi shupavu, ambaye alikuwa ni mfano wa kuigwa. Ana historia ndefu sana katika nchi hii na wale ambao tunatoka maeneo ya Maswa, Maswa iliyokuwa kabla ya kugawanywa katika maeneo ya Wilaya mbili za Bariadi na Meatu, marehemu alikuwa Afisa Kilimo wa Wilaya ya Maswa, kwa kipindi kirefu sana. Alifanya kazi nzuri sana kuboresha kilimo katika Wilaya ya Maswa. Mwenyezi Mungu, ailaze roho yake mahali pema peponi. *Amen.*

Hapo hapo napenda nimpe pole sana mdogo wangu, Mheshimiwa John P. Magufuli, kwa kupotelewa na baba yake mzazi. Naye tunaomba Mwenyezi Mungu, ailaze roho yake mahali pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Spika, ukiona fisi baada ya mvua kubwa ameteleza kwenye kichuguu, basi ujue mvua ilikuwa kubwa sana. Unaelewa nataka kusema nini? Lakini nina kitu kimoja, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kwa maelezo fasaha ambayo ameyatoa mbele ya Bunge lako Tukufu, kujibu hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto. Mheshimiwa Waziri, amejibu kwa kituo kila tuhuma au swali, yeye anasema swali au maswali lakini yote yamejibiwa kwa ufasaha kweli kweli. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kukamilisha rekodi ya Bunge lako Tukufu, wewe unafahamu na Watanzania wote wanafahamu, mimi nilibahatika kuwa Mwanasheria Mkuu wa nchi hii, kwa kipindi takriban cha miaka kumi na tatu. Inapoletwa tuhuma nzito kama hii inayohoji utaratibu wa maamuzi ya Bunge lako, mimi kipindi kile nilikuwa humu nikiishauri Serikali kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ndiyo maana nimeona ni vizuri nikalisaidia Bunge lako katika eneo moja ambalo Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini hakulikamilisha. Nalo linahusu ambayo Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto amesema kwamba, Serikali kupitia kwa aliyekuwa Waziri wa Fedha, alisema kuwa anarejesha ile asilimia kumi na tano ya *depreciation allowance* kwa *unredeemed capital expenditure*. Sasa hoja yake amekuwa akisema nimepitia hadi *Finance Act* ya mwaka 2000, eti hakuona hayo. Eti tunakwenda kinyume na sheria, kwa kuruhusu hayo ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil P. Mramba wakati ule aliyasema humu Bungeni.

Mheshimiwa Spika, sasa nimekuletea nakala ya majadiliano ya Bunge ya Mkutano wa Nane sehemu ya kwanza ya tarehe 11 Juni, 2002 hadi 17 Juni, 2002 kuhusiana na eneo hili. Mheshimiwa Waziri anasema: “Napendekeza kurejesha

kipengele cha *additional fifteen percent capital allowance on unredeemed qualifying capital expenditure* kwenye Sheria ya Madini Na. 5 ya mwaka 1998 kwa wawekezaji waliokuwepo hadi Julai Mosi, 2001 na akaendelea.

Mheshimiwa Spika, kama sote tunavyofahamu, maamuzi yanayoletwa na Waziri wa Fedha kupitia hotuba yake yale ambayo yanahitaji Sheria, hatua zake zinapitia kwenye *Finance Bill* na baadaye inakuwa ya *Finance Act*. Sasa nimewasilisha kwako *Finance Act*, No. 18 ya mwaka 2002, ambayo ilikuwa inafanya marejesho hayo kwa makampuni ambayo yalikuwepo yalikuwa na leseni, yalikuwa na Mikataba na Serikali kabla ya tarehe 1 Julai, mwaka 2001. Kwa sababu ya muda, nisingependa kuwasomea hili, lakini itapendeza iwapo mtoa hoja atapewa naye nakala ya sheria ya nchi ili aweze kuliona hili kwa sababu ni hoja ya msingi sana hii.

**SPIKA:** Nilimpatia nakala mara uliponipa, kwa hiyo anayo.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kusema kweli Serikali imehitimisha kwa kusema uwazi kabisa kwamba, kwa makampuni ambayo ni mapya yaliyoingia kuanzia tarehe 1 Julai, 2001, kipengele ambacho kilikuwa kinaruhusu wapate asilimia kumi na tano ya ziada kwa mtaji ambao haujarejeshwa kwa hao sasa hakuna. Lilifanyika kosa katika uandishi wa mwisho wa sheria hiyo, tukaingiza na makampuni ambayo tayari yalikuwa na Mikataba ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, wewe ni Mwanasheria pia unafahamu kwamba, haiwezekani ukachukua uamuzi *unilaterally*, wa kiimla, kama Serikali unaweza lakini madhara yake ni makubwa sana, kama unataka kuvutia wawekezaji waje nchini kwako na ndiyo maana sheria zote zinatambua haki ambayo ilikuwa imetolewa. Ukiamua kubadilisha sheria, lazima uheshimu hayo au uweke *mechanism* ambayo itamfidia yule ambaye sasa unataka kumwondolea hicho alichokuwa amepata. Kwa hiyo, hilo ni la msingi sana na Serikali yetu ni Serikali inayoheshimu Mikataba ambayo imeingia. Lakini tuseme mapitio ya Mikataba ya Madini na Petroli, ambayo ni ya muda mrefu sana ni kitu cha kawaida sana duniani. Someni maandiko haya mtayaona, lakini aliyetoa maelekezo ya kufanya mapitio ya Mikataba ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, si mtu mwingine na alisema itafanywa na Serikali yake kwa kuongea na makampuni ambayo tunayo. Mheshimiwa Rais, hajasema kwamba tukimaliza zoezi hilo tutakuja kutoa taarifa Bungeni, kazi hiyo aliituma Kamati, Kamati hiyo ni Kamati yake na ripoti hiyo iliwasilishwa kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitakachotokea kwa maeneo ambayo katika kudurusu sheria, yale ambayo tutaelewana na makampuni haya kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, tumeanza vizuri, mengine itabidi tuyalete Bungeni ili yaendane na sheria na kusema ukweli hoja za Mkataba kusainiwa nje ya Tanzania si hoja ya msingi na nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, hakuna sheria iliyovunjwa katika kusaini Mkataba huo nje ya nchi. Imeelezwa vizuri sana na baadhi ya waliochangia kwamba, la

msingi hapa ni yale majadiliano, mnakamilisha mazungumzo yanakuwa mazungumzo mazito kweli.

Ndiyo mnasema katika hatua ya kwanza, naamini Mkataba huo unasema wazi kabisa kwamba, kila *page* ya kwanza tuna *initial* mpaka ile *page* ya mwisho ambayo tunataka kuweka saini, *normally* hatu-*initiate,* maana hiyo ndiyo inaonesha kwamba haya ndiyo tumekubaliana. Haya mimi ningemwelewa sana Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto kama angesema tu kwamba, kuna ushahidi Mheshimiwa Waziri angekwenda akaingiza mambo ambayo hayakuwa yamekubalika na Serikali kabla ya kwenda kule. Lakini kama ataweza kututhibitishia hayo, atutolee hapa hadharani kwenye Bunge lako Tukufu tuyaone hayo.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna moja la msingi sana lililosemwa la kutumia jina la viongozi. Sawa, litumie vizuri basi. Baba wa Taifa Marehemu Julius Kambarage Nyerere, Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi, ni kiongozi shupavu, mahiri, anayeheshimika sana Tanzania na nje ya Tanzania na duniani kote. Kusema kwamba yeye alisema madini ya nchi hii yasiendelezwe mpaka Watanzania watakapokuwa wameelimika, jamani tusimsingizie mzee wa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika uongozi wa Mwalimu mimi nimebahatika sana kulelewa katika Sera ya Kwanza ya Madini ya nchi hii ya Mwaka 1979 na ndiyo iliyozaa Sheria ya Madini ya Mwaka 1979 na ndiyo iliyozaa Sheria ya Kutafuta na Kuendeleza Petroli ya Mwaka 1980. Yote haya yana vivutio, wakati ule Mwalimu aliliona hili mbali sana. Mheshimiwa Rais na Serikali yake wakati ule, walisema kwamba lazima tujenge mazingira mazuri ya kuleta wawekezaji. Sasa leo mnaposema kwamba Mwalimu angekuwepo Mikataba hii isingekuwepo, ni upuuzi mtupu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme lingine, kipindi kile kile tunaongelea kuhusiana na Sera ya Madini na Sheria ya Madini, tuliongea na Wajerumani, Kampuni ya kwanza ambayo tuliwekeana Mkataba wa kutafuta madini ya *Uranium* katika maeneo mengi ya nchi hii, hasa sehemu ya *Selous,* ilikuwa ni kupitia sera hizo. Nimeona niliweke wazi hilo, liwe sahihi kwa sababu kuna picha inayoanza kuonekana kwamba, Mwalimu yeye hakusema tutumie rasilimali hii kuendeleza watu wetu, nchi yetu na kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, naelewa kengele ya kwanza imelia, lakini nimalizie kwa kusema kweli Bunge lako limesikia hoja ya Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, namheshimu sana. Tumesikia hoja nyingi ambazo zinapinga hoja iliyo mbele yetu na mimi napenda niungane na wote waliosimama na kuchangia kusema hawaungi mkono hoja hiyo kwa sababu haina tija, ukweli wote umeshawekwa hadharani. Isipokuwa kama mtu anataka kwenda kuganga njaa kupitia posho ya Bunge, mimi siamini kama huo ni utaratibu mzuri wa kutumia fedha za walipa kodi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, mimi ningependa sana Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto atakapoanza kujibu ...

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Ahaa, sasa namwita tu mtoa hoja kwa sababu naona jambo lenyewe limefikia mwisho. Nadhani tumwite mtoa hoja kwa sababu na muda nao unakwenda. Mheshimiwa mtoa hoja, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nirejee kukushukuru kwa dhati kabisa kwa kuruhusu hoja hii kujadiliwa na Bunge na jambo la kufurahisha sana leo, watu wote ambao kwa kawaida wamezoea kuunga mkono hoja mia kwa mia, leo walikuwa wanapinga hoja. Watu waliokuwa wanapinga hoja leo wameunga mkono mia kwa mia na hii inaonesha ni jinsi gani ambavyo demokrasia yetu inakomaa. *The House at work*, Bunge linafanya kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nimeridhishwa na mijadala mbalimbali ambayo imeendelea ndani ya Bunge na naomba kuchukua fursa hii sasa kwanza, kujibu hoja za wachangiaji mbalimbali. Hoja yangu imechangiwa na jumla ya wachangiaji kumi na wanane na hapakuwa na mchango wa maandishi na naomba niwatambue kama ilivyo desturi ya wenzangu wa upande wa pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wa kwanza alikuwa Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Anna M. Komu, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, Mheshimiwa Suzan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Adam K. A. Malima, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Manju S. O. Msambya, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mheshimiwa Phares K. Kabuye, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir na wa mwisho kabisa ni rafiki yangu sana, Mheshimiwa Andrew J. Chenge.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na hii hoja ya mwisho ya Mheshimiwa Andrew J. Chenge kuhusiana na *fifteen percent, capital allowance on unredeemed qualifying capital expenditure*.

Mheshimiwa Spika, nilichokisema katika hoja yangu na naomba Bunge lako Tukufu linielewe, nilisema Mheshimiwa Waziri wa Fedha mwaka 2002, ali-*reinstate fifteen percent* na alisema hivi na naomba kunukuu, kwa sababu umenipatia nakala halisi ya majadiliano ndani ya Bunge:

"Napendekeza kurejesha kipengele cha *additional 15% capital allowances on unredeemed qualifying capital expenditure* kwenye Sheria ya Madini. Narudia haya ni maneno ya Waziri wa Fedha ndani ya Bunge kwenye Sheria ya Madini Na. 5 ya mwaka 1998 na hoja imeendelea. Hoja yangu namwomba Mheshimiwa Andrew Chenge, anielewe, yeye ni Mwanasheria na nisingependa atumie uzoefu wake wa ndani ya Bunge kupotosha. Nilisema hivyo na naomba kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kunukuu; "Nilipopitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2002, nimekuta sehemu ya nane inazungumzia mabadiliko katika Kodi ya Mapato ya mwaka 1973." Hata katika ukurasa wa kwanza wa Sheria hii yaani *Arrangement of contents*, Sheria ya Madini haitajwi." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kigoma Kaskazini hawakukosea kunichagua. Hapa nina sheria na ukurasa unaoelezea *content* ninao hapa na naomba nitaje *content* moja baada ya moja ili Bunge lako Tukufu liweze kuona.

Mheshimiwa Spika, *contents* ni kama ifuatavyo:-

1. *Preliminary Provisions;*
2. *Amendment of Business Licensing Act 1972;*
3. *Repeal of Car Benefits Tax acts 1991;*
4. *Amendment of the Commodity of Import Supports Regulations Act 1992;*
5. *Amendment of the Customs Tariffs Act 1976;*
6. *Amendment of the Excess Tariffs Ordinance Cap. 332;*
7. *Amendment of the Executive Agencies Act 1997;*
8. *Amendment of the Income Tax Act 1973;*
9. *Amendment of Pools and Lotteries Act 1967;*
10. *Amendment of the Road and Fuel Tools Act 1985;*
11. *Amendment of the Stamp Duty Act 1972;* na
12. *Amendment of the Value Added Tax 1997.*

Mheshimiwa Spika, hakuna *Amendment of the Mining Act*, naomba nirudie Waziri Basil Mramba alivyosema Waheshimiwa Wabunge na mnielewe, napendekeza kipengele cha *additional 15%. (Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kuhusiana na hayo anayoyasema Mheshimiwa Kabwe Zitto. Sheria ya nchi iko katika vitabu vya nchi, mambo ya utangulizi wa *Hansard, Hansard* sio sehemu sheria za nchi. *(Makofi)*

Pili, anayotueleza yawezekana Mheshimiwa Waziri Mtoa Hoja wakati ule kwa sababu yeye sio Mwanasheria hoja ya msingi pale ni nini kilichokusudia kufanyika, sasa tuongoze kwa sababu ….

**SPIKA:** *Order, order*!!!!! Utaratibu jamani.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Kwa sababu unayo na wewe nakala ya sheria ya nchi kama maudhui ya kurejesha kile kifungu hayamo katika sheria ya nchi, mwongozo wako Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Nitamwomba Mheshimiwa Kabwe Zitto, aendelee kidogo niweze kupata nafasi ya kuangalia na nitalitolea mwongozo. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nilichokizungumza katika hoja yangu nimezungumzia, naomba kurudia nilichokizungumza katika hoja yangu. Nilipopitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2002 nimekuta sehemu ya nane inazungumzia mabadiliko katika Kodi ya Mapato na hata katika hoja ya kwanza ya sheria hii ambayo nimeitaja *content* zote, katika *arrangements of contents* Sheria ya Madini haitajwi na ninachofahamu mimi *Hansard* ni Taarifa Rasmi za Bunge na baadhi ya vielelezo ambavyo Waziri alikuja kujibu hoja ametumia *Hansard* kujibu, kwa hiyo, tunataka kuambiwa kwamba tusiamini *Hansard? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hoja hii ambayo Wabunge kadhaa wamechangia kwa sababu nimeshataja Wabunge waliochangia nisingependa kuweza kurudia majina, ingawa baadaye naweza nikarudia majina.

Mheshimiwa Spika, mantiki ya hoja yangu ilikuwa ni kwamba mwaka 2001 Sheria ilibadilishwa na katika hili napenda nieleze Wabunge wote tulivyoingia hapa Bungeni tuligaiwa *CD* zenye sheria zote za nchi toka mwaka 1961 na tumetumia *CD* hizi ambazo zimegawiwa na Ofisi ya Spika kwa ajili ya kufanyia kazi utafiti wetu. Nitakuwa mtu wa ajabu sana niende nizushe tu mambo ambayo sijayafanyia kazi. Kwa hiyo *CD* zote zimeeleza na nimeeleza katika hoja yangu ya msingi kuwa mwaka 2002 Waziri ali-*reinstate* sheria hii na Mheshimiwa Spika, wakati hoja zinajibiwa tumeambiwa kwamba mwaka 2006 makubaliano yamefikiwa na watu wachimbaji wa madini kwamba kipengele hiki kiondolewe na wala mimi sijahoji mantiki ya kuondoa kipengele, nimehoji mantiki ya utaratibu wa uondoaji wa kipengele, ndicho nilichohoji mimi ambalo ni jukumu la Serikali kuweza kujibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maelezo Waziri aliyejibu hoja amesema kwamba mkataba wa Buzwagi uliandaliwa Tanzania na wataalamu wetu na ukapitia taratibu zote zinazopaswa kufuata ikiwa ni pamoja na kuidhinishwa na Kamati ya Ushauri wa Madini na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pia Waziri, Mheshimiwa Nazir Karamagi akawasilisha vielelezo vya ushahidi wa maneno yake. Barua yenye kumbukumbu Na.CDB 14301 ya tarehe 16 Februari, 2007 iliyotoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri wa Madini kwenda kwa Waziri wa Nishati na Madini, barua nyingine yenye kumbukumbu Na. JCA1305016 ya tarehe 16 Februari, 2007 ya kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwenda kwa Kamishna wa Madini.

Kwa mujibu wa barua hiyo kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya ushauri ya Madini inaonyesha wazi kabisa ukiisoma ile barua Waziri ndiye aliyeanzisha kusudio la kutaka Mkataba wa Buzwagi usainiwe. Namshukuru sana Mheshimiwa Phares Kabuye, ameli-*raise* suala hilo. Inavyoonyesha ni kwamba vikao viwili vya Kamati ya Ushauri vilikaa, kikao cha kwanza kilikaa tarehe 6 Februari na kikao cha pili kilikaa tarehe 16 Februari, 2007. *(Makofi)*

Hoja yangu ya Kamati Teule ya Bunge ni kwamba kumbukumbu za vikao vya tarehe 5 Februari na tarehe 16 Februari, 2007 zipitiwe ili Bunge lijiridhishe na kumbukumbu hizo Mheshimiwa Waziri hajazileta hapa *minutes* za Kikao cha tarehe 5 na

cha tarehe 16 zipitiwe ili kuweza kujiridhisha kama Waziri alifuata ushauri ambao ulitolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu ulivyokwenda kabisa kabisa ni dhahiri kwamba Waziri alifahamu kwamba kuna kusainiwa kwa mkataba. Mosi, Waziri anajenga dhana kuwa tukio la kusainiwa kwa mkataba huu lilijitokeza kwa dharura na wakati yeye akiwa safarini ndiyo wanavyotaka Wabunge waamini na wengine wameamini na wanavyotaka jamii iamini.

Mheshimiwa Spika, dhana hii ambayo Mheshimiwa Waziri alitumia nguvu zake zote kuijenga bado mimi kama mtoa hoja naona haina nguvu na nina sababu zangu. Kukamilika kwa maandalizi ya utiaji saini mkataba kunamaanisha pia uwepo wa watiaji saini na kama maandalizi yalishakamilika basi watu wa *Barrick* wangekuwa tayari wapo Tanzania kwa ajili ya kusaini mkataba huo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, inaonyesha kuwa kitendo cha Waziri kusaini mkataba huu London, Uingereza hakikujitokeza kwa dharura, kilipangwa. Waziri alisaini mkataba huu Uingereza, juma la mwisho la mwezi Februari, 2007. Vikao ambavyo nimevieleza vimekaa tarehe 5 na tarehe 16 Februari, 2007 kwa taratibu zozote zile, Waziri hakurupushwi kusafiri, lazima kulikuwa kuna *schedule* ambayo inafahamika kabisa kwamba Waziri atasafiri. Kwa hiyo, alipanga kukutana na watu wa *Barrick* London, *it is very clear* na wala huhitaji Mbunge awe makini sana kuweza kufahamu usawa huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la uharakishaji, Waziri amejieleza kwamba ilipasa tuharakishe tusipoteze uwekezaji naomba niulize kitu hapa. Hivi nani amesema dhahabu ni ndizi inaoza, kwamba ukiacha kusaini itaoza, itaharibika, Taifa litapata hasara, nani amesema? Dhahabu ni madini na yanakaa pale. Kwa hiyo, mimi sipati mantiki ya uharaka wowote ule wa kusaini mkataba huu na kwa kweli bado naamini kabisa kuna sababu ya msingi kabisa, Bunge lako Tukufu kuunda Kamati Teule ili kuweza kuondoa mashaka haya ambayo yamezungumzwa. *(Makofi)*

Kuhusu suala la kusaini London na kutokusaini London ambao watu wameeleza sio sababu na haina maana yoyote na vitu kama hivyo. Mheshimiwa Waziri anasema si muhimu kwamba mkataba umesainiwa London au kutokusainiwa London, anatuonyesha kwamba *format* ya Mkataba wa Buzwagi haionyeshi mkataba ulisainiwa wapi. Kwa mujibu wa hali ya teknolojia ilivyo hili hatulikatai na wala hamna mtu anayelikataa. Mtu anaweza kuwa Buenos Aires, Argentina akaweka sahihi mkataba na kuutuma kwa huko Laspalma, Spain na mwingine akaweka saini. Hili halihitaji kuelezwa ndani ya Bunge lako Tukufu kwani hivi sasa watoto wa shule za sekondari wanafanya *scanning* na pia *attachments* za *E-mails,* kilichotofauti hapa ni kwamba Waziri wetu wa Nishati na Madini hakuwa Dar es Salaam na kupeleka Mkataba London, naomba hii *concept* ieleweke.

Mheshimiwa Spika, *concept* ya kwamba mkataba unaweza ukatumwa kwenye *e-mail* ni pale ambapo mimi leo niko Dodoma, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed

yupo Bujumbura, nachukua mkataba nasaini na-*scan signature* nautuma Bujumbura anasaini *signature*, yeye anakuwa na kopi yake na mimi nakuwa na kopi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili la Buzwagi haikuwa hivyo, katika hili la Buzwagi *part* zote *to the contract* zilikuwa London. Kwa hiyo, ni lazima unaposaini mkataba huo ionyeshe kama umesainiwa London useme *signed in London* tarehe hii na hii, hebu Waheshimiwa Wabunge waangalie sheria zetu zinapowasilishwa hapa Bungeni. Katika sheria yoyote, katika hoja yoyote ambayo Waziri anaileta ni mfano tu wa kawaida pale chini mwisho pale anaandika Dar es Salaam ama Dodoma na kuweza kugaiwa. Sasa hapa tunazungumzia mkataba wa nchi, mkataba kati ya dola na Kampuni binafsi.

Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba kwa mujibu wa maelezo haya ambayo Waziri ameeleza ninaendelea kuwashawishi Waheshimiwa Wabunge wenzangu kukubali kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge ili Bunge lako Tukufu lijiridhishe na kuliridhisha Taifa kwamba Mkataba huu upo sawa sawa, Watanzania watatushangaa tunapoacha maeneo yenye utata bila ya kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Katika suala hili pia watu wanaweza kusainiwa London au Dar es Salaam haijalishi wapi. Juzi mzee mmoja aliniambia vitu vya maana sana, siwezi kusahau katika masuala ya majadiliano na kusainiwa kwa mikataba. Aliniambia unapokuwa katika majadiliano yoyote au unapotarajia kusaini makubaliano yoyote uzingatie vitu vitatu kwa Kiingereza *power, time and information*, katika hali ya kawaida naanzia *power*. Katika hali ya kawaida unapokuwa unataka kukubaliana kitu na mimi ukaja kukubaliana hicho kitu na kuwekeana sahihi nyumbani kwangu *you are weak. (Makofi)*

Kwa hiyo, Waziri anapotuambia kwamba ilibidi atekeleze matakwa ya wawekezaji tena kwenye uwanja wao wa nyumbani kwa vyovyote vile lazima atakuwa *weakened.* Ndiyo maana bado pamoja na majibu haya ya Waziri, naomba Kamati Teule iweze kuangalia labda kwa sababu ya nadharia hii ya *power* inawezekana kabisa kwamba Waziri wetu kwa kwenda kwenye uwanja wa nyumbani wa wenyewe alikuwa *weakened.* Nataka Kamati iweze kuangalia kama maslahi ya Taifa yalizingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maelezo yangu nilihoji masuala kadhaa kuhusiana na maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuna baadhi wamesema kwamba tusitumie tumie majina ya viongozi wetu, mimi kama Mbunge nina wajibu wa kufuatilia matamko ya viongozi wakuu wa nchi. Vile vile ninamheshimu sana Rais wetu wa sasa na siwezi hata kidogo kutokutafakari maagizo yake kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 17 Julai, 2006, akisoma hotuba ya Bajeti Waziri wa Nishati na Madini wa wakati huo Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, alisema kuwa Serikali imesitisha kusainiwa kwa mikataba mipya ya madini. Tazama *Hansard* ya tarehe 17 Julai, 2006 ukurasa wa 41 mpaka 42. Serikali haijatamka ndani ya Bunge lako Tukufu kuwa usitishaji huu umeondolewa na wala hii haikuwa kauli ya Rais tena ni kauli ya Waziri ndani ya Bunge. Bajeti iliyopita na Waziri wa sasa alikuja kwenye Bajeti hii hakuliambia Bunge hili Tukufu kwamba kuna mkataba mpya umesainiwa na Wabunge wengi leo hii wanaizungumzia Buzwagi baada ya ku-*raise* hoja hiyo Buzwagi. Vinginevyo hoja hiyo ilikuwa kimya na Wabunge wote wanajua kwamba leo hii hoja ya Buzwagi inazungumzwa kwa sababu niliizungumza. Waziri hakuliambia Taifa na

alikuwa na nafasi katika hotuba yake ya Bajeti kuliambia Taifa. Kwa sababu mgodi huu utaanza utekelezaji wake ndani ya mwaka huu wa fedha. Ndiyo, kwa hiyo ilikuwa ni jukumu la Waziri kuweza kulieleza Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kama nilivyosema haijatamka tena, kwa hiyo, tulio Wabunge makini, narudia kusema tulio Wabunge makini tulipopata tetesi kuwa kuna mkataba mpya umesainiwa, tukaja kuhoji hapa Bungeni. Mimi kama Mbunge nisingekwenda kuhoji mtaani *as a forum, forum* yangu ni Bunge ndiyo nimekuja kuhoji ndani ya Bunge, sasa kulikoni?

Waziri lazima ajibu masuala haya kikamilifu na Taifa limwelewe ni lini usitishaji huu uliondolewa ambao Waziri Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha alisema. Mathalani Waziri ameweka saini mkataba huu takribani miezi sita tu tangu tamko hilo la Serikali na isitoshe mkataba huu umesainiwa wakati Bunge la Februari lilikuwa tu limemaliza mkutano wake, Bunge halikutaarifiwa kama kuna uamuzi mzito kama huu, jambo hili linatia shaka na shaka yoyote hamna namna ya kuiondoa isipokuwa kwa uchunguzi wa kina na uchunguzi wa kina unafanywa kupitia Kamati Teule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri katika majibu yake anasema kuwa Kampuni ya *Barrick Gold Corporation* imekubali kulipa kodi ya mapato, naomba watu warudi kwenye ukurasa wa tano wa majibu ya Waziri, *this is very serious.* Waziri anasema Kampuni ya *Barrick Gold Corporation* imekubali kulipa Kodi ya Mapato, Kodi ya Mapato yaani *Corporate Tax,* Waziri hajasema *Provisional,* amesema kodi ya mapato na nakala ambayo imewasilisha ndani ya Bunge amesoma. Waziri anataka kutuambia kuwa hizi dola za Marekani milioni saba wanazolipa *Barrick* ni Kodi ya Mapato?

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri aangalie vizuri majibu yake maana yanaweza kuzaa hoja mpya kabisa. Kodi ya Mapato ina Sheria maalumu *Income Tax Act, 2004* na kwa wale Wabunge wengine ambao labda walipewa hoja waseme *Income Tax Act, 1973* tulii-*repeal to 2004*. Hizi dola milioni saba kutoka *Barrick* ...

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza na uniongoze, anafuata yale aliyosoma ama niliyoyasema nilipokuwa nimesimama pale. Kwa sababu nangoja *Hansard* kusudi aone niliyoyasoma pale ama niliyoyasema nilipokuwa nimesimama pale. Kwa sababu nangoja *Hansard* kusudi aone niliyoyasoma pale ama anasimama aliyoyasoma kwenye karatasi.

**SPIKA:** Nimemsikia na ananukuu ukurasa wa tano na mimi nilikuwa nautazama wa hotuba yako. Lakini sijaliona hilo.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** *Bullet* ya tatu katika Ibara ya pili kutoka juu. Lakini Mheshimiwa Spika, hoja yetu ni kwamba malipo ya awali ya kodi.

**SPIKA:** Ndiyo, tusubiri, tusubiri. Namwomba Mheshimiwa Kabwe Zitto kwenye mambo haya ambayo ni mazito aache *technicalities,* zinaleta taabu, kwa mfano nirudi ile ya kwanza nimeisoma sasa. Ni kweli Waziri Mheshimiwa Basil Mramba alipokuwa Waziri wa Fedha alizungumza na akanukuliwa moja kwa moja kwenye *Hansard* kama

ulivyo utaratibu, akaelezea nia yake kuwa napendekeza kurejesha na akaitaja Sheria ya *Mining* ya mwaka 1998. Hatma yake hakufanya hivyo, lakini ukweli sasa ukisoma katika ile *Finance Act* ya mwaka 2002, kodi hiyo aliishughulikia kupitia *Finance Act.* Sasa katika madini vyote viwili vina-*apply* katika *Finance Act,* ikikugusa lazima ulipe kodi. Sasa kutofautisha ili mradi haikuingia kwenye Sheria ya Madini basi ni kosa kwa sababu tu Waziri alikusudia hivyo, hiyo tunafanya kama ni kweli kiufundi ufundi unaweza kusema ni kosa lakini unafika pahala ambapo...

Ndiyo, lakini hapa hatukai kufanya mchezo wa *debating society* ya shule hapa. Hatuko *Secondary School* kusema kwamba una *score point* kwa kutofautisha Serikali inatoza kodi ama kwenye Sheria ya sekta ama kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato. Kodi hii imerejea sasa nongwa ni ipi?

Kwa hiyo, mwongozo wangu kwa ile ya kwanza aliyosema Waziri wa Miundombinu ni kwamba hakuna kosa lolote kwa Waziri kueleza makusudio yake au nia na baada ya hapo kutumia sheria tofauti kutoza kwa sababu hatma yake kodi hiyo inabidi ilipwe kwa nchi yetu.

Hili la pili hili namrudisha tena Mheshimiwa Kabwe Zitto, malipo ya awali ya Kodi ya Mapato kwa Kiingereza ni *Provisional Tax*. Kwa Kiingereza hicho hicho na kwa masuala ya taaluma ya kodi huwezi kusema *Provisional Tax* ni sawa sawa kabisa na *Income Tax*. Kwa hiyo sijui, mimi nadhani Mheshimiwa mtoa hoja nenda kwenye majibu ya Mheshimiwa Waziri utusaidie pale ambapo wewe unaona tatizo la kikweli. Lakini kwenda kwenye matatizo ya kiufundi kama tulivyokuwa tunafanya kwenye *High School* kwa kweli haistahili hapa katika Bunge. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa maelekezo, napenda tu niweke wazi kabisa kwamba katika hotuba ya Waziri amezungumza Kodi ya Mapato, angeishia kodi isingekuwa tatizo, kwa sababu Serikali inaweza kutengeneza kodi ya aina yoyote ile. Lakini amezungumzia Kodi ya Mapato na naomba msome hiyo hotuba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mmoja wa Wabunge waliochangia amesema ni vyema ningeomba kupatiwa mkataba ili niuone na nijiridhishe, Mbunge yeyote makini, hili ndilo angelifikiria la kwanza, yoyote yule. Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani wakati anachangia amezungumza kuwa tarehe 17 Julai, 2007, siku moja tu baada ya kuchangia hoja ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini niliandika barua kwa Waziri wa Nishati na Madini ili anipatie mkataba huo niuone na nakala ya barua ninayo hapa na Mheshimiwa Spika, nilikuletea nakala. Nilitumia kifungu cha Sheria ya Kinga za Bunge, Sheria Na. 3 ya mwaka 1988, kifungu cha 10, mpaka hapa ninapozungumza si tu sijapatiwa mkataba huu bali hata jibu la kupokea barua yangu sijalipata. Nilitoa nakala ya barua yangu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwako Mheshimiwa Spika, sishangai kutojibiwa kwani kuna uharaka kumjibu Mbunge tena chini ya sheria zetu au kuna uharaka kwenda kusaini mkataba London? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kungekuwa na nia njema, Mheshimiwa Waziri angenijibu barua yangu na kunionyesha mkataba chini ya kiapo. Kufichwa kwa mkataba huu inathibitisha kuwa labda kuna mapungufu ambayo Bunge lako Tukufu halitakiwi kuyaona. Hata pale nilipoomba kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kabwe Zitto nikusaidie, tafadhali keti.

Waheshimiwa Wabunge, suala hili la mikataba na kudai taarifa mbalimbali nilizungumza na Mheshimiwa Kabwe Zitto na viongozi wakuu wawili, Kiongozi wa Upinzani Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Dr. Slaa. Nikawaambia hivi pamoja na sheria ile inavyosema utaratibu ni Ofisi yangu kudai kwa niaba ya Mbunge sio kila Mbunge atakuwa anakwenda ofisi yoyote unadai nyaraka. Ikiwa hivyo sisi watu 300 hata tukiondoa Mawaziri 60, Wabunge 240 hebu fikirieni Waheshimiwa kama kutakuwa hakuna utaratibu, yeyote anakwenda ofisi yoyote anadai karatasi anayoitaka na lazima apewe na mkumbuke Waheshimiwa Wabunge baadhi yenu mnafanya biashara, tunajuaje wewe unataka kwa ajili ya maslahi ya nchi au unataka kwa ajili ya biashara zako?

Niliwaarifu na wakatae hapa kwamba kwa njia hii kweli hamjajibiwa, tunaomba mpitie ofisi yangu mimi nizidai, Katibu wa Bunge adai nyaraka Serikalini kwa niaba yenu na mtazipata mkatae. Mnaposimulia mambo haya muwe mnasema na hayo ya ziada. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Waziri ananijibu, alisema eti mimi natafuta *cheap popularity*. Mimi sipo, hivyo hata kidogo, sihitaji *cheap popularity.* Nafanya kazi yangu iliyonileta hapa Bungeni na wananchi wa Kigoma Kaskazini. Sasa kama wananchi wanaona mimi ni maarufu, huu ni uamuzi wao wananchi na kama kuna watu wanachukizwa na umaarufu wangu sina cha kuwasaidia. Ninachowashauri ni kufanya kazi kwa bidii ili wananchi watambue kazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri katika majibu yake amekihusisha chama changu eti kwamba ninaleta siasa. CHADEMA ni chama kilichosajiliwa kihalali kabisa kwa mujibu wa sheria. CHADEMA kama chama cha siasa kina haki zote kufuatilia mijadala ya Bunge na kutoa matamko. Matamko ya chama cha siasa ni jukumu la kisiasa la kila chama *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matamko ya chama cha changu waulizwe viongozi wangu wa chama. Lakini matamko yangu kama Mbunge niulizwe mimi. Ni kuunganisha mambo mahali pasipo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati akichangia Mheshimiwa Suleiman Kumchaya amesema kuwa kuunda Kamati ya Bunge ni kupoteza fedha za wananchi. Nimeshtuka sana kusikia kauli hii, Bunge limepewa Mamlaka na Katiba ya kusimamia Serikali. Njia mojawapo ya kuisimamia Serikali ni kuunda Kamati Teule ya Bunge. Tena hapa tunaunda Kamati Teule ili kujadili suala la madini ambayo mchango wake katika Taifa si wa kupuuzwa. Kamati Teule kwa taarifa ya Mheshimiwa Suleiman Kumchaya inaundwa

na Wabunge takribani watano tu. Hivyo wasiwasi wa fedha za wananchi anautoa wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inashangaza eti leo tunaona taabu kutumia fedha za nchi. Tumesahau kuwa tumetumia fedha nyingi za nchi huko nyuma tena kwa sababu ya mmoja wa watuhumiwa kuleta mashahidi wengi hata wasiohusika katika kesi husika, inashangaza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Suleiman Kumchaya amesema pia kuwa baadhi ya Wabunge wanatumia Bunge kama uwanja wa siasa na Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, ameizungumza hiyo lakini kwa tofuati, sipati mantiki ya hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza Wabunge ni wanasiasa kwa vyovyote vile mjadala wa Bunge haiwezi kukwepa siasa. Lakini wananchi ndiyo wanaojua, ni Wabunge gani wanageuza Bunge kuwa uwanja wa siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilichokifanya ni kuleta hoja yangu, imejadiliwa itafanyiwa maamuzi, nimetekeleza wajibu wangu. Moyo wangu mweupe kabisa uamuzi ni wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Manju Msambya na Mheshimiwa Ruth Msafiri wamezungumzia *video conferencing,* naomba wakajifunze vizuri jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *video conferencing* ni mkutano tu, si kusaini mikataba ya kisheria na wala mifano hii haiendani kabisa na hoja iliyo mbele yetu. *Video conferencing* haliingizii Taifa katika mfungamo wa Kimkataba. Kwa hiyo, kulinganisha kusainiwa kwa mkataba na *video conferencing* ni kuchanganya mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naungana kabisa na Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya aliposema kuwa Katiba na ametaja vipengele vya Katiba inatupa mamlaka ya kujadili mambo haya. Nimalizie hoja yangu kwa hoja mbili muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir na baadae Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir na baada ya maelezo yako wamenijibu na kusema kwamba niadhibiwe.

Mheshimiwa Spika, hoja mahususi iliyo mbele yetu ni hoja ambayo nimeisoma hapa Bungeni. *(Makofi)*

Narudia tena, hoja mahususi iliyo mbele yetu ni hoja ambayo nimeisoma hapa Bungeni. Kanuni za Bunge ziko wazi kabisa. Kama Mbunge ameona nilimzushia Waziri kuna taratibu za Kikanuni tena Mbunge mwenyewe anaweze, Mnadhimu wa Serikali anaweza angeweza kutoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuchanganya mambo haya mawili kwa maoni yangu mimi ni hoja mbili tofauti kabisa kabisa. Lakini Katiba inatoa uhuru, Kanuni zetu zinatoa uhuru, Mbunge anaweza akaleta hoja yake mahususi kuhusiana na suala ambalo Mheshimiwa

Mudhihir Mudhihir amelizingumza na Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir amelizungumza. Hata hivyo naomba kurejea mwaka 1978. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 1978, pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kulikuwa na Jarida linaitwa Cheche, Serikali ikalifungia Jarida hili. Katika toleo la mwisho la Jarida hili la Cheche walisema hivi, *you can burn organisations, you can liquidate people, but revolutionary ideas never die.*" *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inaweza ikatolewa hoja, nimetimiza wajibu wangu, maamuzi ni ya Bunge, moyo wangu ni mweupe, ni jukumu la Bunge kuweza kuamua na kutoa uamuzi. Ninachoomba tu nitendewe haki, nipewe haki ya kusikilizwa kwa sababu haki ya kusikilizwa ni haki ya msingi kabisa kwa hiyo, kama kuna hoja yoyote ya kuniadhibu kwa vyovyote vile na bahati nzuri Mheshimiwa Spika ni Mwanasheria; kwa vyovyote vile nitapata *the right of hearing*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya bado nalishawishi Bunge lako Tukufu njia pekee ya kuweza kuondoa ukungu wote kuhusiana na hoja ambazo nimezieleza ni kuunda Kamati Teule ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*
**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hoja hiyo imetolewa na tutaiamua lakini naomba nitoe maelezo yafuatayo hususan kuhusu hiki alichosema Mheshimiwa Kabwe Zitto hapa mwisho.

Kanuni ya 59 (3), inaruhusu hoja nyingine kuweza kujadiliwa baada ya kuamua ile ya awali. Naomba nisome ile sentensi ya mwisho. Ikiwa kama anavyodai Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir anadhani kwamba Mheshimiwa Kabwe Zitto katika mwenendo mzima na mimi nasema lazima tuyachukue tangu tulikoanzia na ndiyo maana *reference* zote mpaka nakala za Miswada na nakala za sheria na kadhalika ni mlolongo ule ule wa kutufikisha, leo ni kuhitimisha tu. Kwa hiyo, huhesabu unapoangukia lazima uanzie kuhesabu pale ulipojikwaa ndiyo kawaida. *(Makofi)*

Kwa hiyo, niliiweka kiporo hoja ya Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Kanuni ya 59 ambayo inasema kwamba; "Endapo Mbunge mwingine yoyote ataona kwamba uongo uliosemwa na Mbunge huyo mwingine ni mkubwa kiasi cha kuathiri heshima ya Bunge aweza papo hapo kutoa hoja kwamba Mbunge huyo asimamishwe kazi za Bunge kwa kipindi maalumu atakachokitaja katika hoja yake. Hoja ya aina hiyo yaweza kutolewa bila taarifa na itajadiliwa na kuamuliwa kama hoja nyingine yoyote."

Sasa hili ndilo la muhimu kama kuna hoja nyingine kama hii ya Mheshimiwa Kabwe Zitto inayojadiliwa wakati huo basi hoja ya kumsimamisha Mbunge huyo aliyetajwa itatolewa mara baada ya hoja iliyokuwa ikijadiliwa kuamuliwa. Kwa hiyo, sasa tuiamue hoja ya Mheshimiwa Kabwe Zitto.

Hoja iliyombele yetu ni kutaka iundwe Kamati Teule ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 104 ili kuchunguza utiwaji sahihi wa Mkataba baina ya Serikali na Kampuni *Barrick* kuhusu *Buzwagi Mine* na mazingira yote yanayoizunguka hiyo. Hoja hiyo imetolewa na imeungwa mkono. *(Makofi)*

*(Hoja ya Uchunguzi wa Mapitio ya Mikataba ya Madini iliyowasilishwa na Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto ilikataliwa na Bunge)*

**SPIKA:** Wasioafiki wameshinda na kwa kura hizo Bunge limekataa kuundwa kwa Kamati Teule kuchunguza ule Mradi wa Buzwagi.

Sasa tunaingia awamu ya pili na awe makini maana yake hapa si jambo jepesi kumuadhibu Mbunge, mimi nafuata Kanuni tu kwa sababu siwezi kuzuia hoja zinazoletwa mbele yetu lakini tuwe makini. Kwa sababu katika kufanya hivi tusije tukajifikisha pahala Wabunge wasiwe na wepesi wa kuyasema yale wanayolindwa na Katiba katika Ibara ya 100 (1) kwamba wawe na hofu. Lakini kama ukidhihirika uongo basi Kanuni nazo zinachukua hatua yake. Basi Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir nakuomba uendelee pale ulipoishia.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, hoja hii iliyotukutanisha hapa leo na mzizi wa hoja iliyotukutanisha hapa leo unaonekana katika *Hansard* ya tarehe 16 Julai, 2007 ukurasa wa 181 na kwa mara nyingine napenda niikukuu.

Mheshimiwa Kabwe Zitto alisema mambo yafuatayo; "Mheshimiwa Spika, kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri kuhusiana na mkataba mpya wa Mgodi wa Buzwagi ambao Mheshimiwa Waziri ameeleza maelezo ambayo si sahihi, amedanganya na ameeleza vitu ambavyo kwa kweli sivyo ambavyo vipo katika Mkataba ambao ameusaini."

Mheshimiwa Spika, kudangaya Bunge ni kosa kwa mujibu wa Kanuni zetu, lakini kwa kushindwa Mheshimiwa Kabwe Zitto leo kuthibitisha kwamba yale maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Nazir Karamagi kwamba yalikuwa ni ya uongo maana tumemsikiliza na hakuna hata neno moja alilobisha ina maana maneno yake kusema kwamba amedanganya ameeleza vitu ambavyo kwa kweli si ambavyo vipo katika mkataba ambao ameusaini ni kosa kwa mujibu wa Kanuni ya 50(1) ya Kanuni zetu za Bunge. *(Makofi)*

Mheshmiwa Spika, kwa faida ya wengine wanaotusikiliza, ningeomba kunukuu Kanuni hiyo; "Ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni kwa sababu hiyo Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni atawajibika kuwa na hakika kwamba maelezo anayoyatoa ni sahihi na si mambo ya kubuni au ya kubahatisha tu na Spika au Mbunge mwingine yeyote aweza kumdai Mbunge huyo atoe uthibitisho wa usemi wake. Mbunge aliyetakiwa kufanya hivyo atawajibika kutoa uthibitisho huo katika muda atakaopewa na Spika."

Kwa ajili hiyo mtoa hoja alipewa muda huo na Spika na leo ametoa maelezo yake na ameshindwa kuthibitisha uongo wa Mheshimiwa Nazir Karamagi, kwa msingi huo Kanuni ya 59(3) inasema; "Iwapo hadi kufikia mwisho wa muda aliopewa Mbunge aliyeamuliwa kuthibitisha ukweli wa usemi wake kwa mujibu wa Kanuni 50(1) atakataa au atashindwa kutoa uthibitisho huo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge basi Mbunge huyo atachukuliwa hatua na Spika kwa mujibu wa Kanuni 59(2)."

Mheshimiwa Spika, lakini mimi naona uongo huu ni mkubwa zaidi ndiyo maana naomba kitumike kifungu 59(3). Kwa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba Mheshimiwa Kabwe Zitto asimamishwe kazi ya Ubunge kuanzia leo na Mkutano wa Tisa. Nasema hivi si kwa nia ya kumkomoa yeye au wapiga kura wake, nasema hivi ili kuzuia vitendo hivi vya kuzuliana zuliana visiendelee ndani ya ukumbi wako wa Bunge. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. DR. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nataka niwarejeshe kwenye maneno ya Kanuni ili tujue uamuzi tunaotakiwa kuchukua uchukuliwe katika mazingira yapi. Kanuni ya 59(3) inasema na ameinukuu mpaka pale katikati akaicha. Ili Mheshimiwa Mbunge aadhibiwe katika namna aliyomalizia Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, inabidi turidhike kwamba uongo uliosemwa na Mbunge huyo ni mkubwa kiasi cha kuathiri heshima ya Bunge. Ndiyo hayo yanafuata. Kwa hiyo, sasa mjadala uko wazi hoja ya Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir ya kumsimamisha Mheshimiwa Kabwe Zitto, kwa kipindi alichokitaja sehemu iliyobaki ya Mkutano huu na Mkutano wa Tisa imeungwa mkono sasa tunaingia katika hatua ya kuijadili. Nitaomba wale wanaotaka kujadili wasimame na nimeletewa karatasi na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa.

Mheshimiwa Waziri unaanza au unataka kuchangia. Sekretarieti, hebu andikeni majina sasa. Sasa kwa kuzingatia hali halisi ningemwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, atoe hoja kwa sababu tumebakiza dakika 25 na sioni kama zitatuwezesha kulimaliza suala hili. Kwa hiyo, atoe hoja ili tuweze kuendelea kwa muda usiozidi nusu saa. Baada ya saa mbili kasaro robo.

**Hoja ya Kutengua Kanuni za Bunge**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, BUNGE - MHE. DR. BATILDA S. BURIAN:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa mujibu wa Kanuni ya 124 naomba Bunge lako Tukufu likubali kutengua Kanuni ya 21(4) ili tuweze kuendelea na hoja iliyopo mbele yetu mpaka hapo tutakapo hitimisha hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Kutengua Kanuni ya 21 ilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Hoja hiyo imekubaliwa kwa hiyo, tutaendelea hadi ikibidi hasi saa mbili na robo. Sasa Mheshimiwa Dr. Slaa

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, labda mwongozo tu kwa sababu muda ni huo mdogo. Tunaongea muda wa kawaida au tunaongea kwa muda gani.

**SPIKA:** Nadhani ni kwa sababu suala la utaratibu tu kuthibitisha kitu pengine dakika tano inaweza kutosha.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza kuchangia hoja hii ya kwanza ambayo Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir ameitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme kwamba sikubaliani na hoja ya kumsimamisha Mheshimiwa Mbunge kwa sababu kilichokuwepo hapa mbele yetu ni suala la kujadili hoja ya kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge; na ushahidi wote uliokuwa unatakiwa ni wa kwenda kwenye hoja hiyo. Lakini ushahidi wa uongo na ukweli bado ni suala halijajadiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Waziri amewasilisha hapa nyaraka mbalimbali, alichowasilisha kwetu ni nyaraka ambazo zinaonyesha jinsi mchakato ulivyofanyika hadi kufikia yeye kusaini. Kilichowasilishwa ni zile zinazoonyesha kodi ile asilimia 15 kama ilirejeshwa au hapana. Lakini hoja ya Mheshimiwa Kabwe Zitto ilienda mbali zaidi ilienda kwenye kutafuta kama Mkataba wenyewe upo. Mheshimiwa Waziri hajawasilisha ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unapochukua uamuzi wa kumsimamisha mtu ni lazima tuwe na uhakika *beyond reasonable doubt* kwamba Mheshimiwa Kabwe Zitto amedanganya Bunge. Hoja ya kudanganya haiwezi kujengwa kwa sababu tu tumejibiwa hapa au kwa sababu tu imepigwa kura. Kura imeweza kupigwa na ushahidi wa Bunge hili ni kwamba tunapiga kura kwa wingi kwa misingi ya watu walivyokaa kiitikadi si kwa misingi ya ukweli. *(Makofi)*

Sasa unapofika kwenye uamuzi wa kwenda kumsimamisha mtu kwa sababu ya matokeo ya kura hatumfanyii mtu huyo haki. Kwa hiyo, kinachotakiwa sasa ili Mheshimiwa Kabwe Zitto aweze kuchukuliwa hatua na mimi nakubali achukuliwe hatua kama kweli amedanganya Bungeni na kama kweli amesema uongo na kama kweli

amemchafuliwa jina Mheshimiwa Waziri ni lazima Mbunge yeyote wa upande wowote ule achukuliwe hatua kama kweli inathibitika hivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa ili hiyo iwe kweli mimi ninaomba sasa hatua zote zichukuliwe za *document* zote muhimu katika suala hili kama alivyoomba Mheshimiwa Kabwe Zitto, ziwasilishwe, ziangaliwe na Kamati Maalumu ndiyo tujue kwamba amedanganya au hakudanganya. *(Makofi)*

Lakini dhidi ya kupitia kwenye hiyo kwa misingi tu ya kura zilizopigwa nadhani ni kwenda kinyume na utaratibu wowote wa demokrasia katika nchi hii na itakuwa ni kinyume na utaratibu wa demokrasia popote duniani. Kwa kuwa muda ni mfupi naomba niseme tu kwamba katika misingi ya aina hii...

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, muongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Manyanya, mwongozo.
**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kurejea mazungumzo ya msemaji ambaye alikuwa akiendelea katika kifungu cha kusema uongo kwamba humu ndani tunapiga kura kwa kufuata makundi yetu na si kufuata ukweli. Naomba athibitishe.

**SPIKA:** Tumpe nafasi aongee, kila mtu ana haki ya kuongea. Kama unapingana nae basi inabidi. Sasa kwa kuwa aliomba mwongozo, mimi siwezi kuwakadiria Waheshimiwa Wabunge wanapiga kura kwa hisia zipi, hilo ni suala la kila mmoja katika nafsi yake na si vizuri tukakadiriana au tukasema nia ya fulani iko hivi, mimi nadhani hilo tuliache tuendelee na hoja iliyo mbele yetu hapa. *(Makofi)*

Hebu niifafanue, hoja iliyo mbele yetu tena hapa si kuingia kwenye hoja ya kama Mkataba wa Madini upo ama sijui una ubovu gani na kadhalika si hoja hiyo. Hoja hapa ni kama Mheshimiwa Kabwe Zitto amesema uongo kwa kumsingizia Waziri kwamba Waziri alilidanganya Bunge. Ndiyo hoja. Waheshimiwa naweza kuwachukulia hatua kali kabisa hatuna mchezo hapa. Endelea Mheshimiwa Dr. Slaa. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, sasa sina hakika muda wangu uliobaki lakini niendelee pale tu nilipokuwa nimefikia, nilikuwa narejea uzito wa Kanuni tunayoizungumzia. Kanuni tunayoizungumzia ina maneno mazito, hoja ya aina hiyo yaweza kutolewa bila taarifa na ikajadiliwa na kuamuliwa kama hoja nyingine yoyote.

Kwa hiyo, kimsingi hoja hii inaturejesha kwamba majadiliano yatakwenda kwenye utaratibu wa kawaida unavyotakiwa na majadiliano katika hoja yaani Kanuni ya 43.

Sasa kwa ajili ya muda tunakubali tu hapa tujadili katika dakika tano; lakini kimsingi ninachosema kinachosemwa kwamba kasema uonga hakuna ushahidi wowote

katika hotuba iliyotolewa hapa kwamba kasema uongo, wala hakuna ushahidi wowote kwamba Waziri alichosema ndicho sahihi. Kwa sababu tunahitaji kupima *document* mbili ambayo moja inaonyesha ndiyo ukweli na moja inaonyesha uongo, sasa hicho huwezi kukipata kwa kujadiliana kama tunavyofanya, ndiyo maana ninaomba kuwe na *document* hizo mahali na Bunge lako likubali kuwa na Kamati Ndogo au kwa maelekezo utakayotoa wewe, Kamati hiyo ichambue na ikushauri kama kuna uongo au hapana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, labda nirudie tena kilichopo mbele yetu hapa na alicholeta Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir ni kurejea kauli ya Mheshimiwa Kabwe Zitto ya tarehe 16 Julai, 2007 ambapo alimtuhumu Waziri wa Nishati na Madini wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwamba amelidanganya Bunge na kutokana na hilo Mheshimiwa Kabwe Zitto akaleta hoja hapa kujaribu kuthibitisha kwamba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini alilidanganya Bunge.

Waziri wa Nishati na Madini leo ameeleza mtiririko wote wa mchakato wa Mkataba wa Buzwagi. Sasa wawili wote mmewasikia na wengine mmechangia, sasa hapa jambo ni rahisi tu, je, Mheshimiwa Kabwe Zitto alisema uongo kwa kusema kwamba Mheshimiwa Waziri alilidanganya Bunge wakati ule na la pili haliishii hapo lazima ujibu, uongo huo ni mkubwa kwa maneno ya Kanuni ya 59 hapa uongo unatakiwa uwe mkubwa kiasi kwamba umeathiri heshima ya Bunge. Ndiyo hicho tunachosema sio ule uongo mdogo mdogo wa Kanuni ya 50 ule. Ni ule uongo ambao umeathiri heshima ya Bunge. Hilo ndilo mlijadili na mnipe maamuzi. Anayefuata Mheshimiwa Ponsiano Nyami.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii adimu ili nami niweze kuchangia hoja hii kwamba Waziri alilidanganya Bunge. Mheshimiwa Waziri si kwamba amelidanganya Bunge, bali Mheshimiwa Kabwe Zitto ndiyo ambaye amesema uongo unaoweza au ambao tayari umekwisha athiri heshima ya Bunge tayari. Anaposema Waziri amesema uongo na kwa matamshi yake mwenyewe alipokuwa anaelezea hoja yake amesema pia baadhi ya Mawaziri wamekuwa wakisema uongo hapa Bungeni, maana yake ni kwamba Serikali ndiyo imekuwa ikisema uongo na kwa sababu Kiongozi wa Shughuli za Bunge ni Waziri Mkuu anataka kumpaka pia Waziri Mkuu matope kwamba yeye ndiye anayesema uongo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ponsiano Nyami, jamani hebu tafadhalini turudi kwenye hoja. Ni fupi kabisa inahusu matamshi ya Mheshimiwa Kabwe Zitto ya tarehe 17 Julaim 2007 kwa sababu hayo ndiyo yametufikisha hapa na ndiyo siku aliyotoa taarifa kwamba ataleta hoja ya kuundwa kwa Kamati Teule. Sasa yale kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini aliona kwamba ameonewa kwa sababu kasingiziwa kwa kusemekana kwamba yeye alilidanganya Bunge kwa kutoa uongo huu ni hilo tu. Tusiende kwenye makando kando. Sasa tuseme juu ya Mheshimiwa Kabwe Zitto. Mheshimiwa Ponsiano Nyami hebu endelea.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa mwongozo huo. Kutokana na uthibitisho alioutoa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kulithibitishia Bunge na mpaka dakika ya mwisho, Bunge limekubali kwamba Mheshimiwa Waziri hakusema uongo, kwa hiyo, ni wazi kuwa Mheshimiwa Kabwe

Zitto, yeye ndiye ambaye ameweza kulidhalilisha Bunge kwa kusema maneno ya kashfa kwa Mheshimiwa Waziri ambaye amethibitisha ukweli kwamba hakulidanganya Bunge na kwa maana hiyo naunga mkono hoja kwamba Mheshimiwa Kabwe Zitto anastahili adhabu hiyo ili iwe funzo kwa kila Mbunge asiweze kusema maneno au kulidanganya Bunge. Naunga mkono hoja!

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nashukuru kwa kunipa hii nafasi.

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kulirejesha Bunge lako Tukufu katika Kanuni ya 50(1) ambayo inajieleza bayana hapa. Katika hii Kanuni, Bunge lako Tukufu nasikia linaendelea na *review*, ni Kanuni ambayo vile vile nadhani pengine itakuwa *reviewed*, kuhusu *the burden of proof* ilivyo hata katika sheria kwamba; kama kuna Mbunge ambaye anaona ya kwamba Mbunge mwingine anasema uongo…

Sasa anayetakiwa kuthibitisha ni yule anayedai kwamba huyo Mbunge amesema uongo au ni yule ambaye anasemekana amesema uongo? Hii kidogo ina *contradiction*, lakini ninachotaka ku-*prove* hapa ni kwamba ulichotuuliza Mheshimiwa Spika, ni nani anaunga mkono na nani anapinga na huo ndio utaratibu wa kawaida ambao kila siku tunaufuata hapa. *(Makofi)*

Sasa, kama ni hivyo basi, aliyeleta hoja ya kusema ya kwamba Mheshimiwa Kabwe Zitto aadhibiwe ni Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir na Kanuni aliyoi-*quote* ya 59(3) inayosema ya kwamba; "lakini endapo Mbunge mwingine yeyote ataona kwamba uongo uliosemwa na Mbunge huyo ni mkubwa kiasi cha kuathiri heshima ya Bunge, aweza papo hapo kutoa hoja kwamba Mbunge huyo asimamishwe kazi ya Ubunge kwa kipindi maalum." Sasa Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir ametoa hoja, lakini hiyo hoja yake hajaithibitisha, ndio maana hoja ya Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir bado iko *subject to 51* kwamba yeye Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir athibitishe kwamba Mheshimiwa Kabwe Zitto aliyoyasema yalikuwa ni ya uongo. Kwa hiyo, yeye anabeba *the burden of proof* kulingana na hii Kanuni ya 50(1). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ningeomba ya kwamba hili suala kwa sababu lilikuwa liko kwenye mchakato wa kawaida wa Kibunge, tungeacha, tuendelee na mambo mengine, badala ya kuadhibiana hapa. Lakini kama ni hivyo, basi Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir a-*prove* kwamba Mheshimiwa Kabwe Zitto amesema uongo na akishindwa ku-*prove* na yeye pia achukuliwe hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, mimi ya kwangu ni hayo! *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Hiyo ni upotoshaji tu, kwa sababu aliyeanza na hoja ya kutuhumu uongo humu ndani ni Mheshimiwa Kabwe Zitto ndiye alimtuhumu Waziri. Tuachoamua leo ni tofauti. Anachosema Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir ni kwamba, kauli ya Mheshimiwa Kabwe Zitto kwamba Mheshimiwa Waziri wetu wa Nishati na Madini alilidanganya Bunge, haikudhihiri na pengine ni uongo na kwa maana hiyo, ninalowaomba kuamua ni uongo mkubwa kwa mujibu wa Kanuni 59(3). Msilikwepe hilo, hilo ndilo lililopo mbele yetu. Sasa Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir yeye ameridhika hivyo. Sasa ni juu ya kila

mmoja wenu mliojiorodhesha kutoa maoni yenu. Kwa hiyo, namwita sasa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Masuala ya Bunge. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nami niungane na wenzangu ambao tunaunga mkono hoja hii ya kuweza basi kumpa adhabu mwenzetu ili iwe fundisho katika shughuli zetu za utendaji hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tu niseme kwamba Mheshimiwa Kabwe Zitto ni Mbunge kijana, hodari kama walivyo Wabunge wengine vijana kama vile Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar na wengine ambao kwa kweli wamekuwa na mchango mkubwa na kuwakilisha vijana ndani ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jamii na hasa vijana wetu waliopo shuleni, waliopo majumbani wamekuwa ni mashabiki wakubwa wa kuangalia Bunge letu katika vipindi mbalimbali na hasa vinavyorushwa hewani siku zote katika shughuli zetu na kwa kweli vijana wamekuwa ni mashabiki wa Wabunge Vijana walioko humu ndani. Sasa basi, kauli zinazoletwa na vijana Wabunge, tunategemea viongozi hawa wawe ndio *role model* kwa vijana wetu waliopo shuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hapa naomba lieleweke na wanaonisikia, hatuhoji Mheshimiwa Mbunge kuhoji Serikali yake na kutaka maelezo na kutaka ufafanuzi. Ninachohoji kama Mnadhimu Mkuu wa Serikali, nasimamia nidhamu, nahoji kauli ya Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amekuwa na matamshi ya aina kama hii, hii siyo mara yake ya kwanza. Mheshimiwa Mbunge wakati Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki anahitimisha hoja yake, Mheshimiwa Mbunge katika vifungu wakati wa Kamati ya Bunge Matumizi, alidiriki kusema kwamba, naomba ninukuu, nakumbuka alisema: "... Mheshimiwa Spika, nasikitika sana, Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, hawajui wanachokizungumza." Kauli hiyo, ilisikitisha Watanzania wengi.

Mheshimiwa Spika, wengi niliokutana nao, walisema hatukufurahia. Pale tulipokwenda Uwanja wa Jamhuri wakati wa mpira kati ya *NSSF* na Bunge, nilikutana na baadhi ya Watanzania waliokuwepo pale katika mechi na ninaweza kusema kwamba nilikutana na kijana mmoja ambaye ni mlemavu wa miguu, akaniambia, Mheshimiwa Waziri nilifurahi sana ulivyomsimamisha Mheshimiwa Mbunge yule, kauli yake haikuwa nzuri kabisa na watu wengi tulikasirika sana kwa jinsi alivyoweza kusema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mimi naomba niseme kwamba, Mheshimiwa Mbunge bado alikuwa na fursa leo hii kuweza kutoa kauli yake hiyo, kwa sababu gain, katika Kanuni za Bunge ya 59(3), inasema; "Mbunge yule anaweza akafuta usemi wake." Bado alikuwa na nafasi ya kufuta usemi wake leo hii wakati ahitimisha hoja yake hiyo. Lakini kwa makusudi kabisa, hakutaka kufuta, aliona kama vile itampunguzia heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tusimamie nidhamu, tufanye hili suala liwe ni suala ambalo litatoa fundisho kwa watu wetu ambao wanatusikiliza kule. Bunge isiwe mahali ambapo mtu atakuja tu kudiriki na kusema mambo ya kuudhi. Naomba ninukuu maneno aliyoyasema yalikuwa ni maneno makali sana na ni maneno ya kuudhi. Naomba nimnukuu Mheshimiwa Mbunge akitoa taarifa ya kutoa hoja yake hiyo, alisema: "Mheshimiwa Spika, kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri kuhusiana na Mkataba mpya wa Mgodi wa Buzwagi ambao Mheshimiwa Waziri ameeleza maelezo ambayo siyo sahihi, amedanganya na ameeleza vitu ambavyo kwa kweli siyo ambavyo vipo katika mkataba huo."

Mheshimiwa Spika, Mbunge angeweza kusema maneno haya haya bila kumtuhumu Mheshimiwa Waziri amesema uongo na tusingefika hapa leo. Angeweza kusema tu Mheshimiwa Spika, mimi naomba kutoa hoja ya kumtaka Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi wa kina kuhusu mkataba huo aliousaini huko Uingereza. Hii ingetosha! *(Makofi)*

Lakini anapokwenda na kumtuhumu Mheshimiwa Waziri, amedanganya, amesema mambo yasiyo sahihi, Waziri ni kiongozi katika jamii, kiongozi ambaye ana heshima siyo tu hapa Tanzania, lakini kwa watu wote ambao wanafanya naye kazi, viongozi wa nchi za nje, Mawaziri wenzake *(counterparts)* katika nchi zingine wanatakiwa waone kwamba Mheshimiwa huyu anapata heshima katika nchi yake. Sasa pale tunapoanza kumburuza Mheshimiwa Waziri na kuonyesha kwamba Mheshimiwa Waziri ni muongo kabla hata hatujampa nafasi ya kutoa hayo maelezo, kwa kweli hiyo haikuwa nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba tu niseme kwamba maneno aliyoyasema Mheshimiwa Mbunge, mimi nasema ni mazito, yameudhi na yamemsononesha Mheshimiwa Waziri. Naomba kusema kwamba adhabu hiyo, naunga mkono itolewe. Asante sana. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii, lakini kwa heshima zote kabisa, naomba niseme kwamba msemaji aliyenitangulia sasa hivi amenifilisi yale yote niliyotaka kusema na kwa misingi hiyo, sioni sababu ya kuchelewesha shughuli za Bunge lako, bali naunga mkono hoja iliyotolewa. *(Makofi)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kimsingi naungana na waliotangulia kwamba maneno yaliyokuwa yamezungumzwa na Mheshimiwa Kabwe Zitto, yalikuwa ni maneno ambayo hayaridhishi na ninaona kuna uongo ndani yake kutokana na hasa pale aliposema kwamba mkataba unaonekana uko tofauti kwa maana kwamba alikuwa anaongea kama mtu tayari alishaona mkataba, kumbe baadae tumekuja kugundua kwamba alikuwa bado katika kuomba mkataba. Kwa hiyo, mimi naona hiyo ni uongo. Lakini, kwa sababu kwa sisi tunaoamini Biblia, inasema kwamba Mwenyezi Mungu alipoudhika na Godoma…

**SPIKA:** Siyo Dodoma! *(Kicheko)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, Sodoma na Gomora, alipokuwa amesikitishwa, amewatuma wale malaika, lakini kuna waliokuwa wanahuzunika, wakaomba kama unaweza ukapataikana msamaha. Akasema hata wangekuwa watano, ningesamehe. Akashuka mpaka akatokea Bwana Rutu na familia yake. Sasa na mimi najiuliza, katika yale yote ambayo kijana huyu Mbunge anayachangia, je, hatuwezi kuona hata moja ambalo ni jema?

Kwa hiyo, ninaomba kwamba badala ya kumsimamisha kwa sababu Chama cha Mapinduzi, sasa niko kwenye siasa ndicho kilichosababisha kuwa na Vyama vya Upinzani, kilikubali chenyewe kwamba tuwe na hali ile ya kubadilishana mawazo, kwa hiyo, kwa misingi hiyo kwa kutumia nafasi hiyo ya Chama, naomba siyo nia yangu kupingana na hali iliyopo, nina uchungu sana na mambo yaliyojitokeza, lakini naomba kama kuna uwezekano wa kupunguza adhabu hiyo, basi nitakuwa nimefarijika zaidi. Ahsante!

**SPIKA:** Pendekeza adhabu mbadala, ndio Kanuni zinavyosema!

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, adhabu mbadala ninayoiona ni yeye kusema kwamba hatarudia tena kusema maneno kama hayo Bungeni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Naona hiyo, haikuungwa mkono!

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Mimi nina mambo mawili tu. *(Makofi)*

*(Hapa minong'ono ya Waheshimiwa Wabunge ilisikika)*

**SPIKA:** *Order, order,* tusikilizane. Tumsikilize mwenzetu.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Spika, suala la mwanzo ni kwamba je, ile kauli ya Mheshimiwa Kabwe Zitto aliyozungumza ya kusema kwamba alimtuhumu kwamba alidanganya, je, kauli hii kuna athari yoyote katika kulivunjia heshima Bunge letu? Nafikiri hili ndilo suala ambalo ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, sasa tukitizama katika Katiba, Kifungu cha 63(2), moja ya kazi za Bunge ni kusimamia Serikali na unaposimamia Serikali, unapokuwa na *honest belief* kwamba kuna kitu ambacho kimefanyika na *honest belief* ile ukaitoa katika Ukumbi huu wa Bunge, hiyo ni kuonesha kwamba unataka kujua hali ya Serikali inavyotendeka. Kwa hiyo, mimi nasema kwamba Mheshimiwa Kabwe Zitto alikuwa na *honest belief* ingawa baadaye ilitolewa na kuonekana kwamba siyo kweli, hizo ni moja katika kazi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ikiwa kila mtu atakuja hapa, atakuwa na *honest belief,* atasema kitu, halafu kikaonekana kwamba *honest belief* ile si kweli, tukamtia adhabu, Bunge lako Mheshimiwa Spika, ninaweza kusema kwamba litakuwa ni *rubber stamp,*

litataka kila mtu anayesema ndio hicho hicho kiungwe mkono, kitu ambacho kitakuwa ni kinyume kabisa na haki za Wabunge na utaratibu wa Bunge kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa maana hiyo, mimi nahisi maelezo aliyoyazungumza Mheshimiwa Kabwe Zitto hayajaathiri heshima ya Bunge katika mantiki ya kufanya kazi. Kwa maana hiyo, mimi ningeshauri kwamba Mheshimiwa Kabwe Zitto ni kuonywa tu kwamba yale maneno aliyoyatumia yalikuwa ni mazito kidogo, basi mara nyingine angalau atumie maneno laini. Lakini ninachoogopa ni kwamba ikiwa kila mtu anatoa maelezo kwa *belief* katika roho yake kusema kwamba hiki ninaamini kwamba kimefanyika, kikawa *proved* kwamba hakikufanyika, halafu tukampa adhabu, Bunge lako litakuwa ni *rubber stamp* ambayo hiyo siyo kazi ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru! *(Makofi)*

**SPIKA:** Nifafanue tu, haki ya kusema au kuchangia humu Bungeni inalindwa na Katiba. Lakini Katiba hiyo hiyo ambayo imeturuhusu kuunda Kanuni, imeweka mipaka ya namna ya kuitumia haki. Kwa hiyo, uangalifu kuhusu lugha umesisitizwa sana humu, ndiyo maama mnaona Mabunge ya wenzetu watu wanatupiana viti, watu wanapigana ngumi kama Bunge la Italia ilitokea mwaka jana, kauli ikiwa mbaya tutashindwa. Sasa mimi nataka mjielekeze hapo tu. Siyo suala la haki, haki ya kusema ipo. Lakini, sasa nini kinasemwa, wakati gani, kwa ushahidi upi, ndio suala lenyewe hilo. Kwa hiyo, tuendelee. *(Makofi)*

**MHE. ADAM K. A. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, naomba niseme yafuatayo katika hoja hiyo. Kwanza kabisa, naomba niseme kwamba labda sisi wengine tunamfahamu Mheshimiwa Kabwe Zitto kuliko wengine kwa sababu tunapata fursa ya kukaa naye kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi na pale taratibu za mjadala ni tofauti na hizi, kwa hiyo, tunaufahamu mchango wake, tunaufahamu uwezo wake na katika hili ambalo linaamuliwa, hakuna mtu anayeweza kusema kwamba kuna mtu ana-*doubt* kuhusu uwezo wake.

Mheshimiwa Spika, lakini tunachosema, umesema wewe imeathiri heshima ya Bunge. Sasa umenitangulia kidogo, lakini mimi nilitaka kusema wale wanaokwenda mbali huko Italy na Japan na Israel, Kenya tu hapa! Walikuja Wabunge wa Kenya kwenye Kamati ya Fedha wiki iliyopita, wamekaa kule juu. Tulivyokutana nao *Dodoma Hotel* jioni yake, wanasema *your Parliament is very civilized,* Wabunge wa Kenya tu hapo! Sasa sisi tunachosema ni kwamba ile *civilized nature* ya *Parliament* yetu inatokana na kuheshimiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kaka yangu Waziri Mkuu anajua, katika watu wanaoihoji Serikali wanapopata nafasi, mimi ndiye ninakuwa wa kwanza. Lakini ukitaka kuihoji Serikali, uihoji kwa taratibu na nidhamu ambazo sisi katika Bunge hili tumejiwekea. Suala linaloingia hapa siyo kuihoji Serikali, suala linaloingia hapa ni kumvunjia heshima Waziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunajiuliza je, yale maneno ya kumwambia amelidanganya, amelipotosha na yeye ni Waziri, ana nafasi yake. Kwa hiyo, na magazeti yakalichukulia hapo na watu wengine na kusema kweli mimi naungana na Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir anaposema kwamba Mheshimiwa Waziri amedhalilishwa na kauli hiyo na baada ya kudhalilishwa Mheshimiwa Waziri kwa nafasi yake na kwa kauli yake kwa kuwa ameisema Bungeni, kumtuhumu kwamba amesema maneno yale ndani ya Bunge ni kulivunjia heshima Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nakubaliana na adhabu ya Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir na naomba isiwe hiyo tu, kuna mwingine amenong'ona viwe vikao vinne.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi ni katika watu ambao tutaathirika na kutokuwepo kwake kwa sababu tunamhitaji sana kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi. Lakini hatuhitaji watu ndani ya Bunge hili ambao watakuwa hawana nidhamu kiasi cha namna hii.

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja ya kaka yangu Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niseme machache.

Mheshimiwa Spika, mimi nashindwa kusema kwamba kasema uongo na huo uongo kwamba ni mkubwa. Amehoji mkataba kusainiwa London na ni kweli na hakuna aliyekwishakwenda kuona kwamba yale yalikuwa safi au hapana. Yote aliyoyasema, nadhani wengine tumesema si kweli, hapa tumegawanyika. Kuna aliyesema ni kweli, lakini na sisi tukasema si kweli. Lakini, yeye alileta hoja, katoa taarifa kwamba nitakuja nitaleta hoja. Hoja ameileta, kama inaonekana ameshindwa, hivi shitaka linazua lingine pale pale? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Phares Kabuye, unaturudisha nyuma. Tunafuata Kanuni. Kesho na kesho kutwa tutazungumza upungufu na jinsi ya kuboresha Kanuni zetu. Sasa hapo unaweza kuyazungumza na tukarekebisha. Lakini sasa hivi hizi ndio Kanuni tulizonazo hazijabadilishwa na Kanuni ya 59(3) inamruhusu Mbunge bila taarifa kusimama na kutoa hoja kwamba Mbunge mwenzie aadhibiwe kwa kiwango ambacho atakitaja kwa sababu alichokifanya au kukinena kabla huyo mhusika, Mbunge kimeathiri heshima ya Bunge. Sasa wewe jadili hilo.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza mtu si mahakamani, lakini mtu anaweza akajiuliza Bunge ni Waziri? Waziri anaweza akasema nimevunjiwa heshima, akatoa hoja, maana ya Bunge ni nini? Kamsema mtu na mtu huyo hajalalamika, sasa kavunjia Bunge heshima namna gani?

Mheshimiwa Spika, lakini naomba tu niseme kwamba uamuzi wa watu wengi unakuwa hivyo kwa sababu, utanisamehe, wakati najifunza *literature,* nakumbuka mambo ya *Socret,* alisema (msinichukulie kwamba nawasema) kwamba; "ninyi

mwafanya hivyo mkifikiri kwamba mtakwepa kutoa hesabu ya maisha yenu, bali mimi nawaambia kwamba matokeo yatakuja kinyume chake, watu wengi watawataka kutoa hesabu ya maisha yenu nao watakuwa vijana zaidi kuliko mimi na ninyi mtawakasirikia sana."

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, uamuzi wa wengi, aliposema hiyo, wakampigia kura, alipojaribu kujieleza, hata kura zikapungua. Kwa hiyo, uamuzi wa namna hiyo, ninaomba kama ingekuwa Kamati ikakaa, ikachekecha, tungepewa kwamba kweli ukubwa wa uongo unalingana na huu au uongo haupo. Lakini kwa sababu ni umati, uamuzi wa watu wengi, eeh, hapa ni mambo mengi. Kwa hiyo, mimi ninaomba mwisho kwamba angepewa fursa ya kutafuta hivyo vielelezo, inawezekana hakujua kwamba mambo yangelifika hapa. Nakushukuru sana!

**SPIKA:** Kabla sijamwita Mheshimiwa Mbunge, Mzee Malecela, ninapenda kuuliza kama Mheshimiwa Kabwe Zitto anapenda kusema kitu chochote katika mchakato wote huu kwa sababu hakujiorodhesha kusema, pengine anacho cha kuongea. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, *I am a democrat*. Niko tayari kwa maamuzi yoyote Bunge litakayochukua! *(Makofi)*

**MHE. DR. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa nichukue fursa hii kusema naunga mkono hoja ambayo imetolewa na ndugu yetu Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir. Naunga mkono hoja hii na ninataka niseme hili kwa uchungu sana kwamba Bunge hili lazima liwe Bunge lenye heshima ambayo tumeachiwa tangu miaka mingi iliyopita. Mimi sijapata kukuta *debate* ikawa kama ya leo na lilipoanzia, kwanza yeye alianza kusema Waziri amelidanganya Bunge hili. Sasa wengine tunajaribu kusema labda tunasema Mheshimiwa Nazir Karamagi, hapana, siyo Karamagi, ni Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili alilolisema, kwanza limemdhailisha Waziri, limeidhalilisha Serikali, pili, linaleta hisia kwamba Mawaziri wa Chama cha Mapinduzi waongo na wana-CCM, tukumbuke, tunapoapa tunasema kwamba nitasema kweli…

**WABUNGE FULANI:** Daima.

**MHE. DR. JOHN S. MALECELA:** Hapa tumeona Mheshimiwa Nazir Karamagi akaisema kweli na wote hapa katueleza na tukaamini na tukakubali kwamba kweli hakudanganya Bunge hili. Kwa hiyo, mimi ningependa kwamba katika hili tusiwe na huruma kwa sababu wanasema mdharau mwiba ataota nini?

**WABUNGE FULANI:** Tende.

**MHE. DR. JOHN S. MALECELA:** Sasa huu mwiba tuuondoe leo. Wengine watasema kwamba ooh, labda hii itampa sifa kwa watu, hapana! Tusipomuadhibu, kwa watu itaonekana Serikali ya CCM, Mawaziri wa CCM wanasema uongo kwenye Bunge ambayo si kweli. Hii ni Serikali ambayo imechaguliwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, Serikali tunayoiamini chini ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa na

kweli, tuseme kweli kwamba Serikali yetu kila mara inajitahidi. Mawaziri wanapojibu hapa, wanajitahidi kweli kweli, kutoa mambo ya kweli na wakiona haitoshi, huwa wanasema au tuwafuate tuwaongezee au wanasema watatuandikia barua baadaye. *(Makofi)*

Makeshimiwa Spika, kwa kweli baada ya kusema hayo, mimi ningewaomba Wabunge wote pamoja na hata Wapinzani kwamba….shauri yenu, mimi mradi naomba tu, cha hakika sibembelezi! Ila ninachosema yeyote atakayepita katika njia ambayo Mheshimiwa Kabwe Zitto amepita, lazima tumuadhibu na kwa hiyo, nakubalina na hoja ya Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir kwamba Mheshimiwa Kabwe Zitto, aadhibiwe na ni leo. Ahsante! *(Makofi)*

**SPIKA:** Kabla sijamwita mtoa hoja, nalazimika nifafanue hii adhabu imekaa kaaje kama ndiyo itaamuliwa. Tukiamua Waheshimiwa Wabunge leo kwamba imethibitika kuwa Mheshimiwa Kabwe Zitto alimsingizia Waziri wa Nishati na Madini na kwa hiyo alisema uongo, maana yake hatashiriki kwa mujibu wa Azimio ama hoja iliyoletwa na Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, hataruhusiwa kushiriki shughuli za Bunge kuanzia Azimio litakapochukuliwa na adhabu hiyo itaendelea kwa maana ya Vikao vya Bunge na Kamati zake hadi mwaka ujao. Ndio, kwa sababu na mkumbuke Mkutano wa Januari ni wa wiki tatu na Kamati zake wiki mbili na kwa kipindi chote hicho atakuwa…ni Novemba, ndio, ni mwezi Novemba samahani. Hatuna Mkutano mwingine mpaka Januari mwaka ujao.

Adhabu ikichukuliwa inayohusu Mkutano huu na ujao, si ndio alivyosema! Maana yake huu na ule wa Novemba. Mimi naifafanua tu adhabu ili tuielewe. Kwa hiyo, adhabu ni kwamba arejee Januari mwakani, au sivyo? …huku akilipwa nusu mshahara na bila posho. Sasa, basi mmeiona uzito wake na wakati huo huo sauti ya wananchi wa Kigoma Kaskazini iwe kama imezima. Sasa ni zito, mimi niseme tu kuna nafasi hapo ya marekebisho, inaruhusiwa kabisa. Kuna nafasi ya marekebisho na ningemuomba Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir kulitazama hilo kama inawezekana.

Mimi ndiye ninayeongea sasa, kuguna wala hakusaidii, vinginevyo wewe mwenyewe ndiye unaweza kupata matatizo bure, ndio taabu ya kiti hiki. Kwa hiyo, mtulie ninapotoa maelezo, kwa sababu ipo Kanuni nayo ambayo ukionyesha dharau kwa Spika, yatakupata makubwa kuliko ya Mheshimiwa Kabwe Zitto. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir unayo nafasi ya kupendekeza kwa sababu wewe ndiye mtoa hoja, kwa kuzingatia uzito huo niliousema. Kwa hiyo, namwita sasa mtoa hoja! *(Makofi)*

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, niliipenda sana hekima yako ya kumtaka Mheshimiwa Kabwe Zitto kama ana lolote aseme, nilijua kwa utu uzima wako ulikuwa unakusudia nini. Kwa bahati mbaya sana amesema yeye ni *democrat*, litakalotokea na litokee.

Katika mazingira kama hayo, mimi nashindwa kubadilisha msimamo wangu. Kwa hiyo, nimalizie kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuunga mkono hoja yangu na wale ambao hawakuunga mkono, wote wamekuwa

wakitimiza wajibu wao wa kidemokrasia. Ningependa na mimi vile vile nithibitishe kuwa ni *democrat*.

Kwa hiyo, nayameza maamuzi yangu haya kwa uchungu mkubwa, lakini sina njia nyingine ya kusaidia heshima ya Jimbo langu. Ahsante sana!

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja! *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyo mbele yetu iliyoletwa na Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, ni kwamba Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini katika matamshi yake ya tarehe 16 Julai, 2007, alimsingizia Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwamba amelidanganya Bunge na hivyo kumfanya yule Waziri aonekane ni mwongo.

Nilimpa nafasi kuleta hoja hapa ya kuunda Kamati Teule, ameileta, Bunge hili limeikataa baada ya kuridhika na maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwamba hakuna haja kwa sababu maelezo hayo yamejitosheleza na bado kuna nafasi ya kupata hata makala nyingine za maelezo zaidi. Kwa hiyo, sasa hoja iliyo mbele yetu kutokana na hilo ni hiyo ya Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir kwamba sasa Mheshimiwa Kabwe Zitto, kwa kosa hilo alilotenda, asimamishwe chini ya Kanuni ya 59(3) kwa kipindi chote cha Bunge hili kilichosalia na Mkutano wa Tisa. Sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliafiki hoja ya kumsimamisha kazi za Ubunge Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto kwa Mkutano wa Nane na wa Tisa wa Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, natamka kwamba Mheshimiwa Kabwe Zitto, amesimamishwa shughuli za Ubunge kuanzia sasa hadi Mkutano wa Januari mwaka ujao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sina mengi zaidi ya kusema imekuwa ni siku ndefu. Nadhani wote tumejifunza kutokana na yote yaliyotokea. Kwa hiyo, sasa naliahirisha Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 02.05 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano, Tarehe 15 Agosti, 2007 saa tatu asubuhi)*